

MAFUNZO YA HUKMU ZA IBADA

**Kwa mujibu wa Fat'wa za Ayatullah Al-Udh'ma
Sayyid Al Husseini Khamenei (M.A)**

Kimeandikwa na:
Muhammad Ridha Mushfiq Pur

Kimetarjumiwa na:
Hazrat Zahraa Foundation





© **Haki ya kunakili imehifadhiwa na:**
AL-ITRAH FOUNDATION

ISBN: 978 - 9987 - 512 - 74 - 4

Kimeandikwa na:
Muhammad Ridha Mushfiq Pur

Kimetarjumiwa na:
Hazrat Zahraa Foundation

Kimehaririwa na:
Jopo la wahariri

Toleo la kwanza: Agosti, 2010

Kimepangwa katika Kompyuta na:
Hajat Pili Rajabu

Kimetolewa na kuchapishwa na:
Al-Itrah Foundation
S.L.P 19701 Dar es Salaam -Tanzania
Simu: +255 22 2110640
Simu / Nukushi: +255 22 2127555
Barua Pepe: alitrah@raha.com
Tovuti: www.alitrah.org
Katika mtandao: www.alitrah.info

YALIYOMO

Shukrani.....	1
Utangulizi.....	k
Taqliid (1-3).....	2
Wilayatul Faqiih na Uongozi.....	15
Utangulizi wa Twahara.....	20
Maji.....	21
Hukmu za kwenda Haja.....	25
Najisi	28
Vinavyotwahaarisha	37
Wudhu	45
Ghusli	60
Hukmu za Maiti	72
Tayammam.....	82
Masharti ya Tayammam.....	85
Aina za Swala.....	88
Vazi la mwenye Kuswali (1).....	90
Vazi la mwenye Kuswali (2).....	93
Sehemu ya kuswalia (1).....	95
Sehemu ya kuswalia (2).....	97
Hukmu za Msikiti (1)	99
Hukmu za Msikiti (2)	100
Kibla.....	102
Swala za Kila Siku (1- 20).....	105
Swala za Wajibu.....	169
Swala ya Jamaa (1)	172
Swala ya Jamaa (2)	174
Swaumu (1-8).....	179

Khumsi.....	207
Khumsi inayotokana na Faida.....	210
Khumsi ya Faida (1).....	213
Khumsi ya Matumizi.....	216
Khumsi ya Faida (2).....	219
Khumsi ya Mapato (1).....	223
Khumsi ya Madini.....	225
Ngawira.....	229
Jihad.....	230
Kuamrisha mema na kukataza maovu (1).....	233
Kuamrisha mema na kukataza maovu (2).....	234



Neno la Mchaphaji

Kitabu kilichoko mikononi mwako ni tarjuma ya kitabu cha Kiarabu kiitwacho, *Ta'limu 'l-Ahkaam (al-'ibadaat)* kilichoandikwa na Muhammad Ridha Mushfiqpur. Sisi tumekiita, *Mafunzo ya Hukmu za Ibada*.

Kitabu hiki kimekusanya mafunzo mbalimbali yanayohusu ibada na namna ya kuzitekeleza ibada hizo kwa mujibu wa fatwa za Ayatullah Sayyid Ali Khamenei, Kiongozi Muadhamu wa Mapinduzi ya Kiislamu ya Iran. Mwandishi amekusanya mafunzo haya kutoka kwenye kitabu kiitwacho *Rislatu Aj'wibatu 'l-Istifta'aat* cha Ayatullah Sayyid Ali Khamenei. Ndani ya kitabu hiki utakuta taratibu za kufanya ibada zimepangwa kwa mpangilio mzuri kwa ajili ya msomaji kuweza kujifundisha na kuzingatia maudhui yake.

Mwandishi wa kitabu hiki amefanya juhudi kubwa kuhakikisha kwamba msomaji anapata kile alichokikusudia.

Tumekiona kitabu hiki ni chenye manufaa sana, hususan wakati huu wa maendeleo makubwa ya elimu katika nyanja zote, ambapo kila mtu ana kiu ya elimu na kutaka kujua kile anachokiamini kwa usahihi na bila upotoshaji.

Kutokana na ukweli huo, Taasisi yetu ya Al-Itrah Foundation imeamua kukichapisha kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili kwa madhumuni yake yaleyale ya kuwahudumia Waislamu, hususan wazungumzaji wa Kiswahili.




Tunakishukuru kikundi cha wanawake wa Hadhrat Zahra Foundation kwa kukubali jukumu hili la kukitarjumu kitabu hiki. Vilevile tunawashukuru wale wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwake.

Ni matumaini yetu kwamba kitabu hiki kitakuwa ni chenye manufaa makubwa kwa wasomaji wetu.

Mchapishaji:

Al-Itrah Foundation

S. L. P. 19701, Dar-es-Salaam.



SHUKRANI


Ninamshukuru Allah (s.w.t.), na kwa Baraka za Mtukufu Mtume wetu Muhammad (s.a.w.w.) na Watukufu Ahlul-Bait (a.s.), kwa kutujaalia kuweza kufanikisha nia yetu ya kuchapisha kitabu hiki "Mafunzo ya Hukmu za Ibada".

Kitabu kilichopo mikononi mwako ni kile ambacho kimeandikwa na Muhammad Ridha Mushfiq Pur na kutarjumiwa na Hazrat Zahra Foundation, kwa jitihada zao hizi na nyingine Mwenyezi Mungu awalipe malipo mema hapa duniani na kesho huko Akhera.

Natoa shukrani za dhati haswa kwa Al-Itrah Foundation kwa kukubali kukittoa na kukichapisha kitabu hiki, pia natoa shukrani kwa kikundi cha wanawake wa Hazrat Zahra Foundation kwa kukitarjumu kitabu hiki na wale wote ambao kutokana na juhudi zao kitabu hiki kimeweza kuwafikia wasomaji wetu, si rahisi kumtaja kila mmoja aliyeshiriki kuifanya tarjuma hii mpaka kukamilika, ila Allah (s.w.t) peke yake ndiye atakayewalipa malipo mema Inshaallah.

Sababu zilizonifanya nisimamie kazi hii ni kutaka wale watu wazungumzao kiswahili (wasiojua Hukmu za Ibada) waelewe na kufahamu "Mafunzo na Hukmu za Ibada" ili wafanyapo ibada zao wafanye kwa njia sahihi.

Ni matarajio yetu kuwa kitabu hiki kitakuwa ni mwongozo mzuri utakaomwezesha msomaji endapo atayafuata mafunzo yaliyomo barabara kufikia darja ya juu ya ucha Mungu.



Ninamuomba Allah (s.w.t.) aikubali kazi hii na iwe ni yenye manufaa kwa wasomaji wote wa kitabu hiki
Aamin.

Mostafa Ranjbar Shirazi
Mkuu wa Kituo cha Utamaduni cha
Ubalozi wa Jamhuri ya Kiislamu ya Iran,
Dar es Salaam-Tanzania
Barua Pepe: ranjbar85@yahoo.com



UTANGULIZI

Kitabu kilicho mkononi mwako hivi sasa kimekusanya maelezo yanayohitajika kiibada kulingana na fat'wa za Ayatullah Ali Khamenei. Japokuwa mas'ala yanayohusu ibada ni mengi, lakini hapa tumetaja yale tu yanayotumika mara kwa mara katika maisha ya kila siku. Kwa mapenzi ya Allah (s.w.t) tuna imani kuwa siku za usoni tutayaongeza ili tuyakamilishe kwa ajili ya wale wanaohitaji elimu ya juu katika hukmu za dini.

Kitabu hiki kimepangwa na kuandaliwa kwa ajili ya kufundishia ambapo kina sehemu nane zenye jumla ya masomo sabini na saba. Na katika kila somo kuna zoezi la maswali sita, ambapo jumla ya maswali mia nne sitini na mbili na tahqiqi (changamoto) sabini na saba. Majibu mengi ya tahqiqi yanaweza kupatikana katika kitabu kiitwacho *Rislatu Aj' wibatul-Istiftaat* cha Ayatullah Ali Khamenei, kilichochapishwa na Alhuda chapa ya kwanza, na kinapatikana katika ofisi za Ayatullah Ali Khamenei.

Jitihada kubwa imefanyika kuhakikisha kwamba kitabu hiki, kinakuwa katika hali ya usahihi, lakini tunakaribisha maoni ili kuweza kupata uyakinifu zaidi.


Mwisho tunaishukuru Ofisi ya Ayatullah Ali Khamenei, Taasisi ya Kitamaduni ya Amin, Taasisi ya Imam Khomeini, na Taasisi ya uchapishaji ya Miithaq ambao kwa pamoja wamefanya juhudi katika upangaji na hatimaye kuchapisha kitabu hiki.




Ni matumaini yetu kuwa, hatua hii japo kidogo, itawanufaisha wale wote wanaomfuata kiongozi huyu na wenye nia ya kuifahamu fiq'hi (sheria), na iwe ni chumo letu katika akhera.


Ewe Mola mfikishie salamu Mtume wetu Muhammad (s.a.w.w) na kizazi chake kilichotwahaika, na utuwezeshe kuinusuru dini hii ya haki na kuyafuata mafunzo yake. Ifanye faraja ya Imam wa zama (zetu) iwe karibu.

Amin

Muhammad Ridhaa Mushfiq Puur
13/ Rajab Murajab/ 1424.













Sehemu ya Kwanza

TAQLIID



Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Somo la Kwanza

TAQLIID (1)

1. Utangulizi
2. Njia za kuzifahamu Hukmu
3. Aina za taqliid
4. Kutenda bila taqliid

1. Utangulizi

Ni jambo la wajibu kwa kila mtu aliyefikia umri wa kuwajibika kwa mujibu wa sheria, (mukallaf) kujifunza mas'ala ya kisheria yanayo muwajibikia kuyatenda mara kwa mara; mfano: swala, swaumu na baadhi ya matendo (muamalaat) na mengineyo. Na ikiwa kwa kutojifunza hukmu hizo kutamsababishia kuacha mambo ya wajibu na kuingia katika haramu, basi atahesabika kuwa ni muasi.


Mukallaf

Ni mtu mwenye kutimiza masharti ya kuwajibika kwa mujibu wa sheria, ambayo ni:

- a. Balegh
- b. Akili
- c. Uwezo

Alama za balegh ni moja kati ya mambo matatu:

- a. Kuota nywele katika sehemu za siri chini ya tumbo.
- b. Kuota usingizini na kutokwa na manii.
- c. Kutimia miaka kumi na tano kwa kufuatana na kalenda ya Kiislamu kwa mvulana na miaka tisa kwa kufuatana na kalenda ya Kiislamu kwa msichana.



Taqliid

Tendo la kujamiiana ikiwa halikuambatana na utokwaji wa manii si dalili ya balegh, lakini linawajibisha joshu la janaba. Na ikiwa joshu hilo halikufanywa, basi ni lazima lifanyike wakati ambao mtu atafikia umri wa balegh.

Mtu hawezi kuhesabika kuwa ameingia katika balegh ikiwa hazijathibitika juu yake alama za balegh, kwa hivyo hakutokuwa na taklif juu ya hukmu za kisheria.

Hali ya uwezekano wa kudhihiri nywele (sehemu za siri) au kuota ndoto (ya kujamii) haitoshi kumfanya mtu kuwa mukallaf kabla ya umri wa taklif (yaani kutenzwa nguvu na sheria).

Damu anayoiona msichana kabla ya kutimia umri wa miaka tisa kwa kufuatana na kalenda ya Kiislamu haihesabiwi kuwa ni katika alama za balegh.

Kama kuzaliwa kwa mtoto kulihesabiwa kulingana na kalenda ya miladiya (AD), italazimu kufanya mahesabu ya tofauti kati ya mwaka wa miladiyya na mwezi mwandamo (AH) ili kujua alizaliwa katika tarehe gani ya mwezi kwa kufuatana na kalenda ya mwezi mwandamo, (kila mwaka wa kalenda ya mwezi unatofautiana kwa idadi ya siku na mwaka wa Miladiyya).

2. Njia za kuzitambua hukmu

Ili kujua hukmu mbalimbali za kidini, mukallaf anatakikana kutumia mojawapo ya njia zifuatazo:

- a. Ijihad.
- b. Ihtiyat.
- c. Taqliid.

a. Ijtihad

Ijtihad ina maana ya kutoa hukmu za kisheria kutoka katika vyanzo mbali mbali vinavyokubalika na vilivyothibitishwa na wanachuoni kwa mujibu

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

wa dini ya Kiislamu.

Mtu aliyefikia darjaa ya ijihad anaitwa **mujtahid**.

b. Ihtiyat

Ihtiyat ina maana ya kutekeleza mambo ya wajibu ya dini kisheria kwa njia ambayo haitabakia shaka katika usahihi wa utekelezaji.

Kwa mfano kuliacha jambo ambalo baadhi ya maulamaa wanaliona ni haramu na wengine hawakuthibitisha uharamu wake, au kutekeleza jambo ambalo baadhi ya maulamaa wameliona ni wajibu hali ya kuwa wengine hawakuthibitisha uwajibu wake.

Mtu aliyefikia daraja ya ihtiyat anaitwa *muhtaata*.

c. Taqliid


Taqliid ni kule kutekeleza mambo ya wajibu katika dini kwa kuzingatia fat'wa na hukmu zinazotolewa na mujtahid aliyekamilisha masharti ya kuwa mujtahid.

Mtu anayefanya amali zake (matendo ya ibada) kwa taqliid anaitwa **muqallid**.

Mtu ambaye hana elimu katika maswala ya hukmu za dini, ni vyema akafanya mambo yaliyo wajibu kwake kisheria kwa kuzingatia fat'wa za mujtahid.

Ikiwa mukallaf hakuweza kuwa mujtahid, basi afanye taqliid au afanye amali zake kwa ihtiyat. Na kwa kuwa ihtiyat inalazimu kuwa na upeo mkubwa kielimu ni vyema mukallaf akafanya amali kwa kumfuata mujtahid. Kwa hali hiyo, taqliid ni wajibu kwa mtu ambaye ni:

- a. Mukallaf.
- b. Si mujtahid.
- c. Si mwenye uwezo wa kufanya Ihtiyaat.



Taqliid

3. Aina za taqliid ya mujtahid aliyekufa

Kumfuata mujtahid aliyekufa kumegawanyika katika sehemu mbili:

a. Kwanza

Yaani kufanya taqliid kwa mara ya kwanza. Mtu anayeanza kufanya taqliid haifai kwake kumfuata mujtahid ambaye ameshafariki.

b. Kuendelea

Yaani kuendelea kubaki katika kufuata taqliid ya mujtahid aliyekwisha fariki na alikuwa akifanya taqliid yake zama za uhai wake.

Inafaa kwa mtu kuendelea kumfuata mujtahid ambaye amekwisha kufa. Ikiwa alikuwa muqallid wake katika uhai wake hata katika mas'ala ambayo mukallaf alikuwa hajawahi kutumia fat'wa za mujtahid huyo.

Katika kuendelea kufuata taqliid ya mujtahid aliyekufa, hakuna tofauti baina ya kuwa mujtahid huyo alikuwa mjuzi kuliko wengine au hapana. Mukallaf anaweza kubaki katika taqliid ya mujtahid aliyekufa au anaweza kuanza taqliid kwa mujtahid aliyekufa ikiwa itaendana na mujtahid aliye hai.

Ikiwa kubaki katika taqliid ya mujtahid aliyekwisha fariki ni jambo ambalo limeafikiwa na wanachuoni wote wa zama hizo, basi hakuna lazima katika jambo hilo kumreja mujtahid aliye mjuzi zaidi.

Mtu ambaye hakuwa mukallaf katika uhai wa mujtahid, lakini alikuwa akimfuata kwa njia sahihi, basi inafaa kwake kubakia kwenye taqliid yake baada ya kufariki kwa mujtahid huyo.

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Yeyote mwenye kumfuata mujtahid fulani, na baada ya kufariki kwake akamfuata mujtahid mwingine katika baadhi ya mas'ala, kisha mujtahid huyu naye akafariki, basi inawezekana kwake kubaki katika taqliid ya yule mujtahid wa mwanzo katika mas'ala ambayo hakubadilisha taqliid yake, na atakuwa na hiyari katika yale mas'ala aliyobadilisha taqliid yake kwenda kwa mujtahid wa pili, ima kubakia katika taqliid yake au kubadili kwenda kwa mujtahid aliye hai.

4. Matendo ya ibada bila ya Taqliid

Matendo ya kiibada ya mtu wa kawaida yakifanywa bila ya taqliid au kwa taqliid ambayo ni batili, hukmu yake inakuwa ni batili, isipokuwa tu kama:

- a. Matendo hayo yataafikiana na ihtiyat.
- b. Matendo hayo yataafikiana na uhalisia wa hukmu.
- c. Matendo hayo yataafikiana na fat'wa za mujtahid ambaye ni wajibu juu yake kumfuata.

Maswali

1. Mtu anayeacha kujifunza hukmu za kidini ana hukmu gani?
2. Ni zipi alama za balegh?
3. Taja njia za kuzitambua hukmu?
4. Je, taklif kwa ihtiyat ni bora kuliko taqliid? Kwa nini?
5. Eleza aina za taqliid.
6. Ni ipi hukmu ya matendo ya ibada yatakayofanywa bila taqliid?

Changamoto

Ikiwa kazi ya mujtahid ni kutoa hukmu, lakini mara nyingi mujtahid huzungumzia mas'ala ya utumikaji wa hukmu hizo, Je, kuna haja ya kumfuata mujtahid katika uainishaji wake wa hukmu?

Taqliid

Somo la Pili

TAQLIID (2)

Masharti ya Marjaa Taqliid (mtu anayefuatwa).
Mgawanyiko katika Taqliid.

Masharti ya marjaa taqliid (*)

Mujtahid anatakiwa awe:


- a. Mwanamume.
- b. Balegh.
- c. Mwenye akili timamu.
- d. Shia Ithnaashariya.
- e. Aliyezaliwa kihalali.
- f. Hai.
- g. Mwadilifu.
- h. Awe na daraja ya Ijtihad.
- i. Mjuzi zaidi katika zama zake.

Kutokana na umuhimu wa cheo cha marjaa katika kutoa fat'wa, anatakiwa awe na uwezo wa kuidhibiti nafsi yake katika uovu, na wala asiwe ni mwenye kuipupia (kuipenda) dunia.

Uadilifu

Uadilifu maana yake ni hali ya kiroho inayomfanya mwanadamu kuwa na uchaji Mungu na kutekeleza misingi ya wajibu katika dini na hali hiyo imdhibiti kutokuacha mambo ya wajibu na imzuie kufanya mambo yaliyo haramishwa.

Mwadilifu ni mtu mwenye uadilifu au ni mtu ambaye amefikia daraja ya (*) Ni mwanazuoni aliyefikia ngazi ya Ijtihad (yaani mujtahid) anayefuatwa na waumini katika sheria za dini.



Mafunzo ya Hukmu za Ibada

ucha Mungu kiasi kwamba hawezi kwa makusudi kufanya haramu au kuacha wajibu. Hisia za dhahiri tu zinatoshwa kujua uadilifu wa mtu.

Ijtihad

Ijtihad inaweza kuwekwa katika makundi miwili:

1. Ijtihad Mutlaq

Ni ile Ijtihad ya kumfuata faqih ambaye ana uwezo wa kutoa hukmu na Fat'wa katika milango yote ya fiqhi. Huyu huitwa **al-mujtahidul-mutlaq**.

2. Ijtihad mutajazi

Ni ile ijihad ya kumfuata mujtahid ambaye anatoa fat'wa au hukmu katika baadhi ya milango ya fiqhi tu, kama vile swala, swaumu. Huyu huitwa **al-mujtahid al-mutajazi**.

Mjuzi zaidi (ihtiyat wajib)

A'alam, yaani mjuzi zaidi, ni yule mujtahid aliye na uwezo zaidi katika kutambua hukmu za Allah na kutoa fat'wa kuwazidi mujtahid wengine. Na suala hili la kumfuata mujtahid aliye mjuzi zaidi ni suala la kiakili, na hasa pale mujtahid aliye mjuzi zaidi anapotofautiana katika fat'wa na mujtahid wengine, kwa ihtiyat wajib ni vema kumfuata mujtahid huyo.

Nukta muhimu kuhusu masharti ya marjaa

Mujtahid ambaye ametimiza masharti ya kuwa marjaa, si lazima kwake kujitokeza kwa ajili ya u-marjaa, au kuwa na Risalatul-Amaliyyah. Hakuna tatizo kwa mukallaf endapo akitaka kumfuata marjaa ambaye yeye imemthibitikia kuwa ametimiza sharti za ijihad hata kama marjaa huyo hana Risalatul-Amaliyyah na wala hakujitokeza katika u-marjaa.

Hakuna sharti kwa marjaa ambaye ametimiza masharti ya ijihad kwamba ni lazima awe ni miongoni mwa watu wa mji wa mukallaf au mkazi wa nchi yake.

Taqliid

Wazazi pia wanawajibika kuwaongoza watoto wao waliofikia umri wa kutenzwa nguvu na sheria kuhusiana na mas'ala ya ijihad.

Mgawanyiko katika taqliid

Mgawanyiko katika taqliid maana yake ni taqliid kugawanyika katika aina mbali mbali kwa maana kwamba, kila hukmu kuhusiana na aina husika itaambatana na fat'wa za mujtahid anayehusiana na aina hiyo.

Muqalid anaweza kumfuata mujtahid mmoja katika kipengele fulani cha hukmu, mfano mas'ala ya ibada na kisha akamfuata mujtahid mwingine katika mas'ala ya muamala. Katika mgawanyiko huu pia suala la ujuzi zaidi linapewa umuhimu wake.

Maswali

1. Taja masharti ya marjaa taqliid
2. Ni nini maana ya uadilifu, na mwadilifu ni nani?
3. Je, fat'wa ya mujtahid mutajazi inakubalika kwake na kwa wengine?
4. Kwa nini ni lazima kumfuata mujtahid aliye mjuzi zaidi?
5. Je, inawezekana kufuata fat'wa za mujtahid bila kuwa na risala yake?
Toa maelezo.
6. Nini maana ya mgawanyiko katika taqliid, na kuna hukmu gani katika hilo?

Changamoto

Je, kuchunguza hali ya zama na mazingira yaweza kuwa ni moja kati ya masharti ya ijihadi?

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Somo la Tatu

TAQLIID (3)

- a. Njia za kumjua mujtahid.
- b. Njia za kupata fat'wa za mujtahid.
- c. Hukmu za kuhama taqliid.
- d. Mengineyo katika taqliid.

Njia za kumjua mujtahid aliyetimiza masharti

Inawezekana kumtambua mujtahid kwa njia mbili

i. Itmi'nan (kutosheka)

Ni sawa sawa ikiwa kutapatikana kutokana na umaarufu wake kwa watu au kwa uchunguzi binafsi au kwa njia nyinginezo.

ii. Ushahidi wa watu wawili waadilifu miongoni mwa watu wenye maarifa, japokuwa jambo hili haliwajibishi itmi'nan

Endapo ikisimama hoja ya kisheria inayothibitisha kuwa mujtahidi (fulani) anafaa na kwamba ametimiza masharti, basi ikiwa hapakufahamika mwenye kupinga hoja hiyo, hoja hiyo itaendelea kubakia kuwa ni dalili, na inafaa kuitegemea japokuwa haiwajibishi itmi'nani.

Kadhalika si lazima kufanya uchunguzi kuhusu (kuwepo kwa) mwenye kupinga au kuhakiki kutokuwepo kwake.

Njia za kupata fat'wa za mujtahid

Njia hizi zinatumiwa katika kupata fat'wa kutoka kwa mujtahid:

- a. Kusikia moja kwa moja kutoka kwa mujtahid mwenyewe.
- b. Kusikia kutoka kwa watu wawili waadilifu au mtu mmoja mwadilifu.
- c. Kusikia kutoka kwa mtu anayeaminika.
- d. Kuirejea risala ya mujtahid ikiwa risala hiyo imesalimika na makosa.

Taqlid

Hakuna haja ya kusubiri ijaza (ruhusa) ya mujtahid katika kunakili au kubainisha fat'wa ya mujtahid na kuzibainisha hukmu za sheria. (kazi hiyo) haifai kufanywa na mtu ambaye ataingia kwenye shubha na makosa. Endapo mtu atafanya shubha katika kunakili mas'ala fulani, kisha akatan-abahi, basi ni wajibu wake kuisahihisha fat'wa hiyo.

Haifai kwa namna yoyote ile kwa mwenye kusikiliza kilichonukuliwa ikiwa hana yakini juu ya usahihi wa kauli au nukuu ya fat'wa hiyo.

Hukmu ya kuhama taqlid

Inawezekana kumhama mujtahid a'alam ikiwa:

- a. Mujtahid a'alam (mjuzi zaidi) hakutoa fat'wa katika mas'ala husika na asiye a'alam hakufanya ihtiyat bali ametoa fat'wa moja kwa moja.
- b. Katika mas'ala ambayo fat'wa ya asiye a'alam haipingani na ile ya a'alam.
- c. Ikiwa fat'wa ya a'alam inapingana na ihtiyat hali ya kuwa fat'wa ya asiye a'alam inakubaliana na ihtiyat.

Haiwezekani kuhama taqlid ikiwa

- a. Mujtahid yuko hai na anahama kwenda kwa mujtahid mwingine aliye hai pia, hii ni kwa ihtiyat wajib, labda ikiwa Mujtahid amepoteza moja ya sharti za kuwa marjaa.
- b. Kurudi na kufuata mujtahid aliyekufa baada ya kwisha kuhama na kuja kwa Mujtahid aliye hai, mukallaf haruhusiwi kumhama mujtahid kwa kuwa anapata ugumu katika kutekeleza fat'wa za mujtahid huyo, au kwa kuwa na shaka kwamba fat'wa za mujtahid huyo haziendani na zama na mazingira aliyopo.

Mengineyo kuhusu taqlid

- a. Ikiwa mukallaf atapatwa na mas'ala akiwa katikati ya swala na hajui

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

hukmu ya mas'ala hayo, inajuzu kwake kutekeleza swala hiyo kulingana na upande wowote utakaomjia dhana kuwa ni sahihi kisha baada ya swala atawajibikiwa kuuliza. Ikiwa alichofanya kilikuwa ni sababu ya kubatilika kwa swala basi atairudia swala yake.

Kutokujua (al-jahlu) kuna aina mbili

i. Al-jaahil al-qasiir Huyu ni mtu asiyejua na hajitambui kuwa yeye hajui na wala hana njia ya kuondoa hali ya kutokujua kwake.

ii. Al-jahil al-muqassir Huyu ni mtu asiyejua, na anatambua kuwa hajui, na anazo njia za kuweza kuondokana na kutokujua kwake lakini ni mvivu wa kujifunza hukmu.

b. Ihtiyat wajib

Maana yake ni kuwajibikiwa kufanya au kuacha jambo kwa njia ya ihtiyat.

Mukallaf anaweza kumhama mujtahid wake ikiwa mujtahid mwingine alitoa fat'wa juu ya mas'ala ambayo kwa mujtahid wake hakukuwa na fat'wa bali ilitolewa kama ihtiyat wajib. Katika hali kama hii ni lazima kuzingatia mas'ala ya kuzidiana ujuzi.

c. Maneno kama: fihi ishkaal, laa yakhluu minal ishkaal mushkil, yapatikanayo katika vitabu vya kifiq'hi (sheria) yanatoa maana ya ihtiyat, ila ikiwa neno **laa ishkaala fihi** ambalo lina maana ya fat'wa.

d. Hakuna tofauti kati ya neno haijuzu na haramu kwani yanawakilisha maana moja tu ambayo ni ya kukataza.

Maswali

1. Taja njia za kupata fat'wa ya mujtahid.
2. Je, inawezekana kunakili na kubainisha fat'wa ya mujtahid bila idhini yake?
3. Vipi taqliid itahama kutoka kwa mujtahid mjuzi zaidi kwenda kwa asiyekuwa mjuzi zaidi?

Taqliid

4. Kuhama taqliid kunaruhusiwa ikiwa...?
5. Taja aina za kutokujua, yaani *Al-jahl*.
6. Nini tofauti baina ya kusema haijuzu na haram?

Changamoto

Je, inawezekana jukumu la kufanya uchunguzi ili kumpata mujtahid aliyekamilisha masharti ya kufuatwa liwe katika mikono ya wazazi, walimu, au walezi? na Je, maoni ya watu hawa yatakubalika kisheria?

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Somo la Nne

WILAYATUL FAQIIH NA UONGOZI

- a. Maana ya wilayatul-faqiih
- b. Haja ya kuwa na wilayatul-faqiih
- c. Mipaka ya wilayatul-faqiih
- d. Tofauti ya mtazamo wa waliyul faqiih na marjaa taqliid

A. Maana ya wilayatul-faqiih

Ni utawala unaoongozwa na mwanachuoni mwadilifu na anayefahamu dini. Mas'ala ya kuwa na wilayatul-faqiih katika kuongoza na kusimamia mas'ala ya kijamii katika kila zama, na ni miongoni mwa misingi ya kiimani ambayo mizizi yake inatoka katika asili ya Uimamu.

Kutokuwa na imani juu ya wilayatul-faqiih iwe ni kutokana na athari za ijthad au taqliid katika zama za ghaiba ya Imam wa Zama si jambo la kumtoa mtu katika Uislamu. Yeyote ambaye hoja na dalili zitamfanya asi-amini wilayatul-faqiih anasameheka, isipokuwa haifai kulifanya jambo hili kuwa ni lenye kusababisha kuzusha mfarakano baina ya Waislamu.

B. Haja ya kuwa na wilayatul-faqiih

Kwa kuwa Uislamu ndiyo dini ya kweli na ni yenye kubakia katika ulimwengu hadi siku ya Qiyama, ni lazima kuwepo na kiongozi atakaye kuwa na wajibu wa kusimamia na kuwaongoza Waislamu ili kutoingiliwa na shari ya maadui.

Kadhalika (kiongozi huyo atawajibika) kuulinda nidhamu ya jamii ya Kiislamu na kusimamia maswala yote ya kiutamaduni, kisiasa na hata kiuchumi. Pia atasimamia uadilifu na kuondoa dhulma, kuepusha matabaka baina ya wenye nguvu na wanyonge.

Wilayatul Faqiih na Uongozi

Wilayatul-faqiih ni suala la kisheria ambalo linathibitika kiakili, na katika kuliweka wazi jambo hilo kuna njia mbalimbali ambazo zinapatikana katika katiba ya Jamhuri ya Kiislamu ya Iran.

C. Mipaka ya wilayatul-faqiih

a. Kutiiwa

Waliyul faqihi anatakiwa kutiiwa pale anapoamrisha au kukataza jambo na twaa hii inawahusisha hata mafaqihi wengine hadi kufikia kwa wanaowafuata, haijuzu kwa yeyote kupinga maamrisha ya waliyul faqiih kwa sababu ya kuwa ana elimu zaidi hasa ikiwa waliyul faqihi anatambuliwa kisheria.

b. Kutoa hukmu

Waliyul faqiih atoapo hukmu huwa ni ya kuendelea na wala si ya muda mfupi, labda waliyul faqihi mpya atakapoona kuna maslahi katika kuifuta hukmu hiyo.

c. Kusimamia au kutekeleza hukmu

Waliyul faqiih ana wajibu wa kutekeleza na kusimamia hukmu za kisheria (kama kutekeleza hukmu ya mwizi, mzinifu n.k)

d. Ikhtiyari juu ya umma

Waliyul faqihi ana haki ya kutoa maamuzi yanayohusiana na maslahi ya umma wa Kiislamu, na kwa hiyo maamuzi ya waliyul faqiih yanatangulia kabla ya maamuzi ya umma.

e. Usimamizi wa njia za habari

Waliyul-faqiih ana wajibu wa kusimamia njia zote pamoja na vyombo vinavyohusika na usambazaji na uenezi wa habari na maelezo, na katika kueneza maarifa ya dini ya Kiislamu ikiwa ni katika kuleta umoja wa Kiislamu na kusaidia kuondoa matatizo ya Waislamu.

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Nukta muhimu

- a. Uwakilishi wa waliyul faqiihi unapaswa kutiwa ikiwa amri anayotoa inatoka kwa waliyul faqiih.
- b. Katika sheria ya Kiislamu haijuzu kufuata amri kutoka kwa kiongozi bila ya kuwa na mahojiano na mjadala, lakini ikiwa amri hiyo imepitishwa kisheria na kuthibitika utumikaji wake haijuzu kwa mukallaf kuipinga amri hiyo.
- c. Waliyul faqiih hawezi kuwa na utawala wa takwiini, utawala huu unawahusu Maasumina (a.s) pekee.

i. Wilayatul tashri'i

Ni utawala wa kuchunga hukmu za Allah kama ambavyo mzazi au mlezi anavyokuwa walii wa mtoto.

ii. Wilayatul takwiini

Mara nyingi inakwenda sambamba na miujiza kwa idhini ya Allah kama kuwaombea walio na maradhi sugu wapakata nafuu.

D. Kutofautiana rai baina ya waliyul faqiih na marjaa taqliid

Ikiwa baadhi ya amri zinatofautiana kati ya marjaa taqliid na waliyul faqiih, endapo amri hiyo inahusiana na utawala wa nchi na mambo yanayohusu jamii ya Kiislamu, kama kuulinda Uislamu na Waislamu dhidi ya makafiri na wavamizi, lazima amri ya walii ifuatwe. Na ikiwa inahusiana na mambo ya kibinafsi, kila mukallaf ana wajibu wa kufuata amri na fat'wa za marjaa taqliid anayemfuata.

Maswali

1. Nini maana ya wilayatul faqiih na kuna dharura gani ya kuwepo kwa waliyul faqiih.
2. Bainisha wajibu wa Waislamu juu ya mipaka ya waliyul faqiih.
3. Je, amri zilizotolewa na kiongozi aliyekufa zinaweza kuendelea kutumika bila idhini ya kiongozi aliye hai?

Wilayatul Faqiih na Uongozi

4. Muftahid aliyekamilisha masharti ya kufuatwa, Je, ana uwezo wa kutoa na kutekeleza hukmu au adhabu katika zama za ghaiba?

5. Je, inajuzu kumtii muwakilishi wa waliyul faqiih katika mambo ambayo yanasimama katika mipaka ya muwakilishi huyo?

6. Nini wajibu wa mukallaf ikiwa amri ya waliyul faqiih imetofautiana na mambo ya marjaa taqliid?

Changamoto



Je, waliyul faqiih anaweza kufuta au kuondoa hukmu ya dini? kwa nini?

Mafunzo ya Hukmu za Ibada



Sehemu ya Pili

TWAHARA



Twahara

UTANGULIZI WA TWAHARA

Uislamu umetilia umuhimu sana suala la twahara na usafi, ikawajibisha kutekeleza baadhi ya amaali na majukumu ya kisheria kwa sharti la mtu husika awe katika hali ya twahara kama vile ambavyo imemtaka mtu kujitenga na najisi ya aina yoyote au katika baadhi ya maeneo maalum.

Katika fiqhi ya Kislamu - inayomtaka mtu kudumisha tahara na usafi - pia kuna aina maalum ya kuosha ambako ni kutawadha au kuoga (udhu au ghusl) na ambako pia hujulikana kama twahaarah; ambapo wakati mwingine huwa wajibu na wakati mwingine kuwa sunnah (mustahab).

Katika kipengele hiki zimebainishwa hukmu za twahara, vitu vinavyotwaharisha na jinsi ya kutwaharisha mavazi, mwili na vitu vingine, na kadhalika vitu vya najisi na uchafu na mas'ala mbalimbali yanayohusiana nayo

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Somo la Tano

MAJI

- a. Aina za maji
- b. Maji mutlaq
- c. Maji mudhaf
- d. Hukmu ya maji mudhaf
- e. Aina za maji mutlaq
- f. Hukmu za maji mutlaq
- g. Hukmu za shaka katika maji

a. Aina za maji

Maji yako ya aina mbili:

- i. Mudhaf
- ii. Mutlaq

b. Maji mutlaq

- i. Maji ya mvua.
- ii. Maji yanayotiririka.
- iii. Maji yaliyotulia yanagawanyika katika maji ya Kurr (Kullaten) na maji machache.

c. Maji mudhaf

Maji Mudhaf ni maji ambayo yenyewe hayana uhalisia wa kuitwa maji, bila nyongeza ya neno jingine kwa kuwa mara nyingi maji hayo yanatokana na kitu au kuchanganywa na kitu, kiasi kwamba yamekosa ile sifa halisi ya kuitwa (kuwa ni) maji; mfano wake ni kama vile juisi na maji ya chumvi.

d. Hukmu ya maji mudhaf ni:

- i. Hayatwahirishi kitu miongoni mwa najisi.
- ii. Yakiguswa na najisi yananjisika (hata kama hayatabadilika rangi,

Maji

ladha, harufu, na hata maji ya mudhaf yawe yamefikia wingi wa kurr).
iii. Wudhu na joshu kwa maji haya ni batili.

Mara nyingine kuna madawa ambayo huongezwa katika maji na kuyabadili kuwa na kiasi fulani kama ya maziwa, maji hayo hayapati hukmu ya mudhaf, hivyo huweza kutumika kwa ajili ya kutwahaisha, wudhu na joshu.

e. Aina ya Maji mutlaq

Ni maji halisi yaliyo na uhalisia wa maji, kama maji ya mvua, n.k.
Aina za maji mutlaq

- i. Yatokayo mbinguni (mvua)
- ii. Yatokayo ardhini (kisima, chemchem)
- iii. Yaliyotulia ambayo ni mengi (kiasi cha kurr) na yawe na ujazo wa lita 384 na kuzidi, au machache yaliyopungufu ya hayo kwa kiasi chochote.

f. Hukmu za maji mutlaq

- i. Yanatwahaisha najisi
- ii. Yakiguswa na najisi hayanajisiki ila yakibadilika rangi, ladha, harufu. (maji machache yanajisika yakiguswa na najisi).
- iii. Yanatumika kwa wudhu, joshu na twahara nyinginezo.

Uchafu au uzito wa maji haufanyi maji mutlaq kuwa najisi, hasa uzito huo ukiwa unatokana na kuwapo kwa chumvi nyingi katika maji hasa maji ya bahari (kama ilivyo katika bahari ya Aruumiyyah), na maji hayo yanaweza kutumika kwa kufanyia twahara, suala hili linaendana na urfu yaani rai za watu wa eneo hilo.

Hukmu za aina za maji mutlaq

i. Maji ya mvua

Mvua ikinyeshea kitu kilicho najisi hutwahaisha,



Mafunzo ya Hukmu za Ibada

ii. Maji ya kurr na yanayotembea

Kitu chenye najisi kikiingizwa ndani ya maji ya kurr au yanayotembea, hutwahaarika na maji yanabaki kuwa twahara ila kama yatabadilika rangi, ladha na harufu.

Hakuna tofauti katika kutwahaarisha najisi kwa kutumia maji ya kurr au yanayotembea.

iii. Maji machache

1. Ikiwa kitu chenye najisi kitaingizwa ndani ya maji machache, maji hayo yatanajisika na kitu hicho chenye najisi hakitatwahaarika.

2. Yakimiminwa juu ya kitu kilicho na najisi, kitu hicho kinatwahaarika lakini yale yaliyogusa kitu kile yatanajisika.

3. Yakimiminika na kugusa najisi iliyo chini, basi yale tu yatakayogusa najisi ndiyo yatakayonajisika na yatakayobaki juu yatakuwa twahara.

Ikiwa yameunganishwa na kurr au maji yanayotembea yanapata hukmu ya maji yaliyounganishwa nayo.

g. Hukmu za shaka katika maji

i. Maji ambayo yanatiliwa shaka kuwa ni twahara au najisi yana hukmu ya twahara, ikiwa maji yalikuwa ni najisi baada ya muda yakatiliwa shaka kuwa ama yametwahaarika au hapana, yatabaki kuwa ni najisi.

ii. Maji yaliyotimia ujazo wa kurr ikiwa yatatiliwa shaka kwamba yamepungua au la, yatabaki na hukmu ya kurr.

iii. Si lazima kuwa na elimu juu ya maji ya kurr, ila ikiwa itazingatiwa hali ya mwanzo ya ujazo wa kurr inatosheleza.

Maji

iv. Maji yasiyotimia ujazo wa kurr hayawezi kupata hukmu ya kurr ikiwa hakuna yakini juu ya kuwa kwake kurr.

Maswali

1. Taja aina za maji.
2. Elezea maana ya maji mudhafu na mutlaq.
3. Elezea hukmu za maji mutlaq.
4. Nini hukmu ya wudhu na joshu kwa maji ya bahari yaliyokuwa na chumvi?
5. Kuna tofauti gani katika kutwaharisha kwa kutumia maji ya kurr na yanayotembea?
6. Nini hukmu ya maji ambayo hayajulikani kuwa ni twahara au yamena-jisika?

Changamoto

Maji ya chumvi yakichemshwa, mvuke utakaopatikana utaweza kutumika kwa ajili ya wudhu, joshu na kutwaharisha najisi.

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Somo la Sita

HUKMU ZA KWENDA HAJA

- a. Hukmu za haja
- b. Istibraa
- c. Istinjaa

a. Hukmu za haja (kubwa na ndogo)

i. Kuchunga kibla: Hairuhusiwi wakati wa kwenda haja iwe kubwa au ndogo kugeukia upande wa kibla au kukipa mgongo.

ii. Mavazi: Ni wajibu kwa mtu wakati akiwa katika haja (au wakati mwingine wowote) kuhakikisha kwamba anafunika sehemu zake za siri, na asiweze kuonwa na yeyote hata kwa mtoto mdogo ambaye hana uwezo wa kufahamu. Kwa mke na mume si lazima kufunika sehemu za siri.

Zifuatazo ni hukmu ambazo ni makruhu wakati wa kwenda haja

- kufanya haja ndogo wima,
- kufanya haja ndogo kwenye ardhi ngumu na ndani ya mashimo ya wadudu,
- ni makruhu kuzuia haja iwe kubwa au ndogo,
- ni makruhu pia kwenda haja kubwa barabarani, njiani au chini ya miti yenye matunda.

b. Istibraa

i. Baada ya haja ndogo, ikiwa mtu alifanya istibraa, na baada ya hapo yaka-toka majimaji ambayo hayajulikani kuwa ni mkojo au kitu kingine, maji-maji hayo yatakuwa na hukmu ya twahara na si lazima kufanya uchunguzi.

Hukmu za kwenda Haja

- ii. Si wajibu kufanya istibraa hasa ikiwa kuna kidonda katika sehemu husika na kuiminya sehemu hiyo kutasababisha umwagikaji wa damu na kuchelewa kupona kwa kidonda. Ikiwa istibraa haikufanyika majimaji yatakayotoka baada ya mkojo yatakuwa na hukmu ya mkojo.
- iii. Njia bora ya kufanya istibraa ni kuwa baada ya kumaliza haja, kwanza itatwahirishwa njia ya haja kubwa ikiwa ilinajisika, kisha kwa kutumia kidole cha kati kusukuma kwa kuminya kuanzia sehemu ya haja kubwa hadi inapoanzia sehemu ya haja ndogo, kisha kidole gumba kitawekwa juu ya uume na cha kati kitawekwa chini yake, halafu kuminya kwa kuelekea mbele kwenye kichwa cha uume mara tatu, na baada ya hapo atakikamua kichwa cha uume mara tatu na kisha kutwahirisha mahala panapotokea mkojo.
- iv. Hakuna tofauti baina ya kutwahirisha njia ya haja kubwa kabla ya istibraa au baada yake.
- v. Ikiwa baada ya haja ndogo istibraa ilifanyika na wudhu, kisha yakatoka majimaji yanayotiliwa shaka kuwa huenda yakawa ni mkojo au manii, ili kupata hakika au yakini ni wajibu kwa atakayetokewa na hali hiyo kufanya joshu na wudhu ili kujitwahirisha.

Aina za majimaji yatokayo kwa mwanadamu

- i. Maji yanayotoka baada ya manii huitwa **wadhii**.
- ii. Maji yanayotoka baada ya haja ndogo huitwa **wadii**.
- iii. Maji yanayotoka baada ya kugusana kihisia baina ya mke na mume huitwa **madhii**. Majimaji yote hayo ni twahara na hayabatilishi twahara.

c. Istinja (kutwahirisha njia za haja)

Njia ya haja ndogo haitwahiriki ila kwa maji tu ambayo kwa ihtiyat wajib huoshwa mara mbili.

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Njia ya haja kubwa huoshwa kwa maji hadi kuisha kwa najisi, pia huweza kutwahirishwa kwa kutumia mawe matatu, kitambaa na mfano wa hivyo.

Njia ya haja kubwa hutwahirishwa kwa maji tu ikiwa:

- a. Haja iliambatana na najisi nyingine kama vile damu.
- b. Najisi nyingine kutoka nje iligusa sehemu hiyo.
- c. Haja ilienea katika sehemu nyingine.

Maswali

1. Je, ni wajibu kufunika sehemu za siri mbele ya mtoto mdogo?
2. Taja baadhi ya makruhu katika kufanya haja.
3. Hukmu ya istibraa ni ipi?
4. Istibraa ina faida gani?
5. Elezea aina za chembechembe zitokazo kwa mwanadamu.
6. Elezea jinsi ya kutwahirisha njia za haja ndogo na kubwa.

Changamoto

Ikiwa choo kimejengwa kuelekea kibla kwa tofauti ya nyuzi ishirini hadi ishirini na mbili. Je, ni lazima kubadili uelekeo wa choo hicho au sio lazima?

Najisi

Somo la Saba

NAJISI (1)

Najisi ni:

1. Haja kubwa.
2. Haja ndogo.
3. Manii ya mwanadamu.
4. Mzoga au maiti.
5. Damu.
6. Mbwa.
7. Nguruwe.
8. Vileo (Ihtiyat Wajib).
9. Kafiri asiyeamini dini zilizoteremshwa.

Kila kitu kina hukmu ya twahara isipokuwa vilivyotajwa hapo juu ambavyo sheria imebainisha unajisi wake.

1 - 2. Haja kubwa na ndogo

i. Wanadamu na kila mnyama aliye haramu kuliwa mwenye damu inayochupa (inayotoka kwa nguvu wakati wa kuchinjwa), kama panya, haja zao kubwa na ndogo ni najisi.

ii. Wanyama walio halali kuliwa pamoja na ndege walio haramu kuliwa, na wanyama walio haramu kuliwa wasio na damu ya kuchupa kama nyoka na samaki asiye na magamba haja zao ni twahara.

3. Manii

Manii ya mwanadamu ni najisi.

Ikiwa baada ya haja ndogo istibraa itafanyika, kisha yakatoka majimaji ambayo hayana uhakika kama ni manii au siyo, na ikiwa haikupatikana yakini juu ya kuwa kwake manii na hayakuambatana na alama za kisheria juu ya utokaji wake, hayatakuwa na hukmu ya manii na yatakuwa twahara.

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Alama za manii ni

- i. Kwa wanaume kuambatana na shahawa (matamano).
- ii. Kutoka kwa nguvu.
- iii. Kuchoka mwili
- iv. Na kwa wanawake huambatana na shahawa. (ijulikane kuwa kurejea katika alama hizi ni pale ikiwa kuna shaka kuwa kilichotoka ni manii au siyo).

4. Mzoga Maiti

Maiti ya Mwiislamu ni najisi isipokuwa

1. Viungo vyake visivyo na uhai kama kucha, nywele na meno.
2. Shahidi katika uwanja wa vita.
3. Kama ameshaoshwa kwa ukamilifu.

Maiti inatakiwa kuoshwa majosho matatu ndipo itwaharike.

- i. Maiti ya Kafiri (Ahlul Kitab) ni najisi ila viungo vyake visivyo na uhai.
- ii. Maiti ya Kafiri (asiye Ahlul Kitab) ni najisi kila kiungo chake. Mzoga wa mbwa na nguruwe ni najisi kila kitu chake.
- iii. Mizoga ya wanyama wengine (wasiokuwa mbwa na nguruwe) ikiwa wana damu inayochupa, ni najisi ila kama walichinjwa kwa kufuata sheria. Viungo vyao visivyo na uhai kama pembe n.k ni twahara.
- iv. Mizoga ya wanyama wengine (wasiokuwa mbwa na nguruwe) ikiwa hawana damu inayochupa, viungo vyao vyote ni twahara.
- v. Ngozi nyepesi katika nyayo, viganja, midomo inayotoka yenyewe si najisi.
- vi. Nyama, utumbo na vitu vinayopatikana kutoka kwa wanyama ni twahara ikiwa vinauzwa katika nchi ya Kiislamu, na ikiwa vipo katika mikono ya Waislamu. Ikiwa vitu hivyo vimetoka katika nchi za

Najisi

Makafiri vitakuwa ni najisi, ikiwa kutakuwa na yakini katika uchinjaji wake kuwa haukuwa wa kufuata sheria.

5. Damu

- i. Damu ya mwanadamu na kila mnyama mwenye damu inayochupa ni najisi, awe ni mnyama halali au haramu kuliwa.
- ii. Damu inayobaki katika mwili wa mnyama baada ya kuchinjwa ina hukmu ya twahara.
- iii. Damu ipatikanayo ndani ya yai ina hukmu ya twahara lakini ni haramu kuila damu hiyo.

6 -7. Mbwa na nguruwe

- a. Mbwa na nguruwe ni najisi na hakuna tofauti katika hukmu hii kati ya viungo vilivyo na uhai au visivyo na uhai.
- b. Haijuzu kutumia manyoya ya mbwa wala nguruwe kutengenezea kitu ambacho kitatumika katika twahara. Mfano chombo cha kutawadhia au kufanyia joshu, lakini inajuzu kutumia katika mambo ambayo hayahitaji twahara mfano, kutengenezea kalamu kwa ajili ya kuchorea.

Maswali

1. Taja vitu vilivyo najisi.
2. Je, kinyesi cha ndege walio haramu kuliwa kina hukmu ya najisi?
3. Taja alama za manii kisheria.
4. Maiti inakuwa twahara wakati gani?
5. Ni vipi nyama na ngozi ya wanyama itokayo katika miji isiyo ya Kiislamu inakuwa twahara?
6. Tone la damu lipatikanalo ndani ya yai lina hukmu gani?

Changamoto

Ikiwa mtu atajipigiza ukutani na damu ikatoka na kuwarukia wengine itakuwa na hukmu gani?

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Somo la Nane

NAJISI (2)

8. Vileo

- a. Kila aina ya kileo chenye asili ya kimiminika ni najisi kwa mujibu wa ihtiyat wajib.
- b. Bangi na dawa za kulevya kwa asili si najisi hata ikichanganywa na maji.
- c. Maji ya zabibu yaliyochemshwa na hayakupungua theluthi mbili baada ya kuchemshwa kwake, ikiwa si kileo si najisi lakini ni haramu kula.
- d. Endapo kiasi fulani cha zabibu mbichi kitawekwa ndani ya maji yanayo chemka na kuwekwa humo kiasi kidogo sana cha zabibu, kisha maji yake yakachanganyika na maji ya zabibu mbichi kwa namna ambayo maji hayo hayawezi kuitwa kuwa ni maji ya zabibu, basi ni halali kuliwa. Lakini zabibu peke yake ikichemshwa ni haramu kuliwa.

9. Kafiri

- a. Mtu anayepinga tawhiid, au moja kati ya mambo ambayo ni dharura katika Uislamu, mfano swala na swaumu, au akawa na itikadi ya kuwa na mapungufu kwa Utume wa Mtume (s.a.w), mtu huyo ni kafiri na najisi isipokuwa Ahlul Kitabu.
- b. Kupinga moja kati ya dharura za dini kutaleta ukafiri pale tu ikiwa kupinga huko kutapelekea kupinga Utume, au kumpinga Mtume, au kuingiza mapungufu katika sheria.
- c. Kafiri ambaye ni Ahlul Kitab ana hukmu ya twahara.

Najisi

- d. Ahlul Kitabu ni wale wanaoamini moja kati ya dini ambazo zime-teremshwa na Allah (s.w.t), kama Mayahudi, Manaswara na Majusi (wanaoabudu moto) pamoja na Wasabai ambao wanadai kumfuata Mtume Yahya (a.s) na wanasema kwamba wanacho kitabu chake kama mwongozo wao.
- e. Kuamini Utume wa Mtume Muhammad (s.a.w.w) si kigezo pekee cha kuwa ni Mwislamu, hasa ikiwa matendo yao wanayatenda kwa kuwafuata wazee wao. Hawa hawazingatiwi kuwa ni Waislamu, lakini wakiwa ni Ahlul Kitab wana hukmu ya twahara.
- f. Mwislamu aliyeritadi ni Kafiri na ikiwa kuritadi kwake hakuungii katika Ahlul Kitab basi atakuwa najisi .

Kuacha kufanya maamrisha ya dini kama swala na swaumu hakumfanyi Mwislamu kuwa Kafiri wala kuwa najisi. Na bado Mwislamu huyu mwenye kuasi atakuwa na haki zote kama Mwislamu mwingine ikiwa hajadhihirisha kuritadi kwake.

- g. Watu wanaoitakidi uungu wa Sayyidna Ali ni makafiri na ni najisi.
h. Mtu anayewafanyia uadui Maimamu Maasum ni Kafiri na ni najisi.
h. Wafuasi wa Madhehebu ya Bahai ni najisi.

MAS'ALA YANAYOFUNGAMANA NA NAJISI

Jasho la mwenye janaba la haramu ni twahiri lakini kwa ihtiyat asiswali nalo.

Jasho na mate ya aliyekula nyama ya haramu au najisi (kama nyama ya nguruwe) ni twahira.

Athari hafifu ya rangi ya damu iliyobaki kwenye nguo iliyotwaharishwa na haiondoki kwa kuoshwa ni twahara ikiwa hakuna dhati ya damu iliyobakia Matapishi ni twahara yawe ya mtoto mchanga au mtu mzima.

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Maswali

1. Kwani alkoholi ni najisi?
2. Ni kwa mtazamo gani kupinga dharura za dini kunapelekea ukafiri?
3. Maana ya Ahlul Kitabu ni nini? Na Ahlul Kitab wana hukmu gani juu ya unajisi na utwahara wao?
4. Bainisha hukmu juu ya madhehebu ya Bahai
5. Jasho lipatikanalo kutokana na janaba ya haramu lina hukmu gani?
6. Je, athari ya damu ibakiayo juu ya nguo baada ya kufuliwa ina hukmu ya najisi?

Changamoto

Wafuasi wa madhehebu ya Ismailiya wana hukmu gani katika unajisi na utwahara?

Najisi

Somo la Tisa

NAJISI (3)

Najisi

1. Njia za kuthibitisha najisi.
2. Jinsi vitu twahara vinavyonajisika.
3. Hukmu za najisi.
4. Wasiwasi na jinsi ya kuuondoa.

1. Njia za kuthibitisha najisi

Kitu najisi kinaweza kuthibitika kwa njia tatu:

- a. Mtu kuwa na yakini juu ya unajisi wa kitu.
- b. Mmiliki wa kitu aeleze juu ya unajisi wa anachokimiliki.
- c. Watu wawili waadilifu washuhudie juu ya unajisi wa kitu.
- d. Mtoto anayekaribia balegh atakubaliwa maneno yake juu ya unajisi wa kitu ikiwa anakimiliki.

2. Jinsi vitu twahara vinavyonajisika

Kitu twahara kitanajisika ikiwa:

- a. Kitagusana na kitu najisi.
- b. Kimojawapo au vyote viwili kiwe na unyevunyevu ili kuweza kulowesha kingine.
- c. Unyevunyevu huo unaweza kuhama (kwa kukilowesha kingine)
- d. Kugusana huko kusiwe kwa ndani.

Unyevunyevu (wa kitu chenye najisi na kitu chenye twahara) ni ule ambao kiasi chake kinaweza kuhama kutoka kwenye kitu chenye najisi na kwenda kwenye kitu kingine (kilicho twahara) pindi kimojawapo kitakapogusa kingine Ikiwa sehemu moja ya kitambaa au kitu mfano wa hicho kimegusa

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

najisi, ni sehemu hiyo tu ndiyo itakayonajisika na sehemu zilizobaki zitakuwa twahara.

Maji yanayoingia kwenye mdomo ulio na damu iliyoganda kwenye ufizi kisha yakatoka yana hukmu ya twahara ingawaje vizuri ni kujiepusha nayo, vilevile chakula pia hakuna mushkeli hata kukimeza.

Mutanajisi maana yake ni kitu kilichonajisika kwa kugusana na dhati ya najisi (najisi yenyewe), kitu hiki kinaweza kunajisi kingine, na kingine kunajisi kitu kingine kwa mujibu wa ihtiyat wajib. Kinachonajisika kwa mara ya tatu hakitanajisi kingine.

3. Hukmu za najisi ni

- a. Ni haramu kula na kunywa kitu najisi. Pia ni haramu kumlisha mtu ambaye hana habari juu ya najisi hiyo. Lakini ikiwa ataonekana mtu akiswali na nguo iliyonajisika au kula chakula cha najisi haina lazima kumueleza juu ya unajisi wa kitu hicho.
- b. Si lazima kumweleza mfuaji wa nguo juu ya kuwa (nguo hizo) zina najisi, lakini mwenye nguo lazima apate yakini juu ya utwahara wake kabla ya kuitumia.
- c. Kama mgeni amekitia najisi kitu cha mwenyeji wake ambacho si chakula wala kinywaji, si lazima kumpa habari mwenyeji wake.

4. Wasiwasi na jinsi ya kuuondoa

Watu wenye wasiwasi ambao mara zote wanahisi kuwapo kwa najisi wanaweza kufuata njia zifuatazo katika kuondoa wasi wasi huo:

- a. Katika jambo lolote wakitia shaka juu ya utwahara au unajisi wake kwa mujibu wa sheria ya dini watahukumu kuwa kitu hicho ni twahara.
- b. Hata katika baadhi ya nyakati wakiwa na yakini juu ya najisi, watahukumu kuwa ni twahara isipokuwa watakapoona najisi kwa macho yao ndio watahukumu kuwa kitu hicho ni najisi.

Najisi

- c. Kitu chochote kilichonajisika, baada ya kuondolewa najisi kikioshwa mara moja chini ya maji ya bomba kinatwaha. Si lazima kuendelea kukiosha, ikiwa kitu hicho kina asili ya kitambaa au mfano wa hivyo. Kwa ihtiyat wajib kukamuliwa pia kunahitajika ili kuondoa maji yaliyomo ndani yake.
- d. Hukmu za Uislamu ni nyepesi sana na zinaendana na maumbile ya wanadamu, basi msiifanye kuwa ngumu kiasi cha kuleta shida katika maisha, na Allah haridhii mtu kujitaabisha au kuwataabisha walio nyuma yake.
- e. Hali hii ya wasiwasi ni ya kupita tu na inaweza kutibika, kwa kuweka imani na kumtegemea Allah (s.w.t)

Maswali

1. Je, kauli ya mtoto anayekaribia kuwa balegh kuhusu unajisi wa kitu anachokimiliki inaweza kukubaliwa?
2. Taja na eleza jinsi kitu twahara kinavyoweza kunajisika.
3. Nini maana ya unyevunyevu unaoenea?
4. Kitu kilichonajisika kinaweza kunajisi kitu kingine mara ngapi?
5. Ikiwa mgeni amenajisi moja ya kitu cha mwenyeji wake Je, anao wajibu wa kumueleza mwenyeji wake?
6. Mtu mwenye wasiwasi akiwa hana yakini juu ya unajisi wa kitu atatumia hukmu gani?

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Somo la Kumi

VINAVYOTWAHARISHA (1)

1. Mutwahirat (vinavyotwahirisha)

Ni vitu vinavyotumika kutwahirishia vitu vilivyonajisika, vitu hivyo ni:

1. Maji
2. Ardhi
3. Jua
4. Istihala
5. Intiqal
6. Islamu
7. Kufuata
8. Kuondoka kwa najisi
9. Istibraa
10. Kughibu Mwislamu.

1. Maji

a. Jinsi ya kutwahirisha vyombo vilivyonajisika

- i. Kwa maji machache kitaoshwa mara tatu, isipokuwa kwa maji mengi (Kurr) au yatembeayo kitaoshwa mara moja.
- ii. Kama kimetumiwa na mbwa kwa kula kitu chenye majimaji au amekil-amba, lazima kwanza kiohwe kwa mchanga kisha maji. Na kwa maji machache kitaoshwa mara mbili baada ya kusuguliwa kwa mchanga.
- iii. Chombo kilichotumiwa na nguruwe kula chakula cha majimaji ndani yake, kinatakiwa kuoshwa mara saba kwa maji lakini si lazima kuosha na mchanga.

b. Jinsi ya kutwahirisha vitu vingine vilivyonajisika

- i. Ikiwa najisi imeondolewa kinaweza kuoshwa mara moja tu kwa maji ya

Vinavyotwahaisha

kurr na yanayotiririka au kuoshwa kwa maji ya bomba. Ni lazima ihakikishwe kuwa maji yameenea sehemu zote, nguo na mfano wake ni lazima kwa ihtiyat wajib kukamuliwa.

ii. Kitu kilichonajisika kwa mkojo, kitatwahaisha kwa kuoshwa mara mbili kwa maji machache baada ya kuondoka kwa najisi hiyo. Kama kitu kimenajisiwa kwa kitu kisichokuwa mkojo, baada ya kuondoa dhati ya najisi (najisi halisi) kitatwahaisha kwa kuoshwa mara moja.

iii. Kitu kinachotwahaishwa kwa maji machache, ni lazima maji yale yaondolewe ikiwa kitawezekana kukamulika.

iv. Katika kutwahaisha kitu kama zulia si lazima kukamua ikiwa yalitumika maji ya bomba, ila kama maji yamegusa sehemu iliyo najisi baada ya kuondoka kwa najisi yenye kuonekana, na maji hayo yalitolewa katika nguo au zulia kwa njia ya mkono wakati bado maji yanaendelea kutoka sehemu hiyo inatwahaisha.

v. Nguo zenye najisi zikiwekwa katika chombo na kufunguliwa maji ya bomba na kuenea sehemu zote, maji yatokayo katika nguo hizo na vyombo vyote vitatwahaisha, lakini kwa ihtiyat wajib lazima nguo zikamuliwe.

vi. Nguo zenye najisi na ambazo zikitiwa maji zinatoa rangi, ikiwa rangi hiyo haitasababisha maji kuwa mudhaf, nguo hizo zitatwahaisha.

vii. Tanuri lililotengenezwa kwa udongo uliochanganywa na maji yaliyo najisika linatwahaisha kwa kuosha sehemu zenye kuonekana za tanuri hilo.

Maswali

1. Taja vitu vinavyotwahaisha.
2. Eleza jinsi ya kutwahaisha vyombo.
3. Je, katika kuosha nguo zilizonajisika kwa maji ya kurr na yanayotembea

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

kuna ulazima wa kukamua? Au inatosha tu baada ya kuondoa najisi?

4. Katika kutwaharisha nguo (zilizonajisika) kwa maji ya kurr na yanayotembea, je, inatosha tu kwa kukamua ndani ya maji au lazima ikamuliwe nje ya maji?

5. Je, kuna uwezekano wa kutwaharisha tanuri lililotengenezwa kwa udongo uliochanganywa na maji yaliyo najisika?

6. Nguo zilizonajisika ikiwa wakati wa kutwaharishwa zitatoa rangi, zitatwaharishwa kwa njia gani?

Changamoto

Nguo zinazooshwa kwa mashine hutwaharika?

Vinavyotwaharisha

Somo la Kumi na Moja

VINAVYOTWAHARISHA (2)

Vitu vinavyotwaharisha

2. Ardhi

Kutokana na athari ya kutembea katika ardhi soli ya kiatu au nyayo ikinajisika, vitu hivyo hutwaharika kwa kutembea mwendo wa karibu hatua kumi katika ardhi kavu na twahara, kwa sharti kwamba kusiwe na najisi yenye kuonekana. Sakafu ya simenti au vigae haitwaharishi soli ya kiatu wala nyayo.

3. Jua

Jua hutwaharisha ardhi, miti, majani, majengo na kila kitu kisichohamishika kama majumba na kila kilichotumika kama madirisha, milango nk.

Ili Jua litwaharisha ni Lazima:

- i. Kitu chenye najisi kiwe kimelewa.
- ii. Kusiwepo na najisi yenye kuonekana (najisi hiyo iondolewe).
- iii. Kusiwe na kizuizi cha jua kufika sehemu hiyo (kama vile wingu au pazia).
- iv. Kitu hicho kikauke kwa jua.

4. Istihala (kubadilika)

Kitu najisi ikiwa kitabadilika na kuwa kitu kingine ambacho ni twahara. Mfano pombe itakapobadilika na kuwa siki, kitu hicho kitakuwa twahara, lakini ngano iliyonajisika ikiwa unga haitakuwa twahara.

5. Intiqal (kuhama)

Damu ya mwanadamu inayonyonywa na mbu au mdudu mfano wa huyo, kwa muda wote ambao damu hiyo itahesabika ni ya mwanadamu, itakuwa

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

na hukmu ya najisi. (Mfano damu inayonyonywa na luba) lakini ikipita muda na damu hiyo kuhesabika kuwa ni ya mdudu huyo inakuwa twahara

6. Uislamu

Kafiri ni najisi, lakini akipiga shahada mbili basi anakuwa amekwishatwaharika mwili wake wote. Ahlulkitab ni twahara

7. Kufuata.

Kafiri akisilimu watoto wake watamfuatia katika utwahara, vile vile vitu anavyooshewa navyo maiti vinatwaharika baada ya kukamilka majoshao matatu

8. Kuondoka dhati ya najisi

Ikiwa mwili wa mnyama umenajisika na ikiwa najisi hiyo imeshaondoka, mnyama huyo atatwaharika, na haina lazima ya kuosha. Hukmu hii pia inatumika kwa sehemu za ndani za mwanadamu kama mdomo, pua, kwa sharti kwamba najisi hiyo isiwe ya kutoka nje, basi damu itokayo katika meno ikipotelea katika mate mdomo utakuwa twahara.

9. Istbraa

Mnyama aliyekula kinyesi cha binadamu kiasi cha kuimarika nyama yake na mifupa yake, atakuwa najisi pamoja na mkojo wake na kinyesi, lakini atatwaharika kwa kutengwa asile tena kinyesi kwa muda wa siku 40 kwa ngamia, 20 ng'ombe, 10 mbuzi na kondoo, 5 bata na 3 kuku.*

10. Kughibu kwa Mwislamu

Kama kuna yakini kwamba mwili wa mwanadamu au moja ya vitu anavyomiliki kimenajisika, na Mwislamu huyo akatoweka kwa muda, aliporejea akawa ameambatana na kile kitu kilichokuwa najisi na anakitumia katika jambo linalohitaji utwahara, basi kitu hicho kitahukumiwa kuwa ni twahara ikiwa mtu huyo alijua unajisi wake na ni mjuzi wa hukmu za twahara na najisi.

**Tarirulwasila* mas'ala 10

Vinavyotwahirisha

Maswali

1. Kutembea juu ya sakafu ya simenti au vigae kuna twahirisha nyayo au soli ya kiatu?
2. Masharti ya kutwahirisha kwa jua ni yapi?
3. Taja vitu vitatu vitakavyoweza kuwa na hukmu ya istihala.
4. Mafuta yaliyonajisika ikiwa yatafanyiwa hali ya kikemikali na kupatikana uhalisia wake yatatwahirika?
5. Damu iliyonyonywa na luba kutoka kwa mwanadamu ina hukmu gani? Kwa nini?
6. Kuondoka kwa najisi yenye kuonekana kunasababisha twahara ya... Elezea

Changamoto

Je, kipooza joto kilichopo bafuni na unyevunyevu utokao juu yake vina hukmu ya twahara?

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Somo la Kumi na Mbili.

VINAVYOTWAHARISHA (3)

1. Njia za kuthibitisha twahara.
2. Asili ya Twahara.
3. Hukmu ya Vyombo.

1. Njia za kuthibitisha twahara

Kutwaharika kwa kitu kutathibitika ikiwa:

- a. Mtu mwenyewe atakuwa na yakini ya kutwaharika kwa kitu.
- b. Mmiliki wa kitu kueleza juu ya utwahara wa kitu anachokimiliki.
- c. Watu wawili waadilifu watoe habari juu ya utwahara wa kitu.

Mtoto anayekaribia balegh atakapoeleza juu ya utwahara wa kitu anachokimiliki, maelezo yake yatakubaliwa.

2. Asili ya twahara

Izungumzwapo najisi na twahara ni kwamba kitu chochote kabla haki-jathibitika unajisi wake kinakuwa na hukmu ya twahara, na hakuna haja ya maswali wala uchunguzi.

Mambo ambayo ni mfano wa twahara ni kama

- a. Mtoto anayejinajisi mara kwa mara: mate yake, chakula anacho kibak-isha, na mkono wake uliolowa ikiwa havijathibitika unajisi wake vinakuwa na hukmu ya twahara.
- b. Povu ambalo halijulikani limetoka katika nguo yenye najisi au twahara lina hukmu ya twahara.
- c. Nguo zipelekawazo sehemu maalumu za kuoshea (dry-cleaners) ikiwa

Vinavyotwahirisha

tangu mwanzo hazikuwa na najisi zina hukmu ya twahara, hata kama itajulikana kwamba kunatumika kemikali katika kukaushwa nguo hizi.

- d. Maji yakimwagwa katika sehemu ambayo haijulikani kuwa ni twahara au najisi inatumika hukmu ya twahara.
- e. Maji yanayomwagika kutoka katika magari yanayobeba taka, yana hukmu ya twahara.
- f. Vitu vya urembo kama rangi ya mdomo (lipstick) na vinginevyo vina hukmu ya twahara.
- g. Mguu uliovaliwa kiatu utatwahirishwa kwa ajili ya swala ikiwa kuna uhakika kuwa kiatu hicho kimetokana na ngozi ya mnyama aliyechinjwa kwa njia ambayo si halali na mguu huo ukatoa jasho ndani ya kiatu hicho.
- h. Vifaa vya uchoraji au upakaji rangi ambavyo havijulikani vimetokana na manyoya ya mnyama halali au haramu vina hukmu ya twahara.
- i. Mtu asiyejulikana kama ni Mwislamu au Kafiri ana hukmu ya twahara na si lazima kuuliza juu ya dini yake.
- j. Kuta na milango ya nyumba na hoteli za Makafiri wasiokuwa Ahlul-Kitab kama vile Mabudha pamoja na kila kitu chao na wengineo ni najisi. Ikilazimika inakuwa ni wajibu kutwahirisha vile vitu ambavyo vinahitajika kwa ajili ya swala, kula na kunywa.
- k. Vitu vitumikavyo kwa pamoja kwa Waislamu na wasio Waislamu kama magari, viti, n.k ni twahara.
- l. Alkoholi ambazo hazijulikani kama zina asili ya kilevi au hapana kimi-minika chake kitakuwa na hukmu ya twahara.

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

3. Hukmu za vyombo

- i. Ni haramu kula na kunywa kwa chombo kilichotengenezwa kwa dhahabu au fedha, lakini kwa matumizi mengine kama kuhifadhia maji n.k si haram.
- ii. Chombo kilichotiwa maji ya dhahabu au fedha au kutengenezwa na madini mengine kisha kuchanganywa na dhahabu au fedha hakina hukmu ya dhahabu wala fedha.

Maswali

1. Taja njia za kuthibitisha twahara.
2. Asili ya twahara ina maana gani?
3. Chakula kilichobakizwa na mtoto anayejitia najisi mara kwa mara kina hukmu gani?
4. Nini hukmu ya nguo zinazopelekwa katika mashine ya kukaushia?
5. Nini hukmu ya maji yanayotuama katika barabara?
6. Nini hukmu ya kumiliki kitu cha dhahabu ama fedha?

Changamoto

Baadhi ya dhifa vyakula vyake huletwa katika vyombo vya fedha. Je, huku sio kula kwa kutumia vyombo hivyo? Toa hukmu yake.

Wudhu

Somo la Kumi na Tatu.

WUDHU (1)

1. Maana ya wudhu
2. Jinsi ya kutawadha

1. Maana ya wudhu

Wudhu maana yake ni kuosha uso na mikono na kupaka sehemu ya mbele ya kichwa na juu ya miguu kulingana na masharti maalumu. Kitendo hiki katika sheria ndio utangulizi kwa ajili ya ibada za wajibu na za mustahabu, kama swala, twawafu, kusoma na kuingia msikitini.

2. Jinsi ya kutawadha

- i. Kuosha uso kuanzia mwanzo wa maoteo ya nywele hadi kidevuni.
- ii. Kuosha mikono kuanzia kwenye kiwiko hadi vidoleni.
- iii. Kupaka sehemu ya mbele ya kichwa.
- iv. Kupaka sehemu ya juu ya mguu kuanzia vidoleni hadi kwenye kongo.

i - ii. Kuosha uso na mikono

- a. Katika kuosha uso inalazimu kuosha upana ambao ni sawa na upana kati ya kidole gumba na cha kati.
- b. Kama uso una nywele nyingi inatosha kuosha katika nywele hizo labda kama sehemu ambazo ngozi inaonekana.
- c. Kuosha kunatimia pale maji yatakapoenea katika sehemu zote za kiungo.
- d. Kuosha uso na mikono mara ya kwanza ni wajibu, mara ya pili inajuzu na mara ya tatu haijuzu.

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

iii - iv. Kupaka kichwa na miguu

- a. Kupaka juu ya ngozi ya kichwa si wajibu, bali inatosha kupaka sehemu ya mbele tu ya nywele ila ikiwa nywele za sehemu nyingine zimekusanyika mbele, au nywele za mbele zikiwa ndefu kiasi cha kuangukia mbele katika uso, kupaka nywele za aina hiyo haitajuzu, inabidi kuzisogeza pembeni nywele na kupaka ngozi au nywele za chini kabisa.
- b. Mtu atakayekuwa ameweka nywele za bandia kichwani mwake ikiwa ni kama kofia anaweza kutoa na kupaka.
- c. Mahala pa kupaka miguu ni kuanzia kwenye vidole hadi mwanzo wa ugoko na wala haijathibiti kupaka chini ya vidole.
- d. Kama upakaji wa miguu haukuanzia mwanzo wa vidole na ikapakwa sehemu tu ya juu ya mguu pamoja na vidole kiasi basi wudhu huo utakuwa batili.
- e. Kupaka kichwa na miguu hutumika maji yaliyobaki mikononi baada ya kuosha, kama hakukubaki majimaji mtu hatatakiwa kulowesha mkono bali atachukua majimaji yaliyobaki katika sehemu nyingine ambazo tayari zilishaoshwa kwa nia ya wudhu kama uso na kupaka katika sehemu hizo.
- f. Ihitiyat wajib kichwa kipakwe kwa mkono wa kulia na si lazima kuanzia juu.
- g. Maji ya kupaka hayatakiwi kuchanganyika na maji ya nje mfano mtu akafunga bomba lililo na majimaji kwenye koki yake hali ya kuwa alishaosha mkono wa kulia, kupaka kwa maji hayo kutakuwa na mushkil.
- h. Sehemu inayopakwa ni lazima iwe kavu kuweza kuonekana athari ya kupakwa maji.

Wudhu

- i. Ikiwa sehemu ya kupakwa imeingia najisi ambayo ni vigumu kutolewa, itatumika hukmu ya tayammam.
- j. Mlemavu wa miguu ambaye anatembelea viatu maalumu au magongo ataweza kupaka viatu vyake ikiwa kuna ugumu wa kuvua ili kupaka miguu.
- k. Mtu ambaye hawezi kujizuia kutokwa na upepo, atatakiwa kutawadha kwa kila swala hata kama katikati ya swala alikatikiwa na wudhu kwa athari ya upepo huo.
- l. Hakuna tofauti katika jinsi ya kutawadha kwa mwanamke na mwanaume bali kwa wanaume ni mustahabu kuosha mikono kwa kuanzia nyuma na wanawake mustahabu kuanzia mbele.

Maswali

1. Eleza jinsi ya kutawadha na taratibu zake.
2. Je, kuosha mara tatu kunabatilisha wudhu? Elezea.
3. Nini hukmu ya mtu anayetawadha kwa kufunga na kufungua bomba.
4. Je, unyevunyevu wa kichwa ukigusana na unyevunyevu wa uso wudhu hubatilika?
5. Je kuwepo na kiasi cha maji katika sehemu za kupaka wakati wa kupaka kuna hukmu gani?
6. Elezea tofauti ya wudhu baina wudhu wa mwanamke na wudhu wa mwanaume.

Changamoto

Mtu aliyekatika mkono wa kulia anaruhusiwa kutopaka mguu wa kulia?

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Somo la Kumi na Nne

WUDHU (2)

Masharti ya wudhu

Masharti ya wudhu

- a. Mwenye kutawadha awe na nia ya kutawadha kwa ajili ya Allah (s.w.t).
- b. Mwenye kutawadha asiwe na udhuru (ugonjwa) katika kutumia maji.
- c. Maji ya kutawadhia yawe mutlaq, twahara na mubah, yaani yawe ya halali.
- d. Chombo cha kutawadhia kiwe mubah.
- e. Viungo vinavyotiwa wudhu viwe twahara na kusiwe na kitu chenye kuzuia maji kufika kwenye viungo.
- f. Lazima kufuata mpangilio wa wudhu katika kuosha na kupaka.
- g. Kuwepo na kufuatanisha, yaani kusiwe na ucheleweshaji katika kutawadha kiungo kimoja hadi kingine.
- h. Kuwe na muda wa kutosha baina ya kutawadha na kuswali.

1. Nia

Wudhu lazima ufanywe kwa nia ya kujikaribisha zaidi kwa Allah (s.w.t), basi ikiwa wudhu utafanywa kwa nia nyingine kama vile kujionesha mbele za watu wudhu utakuwa batili.

- i. Maji yasiwe na kizuizi kwa mwenye kutawadha kama ugonjwa, kuzidisha ugonjwa, au kubaki na kiu.
- ii. Maji ya wudhu yawe mutlaq na yasiwe mudhaf.

2. Kutokuweco na kizuizi cha kutumia maji

Mwenye kuhofia kudhurika na maji ya udhu au kuyahitajia kwa ajili ya kiu

Whudhu

basi asitawadhe

3. Maji ya wudhu yawe mutlaq

Haifai kutawadha na maji mudhaf.

4. Maji ya wudhu yawe twahara yasiwe najisi

Ikiwa mtu amepata maji machafu kama maji hayo ni mutlaq anaweza kutawadhia na hakutakuwa na nafasi ya tayammam.

5. Maji ya wudhu yawe mubah

Yasiwe ya mtu au yasitumike bila idhini ya mmiliki, sehemu zilizotengwa za umma zinaweza kutumika kwa wudhu.

Ikiwa idara ya maji imepiga marufuku ufungwaji wa pampu za kupandisha maji, mtu akafunga na kutumia maji hayo kwa ajili ya wudhu, wudhu wake utabatilika. Kama mtu halipi bili ya maji wudhu atakaopata kwa maji hayo yasiyolipiwa ni batili.

Maswali

1. Taja masharti ya wudhu.
2. Maji ya kutawadhia yana masharti gani?
3. Ikiwa maji ni machafu, yatafaa kutawadhia au itatumika hukmu ya tayammam?
4. Kutawadha katika maofisi na majengo ya umma kuna hukmu gani?
5. Ikiwa kumefungwa pampu ya kupandisha maji ambapo idara ya maji imekataza utumiaji wake, Je, maji hayo yatafaa kutawadhia?
6. Mtu ambaye halipi bili ya maji wudhu wake utakuwa sahihi kwa maji yale asiyoyalipia?

Changamoto

Je, ni makruhu kukausha maji baada ya kutawadha?

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Somo la Kumi na Tano

WUDHU (3)

Masharti ya wudhu (2)

6. Uhalali wa chombo

Chombo cha kutawadhia kinatakiwa kuwa halali, yaani kiwe halali katika utumikaji wake, na kama ni mali ya mtu mwingine basi ni lazima kupata ruhsa ya kutumia

7. Utwahara wa viungo vya wudhu

Ni sharti kwa viungo vya wudhu kuwa twahara iwe ni vya kuoshwa au kupakwa.

Ikiwa kiungo cha wudhu kilinajisika baada ya kutawadha, wudhu unabaki kuwa sahihi, ila itawajibika kutwaharisha mahala hapo kwa ajili ya swala.

Ikiwa baadhi ya viungo vya wudhu vina najisi na kisha mtu akatawadha, ikija shaka kwamba najisi iliingia kabla ya wudhu au baada ya wudhu, ikiwa itathibiti kuwapo kwa najisi ile kabla ya wudhu, basi wudhu utabati-lika.

Ikiwa imethibiti kuwa najisi ilitokea baada ya wudhu, basi wudhu utakuwa sahihi ila katika hali zote lazima kutwaharisha sehemu hiyo.

8. Kusiwe na kizuizi

Viungo vya wudhu ni sharti visiwe na kizuizi kitakachozuwia maji kugusa sehemu hiyo, kwani kuwapo kwa kizuizi kunabatilisha wudhu.

a. Mnato wa kawaida unaopatikana kwenye ngozi au nywele hauhisabiki kuwa ni kizuizi; ispokuwa ukiwa ni kwa kiasi cha kuzuia kufika maji.

Wudhu

- b. Rangi ya kucha inazuia maji kugusa ngozi.
- c. Rangi watumiazo wanawake katika nywele na nyusi ikiwa hazina mafuta hazitazuia maji kugusa nywele.
- d. Ganda la chokaa au sabuni linalokuwa kwenye ngozi baada ya kukauka halitazuia maji, ila ikiwa lina unene.
- e. Kitu chochote kitakachokuwa katika mwili ikiwa kitajenga shaka katika kuzuia maji ni vema kikaondolewa.

9. Tartib (mpangilio)

Matendo ya wudhu yanatakiwa kutekelezwa kwa kufuata mpangilio, kutokuwapo na mpangilio kunabatilisha wudhu.

10. Muwalaat (kufuatanisha)

Matendo ya wudhu yanatakiwa kufuatanishwa kwa mfuatano wa kawaida, kwa maana ya kwamba kusiwepo na ucheleweshaji kiasi cha kupoteza hali ya kufuatanisha.

11. Mubasharat

Mwenye kutawadha anatakiwa kufanya matendo yote ya wudhu mwenyewe.

- a. Mtu asiyeweza kutawadha kwa sababu ya maradhi au mengineyo, ni wajibu apate mtu wa kumsaidia, lakini ni wajibu kwa mwenye kutawadha kuweka mwenyewe nia ya kutawadha na kupaka ikiwa ataweza, au atasaidiwa kwa kuchukuliwa mkono wake na kupakwa, na kama hilo pia haliwezekani, msaidizi atachukua unyevunyevu wa maji kutoka katika mikono ya mwenye kutawadha na kumpaka.
- b. Na ikiwa mwenye kutawadha hana mikono au viganja, atachukua maji kutoka katika viwiko, na kama haiwezekani atachukua kutoka usoni.

12. Kuwe na muda wa kutosha

Ikiwa muda ni mchache na iwapo kutawadha kutasababisha swala nzima au kiasi cha swala kuswaliwa nje ya wakati, kwa hali hii wajibu wa mtu ni kutayammam.

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Ikiwa muda wa kutayammam uko sawa na muda ambao ungetumika kutawadha, basi wajibu wa mtu huyo utakuwa ni kutawadha na si kutayammam.

Maswali

1. Taja masharti yanayohusu viungo vya wudhu.
2. Kuna masharti gani wakati wa kutawadha?
3. Kiungo cha wudhu kikinajisika baada ya kuweka wudhu na kabla ya kumaliza wudhu kutakuwa na hukmu gani?
4. Hali ya kuwa na mafuta katika nywele au uso inahesabika kuwa ni kizuizi cha wudhu?
5. Kama kuna kitu kimeganda katika ngozi ila kuna shaka kuwa ni miongoni mwa vinavyozuwia maji au hapana, Je, ni nini hukmu ya kitu hicho?
6. Elezea tofauti kati ya tartib na muwaalat.

Changamoto

Je, kupaka juu ya soksi nyepesi kunatosheleza kupaka mguu?

Wudhu

Somo la Kumi na Sita

WUDHU (4)

1. Wudhu irtimas
2. Wudhu jabira
3. Vinavyobatilisha wudhu
4. Hukmu za wudhu

1. Wudhu Irtimas

Wudhu wa irtimas unafanyika kwa kuzamisha uso au mikono ndani ya maji na kuitoa kwa nia ya wudhu badala ya kumwagia maji juu yake.

Hukmu za wudhu Irtimasi

- a. Ni sharti katika wudhu irtimasi kuchunga hukmu za kuosha kuanzia juu kuja chini.
- b. Inajuzu katika wudhu huu kuzamisha kichwa au mikono mara mbili katika maji, mara ya kwanza kwa nia ya wajib na mara ya pili ni mustahab, kuzidisha zaidi ya mara mbili ni kinyume cha sheria.
- c. Kwa wudhu irtimas nia ya kuosha mikono ni wajibu kuwekwa wakati wa kutoa mikono kutoka majini ili kuwezekana kupaka kichwa na miguu kwa maji hayo.

2. Wudhu wa jabira (bandeji)

Ikiwa bandeji imefungwa kwenye jeraha, wakati wa kutawadha ni wajibu kuosha sehemu zinazowezekana, na kisha kupaka juu ya bandeji kwa unyevu unyevu uliopo mkononi.

Hukmu za wudhu wa bandeji

- a. Ikiwa katika uso au mikono (yaani viungo vya kuosha) kuna jeraha au

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

kidonda kilicho wazi, na kama maji yakigusa hayadhuru basi ni wajibu kuoshwa sehemu hiyo, na kama yanadhuru basi itaoshwa sehemu ya pembeni yake na kwa ihtiyat mkono wenye maji maji upitishwe juu ya jeraha ikiwa hakuna madhara.

- b. Ikiwa katika kichwa au miguu (ambavyo ni viungo vya kupaka) haiwezekani kupaka maji katika sehemu hizo, basi wajibu wake ni kutayammam badala ya kutawadha, ila ikiwa inawezekana kuweka kitamba juu yake na kupitisha majimaji basi kwa ihtiyat kitawekwa kitamba na kupakwa kisha kufanya tayammam.
- c. Ikiwa jeraha halikauki damu daima hata likiwekwa bandeji, kwa hali hii italazimu kupatikana bandeji ambayo hairuhusu damu kusambaa.

3. Vinavyobatilisha wudhu

Mambo yanayotengua na kubatilisha wudhu ni:

- a. Kutokwa na haja ndogo au kubwa.
- b. Kutokwa na upepo.
- c. Usingizi unaopoteza hisia za kusikia na kuona.
- d. Kupatwa na hali inayopoteza fahamu kama kulewa na wendawazimu
- e. kuzimia.
- f. Istihadha.
- g. Kupatwa na hali inayosababisha kuoga, kama vile janaba hedhi n.k.

4. Hukmu za wudhu

- a. Mtu asiyejua mambo yanayotengua wudhu kisha akajua baada ya kuwa yameshamtokea, inamuwajibikia kurudia wudhu kwa kuzingatia matendo ya twahara na kama alishaswali kwa wudhu ule itawajibika kurudia swala ile.
- b. Mtu aliye na shaka nyingi katika matendo ya wudhu au sharti zake, atakapo tia shaka juu ya utwahara wa maji au uhalali wake anatakiwa asishughulishwe na shaka yake.

Wudhu

c. Shaka zipatikanazo katika wudhu ziko za aina mbalimbali:

i. Shaka katika asili ya wudhu

Kama mtu atatia shaka kuwa ametawadha au hapana, katika hali hii ikiwa kabla ya kuswali ni juu yake kutawadha. Na ikiwa ni katikati ya swala, itabidi kukata swala na kutawadha kisha kuianza tena swala hiyo. Na ikiwa ni baada ya kumaliza swala, basi swala yake ni sahihi, lakini ni wajibu wake kutawadha kwa ajili ya matendo mengine yanayohitaji twahara, kama vile swala.

ii. Shaka katika usahihi wa wudhu

Kwa mfano, akitia shaka kwamba wudhu aliotia ni sahihi au la, basi itabidi auchukulie kwamba wudhu wake aliotia ni sahihi.

Maswali

1. Katika wudhu wa irtimasi, Je, inajuzu kuzamisha viungo mara kadhaa katika maji au inajuzu mara mbili tu?
2. Mtu aliye na jeraha au mpasuko katika kiungo cha wudhu anawajibika kufanya nini?
3. Mtu mwenye jeraha katika kiungo cha wudhu ikiwa bandeji haitazuia utokaji wa damu anawajibika kufanya nini?
4. Taja vitu vinavyobatilisha wudhu.
5. Je, mtoto ambaye hajabalegh anaweza kupata hadathi ndogo?
6. Mtu akiwa na shaka kuwa wudhu wake ni batili au sahihi afanye nini?

Changamoto

Mtu anayetawadha tofauti na wengine kulingana na muda hukmu ya wudhu wake itakuwaje ikiwa pindi anapotawadha anachukua muda mrefu sana?

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Somo la Kumi na Saba

WUDHU (5)

Matendo yafuatayo yanahitaji wudhu ili kuyatenda

1. Sharti la kusihi (kukubalika)

Hii ina maana kwamba amali (matendo ya ibada) itendwayo bila wudhu ni batili.

Amali hizo ni

- a. Swala zote na vigawanyo vyake isipokuwa swala ya maiti.
- b. Matendo yaliyosahaulika (katika swala kama vile Tashahud, Salaam na Sijda.
- c. Kufanya twawafu ya wajibu inayokuwa katika ibada ya Hijja au Umra ya wajib au mustahab.

2. Sharti la kujuzu

Hii ina maana kwamba amali ikitendwa bila ya wudhu ni haramu. Amali hizo ni:

- a. Kugusa maandiko ya Qur'an Tukufu.
- b. Kugusa majina ya Allah (s.w.t) na maandishi ya sifa zinazomhusu.
- c. Kugusa majina ya Mitume na Maasumina kwa ihtiyat.

Haijuzu kugusa jina la Allah, na ikiwa limeambatana na jina lingine kama Abdullah. Inajuzu kuandika jina la Allah kwa njia ambayo haitakuwa na ishkali (tatizo) kugusa bila wudhu.

Wudhu

3. Sharti la kukamilika kwa amali

Ni kama vile kuwa na wudhu kwa ajili ya kusoma Qur'an.

4. Kuhakiki

Baadhi ya matendo hayapati uhakika wa kuwa kwake ila kwa kuwa na wudhu kama mtu kutawadha hali ya kuwa ni twahara.

5. Sharti la kuondoa karaha

Kuna baadhi ya matendo ni makruhu (hayapendezi) na karaha yake haiondoki ila kwa wudhu, kama vile kutawadha ili kuondoa makruhu ya kula hali ya kuwa mtu ana janaba. Bila shaka karaha hiyo huondoka kwa kutawadha.

Nukta kuhusiana na kugusa aya na majina ya Allah (s.w.t), Mitume na Maasumin (a.s.)

- a. Si vibaya kuvaa kidani au pete iliyoandikwa aya na majina ya Allah (s.w.t), Mitume na Maasumina (a.s). Ni jambo la wajibu kujiepusha visiguse mwili wakati utakapokuwa huna twahara.
- b. Si sharti kwa mwandishi wa aya za Qur'an na majina matukufu ya Allah (s.w.t), Mitume na Maasumina (a.s) kuwa na twahara, lakini haijuzu kugusa hadi awe na twahara.
- c. Si vibaya kuchapisha aya za Qur'an na majina matakatifu, lakini ni lazima kwa vitakayemfikia mkononi mwake achunge hukmu zake za kisheria kwa kujiepusha kuvunja heshima yake na kuvitia najisi na pia kuvigusa bila ya kuwa na twahara.
- d. Si vibaya kutupa kitu kilichoshikamana na aya za Qur'an katika mto au maji yanayotiririka, ila kama jamii husika italionga kuwa ni kosa.
- e. Si vibaya kuzika aya za Qur'an, ila haijuzu kuzichoma na ikiwa jamii inalikataa basi huwa ni haramu.

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Maswali

1. Je, inajuzu kuchukua wudhu kwa ajili ya swala ya wajibu kabla ya kuingia muda wa swala?
2. Je, Inawezekana kuswali dhuhrain kwa wudhu wa swala ya alfajiri?
3. Ni majina gani matukufu ambayo ni haramu kugusa bila kuwa na wudhu?
4. Kugusa majina kama Abdallah, Habiballah bila kuwa na wudhu kuna hukmu gani?
5. Je, kugusa bendera ya Jamhuri ya Kiislamu ya Iran bila wudhu ni haramu?
6. Je, Inajuzu kugusa maandishi (ya majina ya Allah) yaliyopo juu ya pete?

Changamoto

Je, vipofu wanaosoma Qur'an wakati wa kujifunza au kuigusa kwa mikono maandishi yao maalumu inawalazimu kuwa na wudhu?

Ghusli

Somo la Kumi na Nane

GHUSLI (1)

1. Maana ya ghusli

Ghusli ni kuoga mwili mzima kuanzia kichwa hadi miguu kwa kufuata masharti maalumu.

2. Vigawanyo vya ghusli

Ghusli imegawanyika katika sehemu mbili

a. Ghusli za wajibu

Ambazo nyingine zinawahusu wanawake na wanaume kwa pamoja na nyingine zinawahusu wanawake peke yao tu.

b. Ghusli zinazowahusu wanawake na wanaume ni:

- i. Ghusli ya janaba
- ii. Ghusli baada ya kugusa maiti
- iii. Ghusli ya maiti
- iv. Ghusli kwa ajili ya nadhiri au kiapo.

c. Ghusli zinazowahusu wanawake peke yao:

- i. Ghusli ya Hedhi
- ii. Ghuli ya Nifasi
- iii. Ghusli ya Istihadha

3. Jinsi ya kufanya ghusli

Ghusli inaweza kufanyika kwa njia mbili, nazo ni:

a. Tartib (utaratibu)

Ni kule kuoga mwili mzima kwa utaratibu maalum kwa kuanzia kichwa hadi shingo, kisha kufuata upande wa kulia na hatimaye kushoto.

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

b. Irtimas (kuzama)

Ni kuoga mwili wote kwa kuuzamisha ndani ya maji na kuhakikisha kuwa maji yameenea sehemu zote za mwili. Katika ghusli hii ni wajibu kuhakikisha kuwa nywele zote zinaenea maji hata kama nywele hizo ni ndefu sana. Si wajibu kusimama na kuelekea kibla wakati wa ghusli.

Si vibaya kuanza kuosha mwili au sehemu ya mwili kabla ya kuweka nia ya ghusli au kuanza kufanya ghusli.

Katika ghusli ya tartibi ikiwa mtu hatoufuata utaratibu maalum ama kwa kusahau au makusudi au kwa kutoyajua mas'ala yake, basi ghusli yake inabatilika.

Baada ya kufanya ghusli mtu akigundua kwamba sehemu moja ya mwili haikupata maji, atakuwa na wajibu wa kufanya yafuatayo:

- a. Ikiwa ghusli ni ya irtimas inabidi arudie tena kufanya ghusli, iwe anaijua sehemu ambayo haikupata maji au haijui.
- b. Ikiwa ghusli ni ya tartibi, atarudia kufanya ghusli ikiwa hajui ni sehemu gani haikupata maji, ikiwa anajua hakueneza maji upande wa kushoto basi ataosha sehemu hiyo tu ambayo ilikuwa haikupata maji.
- c. Na kama ni upande wa kulia ataosha sehemu hiyo ambayo haikupata maji na kisha ataosha upande mzima wa kushoto. Na kama ni kichwa na shingo ndio havikupata maji ataosha sehemu hizo na kisha kuosha upande mzima wa kulia na kisha upande mzima wa kushoto.

4. Ghusli jabira

Ghusli ya jabira ina hukmu sawa na wudhu wa jabira.

Ghusli

Maswali

1. Taja ghusli za wajibu.
2. Ghusli zinaweza kufanyika kwa njia ngapi?
3. Je, katika ghusli ya tartibi inatoshwa kuzingatia mpangilio baina ya kichwa na viungo vingine na, Je, ni lazima pia kuzingatia utaratibu baina ya upande wa kulia na kushoto?
4. Je, ni wajibu pia kuosha nywele ndefu?
5. Je, ni wajibu kuelekea kibla wakati wa kufanya ghusli?
6. Mtu atawajibika kufanya nini baada ya ghusli akigundua kuwa moja ya sehemu haikupata maji?

Changamoto

Je, ni sharti kutiririsha maji juu ya mwili wakati wa ghusli?

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Somo la Kumi na Tisa

GHUSLI (2)

5. Masharti ya ghusli

Masharti yote yaliyotajwa katika wudhu pia yanatumika katika ghusli, isipokuwa kuosha kuanzia juu kwenda chini jambo ambalo ni wajibu katika wudhu. Katika ghusli si wajibu kuanza juu kushuka chini, na pia katika ghusli hakuna lazima ya muwalati, yaani kufuatanisha matendo kwa maana kwamba baada ya kuosha kiungo kimoja cha ghusli mtu anaweza kupitisha muda mrefu na hata kujishughulisha na shughuli nyingine na kisha kuen-delea na sehemu inayofuata.

Katika ghusli lazima kutwahirisha kila sehemu ambayo ina najisi kabla ya kufanya ghusli, na ni lazima pia kuondoa kila aina ya kitu ambacho kinaonekana kuwa ni kizuizi katika kufikisha maji (mwilini) wakati wa ghusli.

6. Hukmu za ghusli ni

a. Endapo katikati ya kufanya ghusli mtu akapatwa na hali ambayo inavun-ja wudhu, hali hiyo haipelekei ghusli kuwa batili na wala haitakiwi kuan-za tena ghusli kutoka mwanzo, bali ataendelea na kufanya ghusli kisha kutawadha kwa ajili ya swala.

b. Ikiwa mtu anawajibikiwa na ghusli zaidi ya moja ziwe za wajibu au za mustahabu, anaweza kufanya ghusli zote kwa nia moja, ikiwa baina ya ghusli hizo kutakuwa na ghusli ya janaba, ghusli hiyo itatosheleza ghusli zote zilizo wajibu kwa mtu huyo, ila kwa ihtiyat mustahabu aweke nia kwa ghusli zote zinazomuwajibikia.

c. Ghusli za wajibu zote hazitoshelezi wudhu ila ghusli ya janaba.

Ghusli

- d. Baada ya ghusli mtu akagundua kuwa ilikuwa batili atawajibika kulipa swala zote alizoswali akiwa na ghusli ile.
- e. Shaka katika ghusli kama imefanyika au hapana italazimu kwa mtu kurudia ghusli hiyo ikiwa alitaka kufanya amali ambayo inahitaji ghusli ila swala alizoswali na ghusli hiyo ni sahihi.
- f. Shaka katika ghusli kama ni sahihi au si sahihi ikiwa atakuwa na vigezo vinavyompa usahihi wa jambo hilo, ghusli itakuwa sahihi.

Maswali

1. Je, kuna tofauti gani baina ya masharti ya wudhu na ya ghusli?
2. Je, ni lazima mwili mzima kuwa twahara wakati wa kufanya ghusli?
3. Je, mtu anayefanya ghusli akitokewa na jambo linalovunja wudhu atatakiwa kurudia ghusli yake?
4. Je, mtu mwenye wajibu wa kufanya ghusli zaidi ya moja, atatosheleza ghusli zote kwa kufanya ghusli moja?
5. Kinyume na ghusli ya janaba, Je, ghusli nyingine zinatosheleza wudhu?
6. Je, mtu aliye na shaka kama amefanya ghusli au la ana wajibu gani?

Changamoto

Je, kufanya ghusli na maji yaliyotumika kwa ajili ya ghusli ni sahihi?

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Somo la Ishirini

GHUSLI (3)

7. Ghusli ya janaba

a. Kinachosababisha janaba

Mwanadamu anapata janaba kwa njia mbili:

- i. Kukutana kimwili kwa hali yoyote ile, iwe ya halali au ya haram, manii yatoke ama yasitoke.
- ii. Kutokwa na manii kwa hali yoyote ile, iwe mtu alikuwa macho au kalala, kwa makusudi au bila kukusudia.
- iii. Majimaji yatokayo kwa wanaume ikiwa yaliambatana na ladha ya kijinsia, kuruka na kuchoka mwili yatakuwa na hukmu ya manii, ikiwa hakuna dalili yoyote katika hizo tatu au moja kati ya hizo, hayatakuwa na hukmu ya manii ila kama itathibitika kwa njia nyingine.
- iv. Majimaji yatokayo kwa mwanamke kiasi cha kumfikisha kwenye kiwango cha ladha ya kijinsia na kuchoka, yana hukmu ya manii na lazima afanye ghusli ya janaba, ila kama ana shaka juu ya kutoka kwa majimaji hayo au kufikia kiwango hicho hayatakuwa na hukmu ya manii.
- v. Manii yakiingia katika mfuko wa uzazi bila kujamiiana hayatasababisha ghusli ya janaba.
- vi. Ikiwa itathibitika kuwa sehemu ya kichwa cha uume imeingia kwenye uke basi ni wajibu kwa mwanamke na mwanaume kufanya ghusli ya janaba, hata kama manii hayajatoka, na hata kama mwanamke hajafikia hali ya kupata ladha ya kijinsia.
- vii. Baada ya jimai iwapo mwanamke atafanya ghusli hali ya kuwa manii

Ghusli

bado yamebaki katika fuko lake la uzazi na baada ya kufanya ghusli manii yakatoka ghusli yake itakuwa sahihi na manii yaliyotoka baada vya hapo ni najisi. Na kama manii hayo ni ya mwanaume, basi haitakuwa wajibu kwake kufanya ghusli.

viii. Baada ya mwanamke kufanyiwa vipimo kwa ndani kwa kutumia vifaa vya tiba, maadam manii hayakutoka basi haitakuwa wajibu kwake kuoga.

b. Mambo yaliyo haram kwa mwenye janaba ni

- i. Kugusa maandishi ya Qur'an na majina na sifa za Allah (s.w.t) pamoja na majina ya Mitume (a.s) na Maasumina (a.s) kwa ihtiyat wajib.
- ii. Kuingia katika misikiti mitukufu ya Makka (Masjidul-Haram) na Madina (Masjidun-Nabii) hata kwa kupita mlango mmoja na kutokea mwingine.
- iii. Kusimama ndani ya misikiti mingine ila yawezekana kuingia kwa mlango mmoja na kutokea mwingine.
- iv. Kuweka kitu msikitini.
- v. Kusoma aya zilizo na sijda ya wajibu ambazo ni aya ya kumi na tano ya Sura ya thelathini na mbili (Sajda), aya ya thelathini na saba ya Sura ya arobaini na moja (Fuswilat), aya ya sitini na mbili ya Sura ya hamsini na tatu (An-Najm), na aya ya kumi na tisa ya Sura ya tisini na tisa (Al-Alaq). Hizi ni Sura ambazo msomaji na msikilizaji wanakuwa na wajibu wa kusujudu mara wanaposoma au wanaposikia, ila si vibaya kusoma aya nyingine zilizobakia.

Haijuzu kuingia katika maziara ya Maasumina kwa mwenye janaba. Kumbi ambazo hutumika kwa ajili ya ibada za swala za jamaa hazina hukmu za misikiti.

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

c. Hukmu za ghusli ya janaba

- i. Katika kutekeleza wajibu wa kisheria udhuru unakubalika. Kwa mtu aliye na udhuru wa kufanya ghusli ya janaba anawajibikiwa kufanya tayammam.
- ii. Ikiwa mtu anajua kwamba akikaribiana na mwenza wake atakuwa na wajibu wa kufanya ghusli ya janaba hali ya kuwa hana maji au wakati haumruhusu kufanya ghusli ili aweze kuwahi muda wa swala, anaweza kufanya tayammam na hata kufanya amali nyinginezo kwa tayammamu hiyo, ila ikiwa udhuru wake ulikuwa ni uchache wa muda, tayammam yake itatumika kwa ajili ya ibada aliyokusudia tu na si nyinginezo baada ya hapo.
- iii. Mtu aliyefanya ghusli ya janaba akitokwa na maji maji ambayo hajui kuwa ni ya manii au la, ikiwa kabla ya kufanya ghusli hakufanya istibraa kwa kwenda haja ndogo kwanza, majimaji hayo yatakuwa na hukmu ya manii na atawajibikiwa kufanya ghusli.
- iv. Kitu kikiingia katika nguo kama hakijajulikana kuwa ni manii au la, na kama kimetoka kwa mhusika au la, hakitakuwa na hukmu ya manii.
- v. Mtu aliyefanya ghusli ya janaba hatakiwi kutawadha bali ghusli yake inatosheleza matendo yote ya ibada yanayohitaji wudhu.
- vi. Baada ya ghusli ya janaba, mtu akiwa na shaka juu ya ghusli yake kubatilika, hatakuwa na lazima ya kutawadha kwa ajili ya swala, ila atafanya hivyo kwa ihtiyat.

Maswali

1. Sababu za janaba ni zipi?
2. Ni vipi majimaji yatokayo kwa mwanaume yatahukumiwa kuwa ni manii?

Ghusli

3. Janaba itathibiti vipi kwa mwanamke bila kujamiiana?
4. Je, mwanamke anao wajibu wa kufanya ghusli ya janaba baada ya kufanyiwa matibabu sehemu ya njia ya siri?
5. Ni mambo gani yanakuwa haramu kwa mwenye janaba?
6. Kama kuna doa katika nguo na halijulikani kuwa ni la manii au la kitu kingine, Je, ni nini hukmu yake?

Changamoto

Nini maana ya **haram** za maasumina (a.s) ambazo ni haijuzu kuingia kwa mwenye janaba?

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Somo la Ishirini na Moja

GHUSLI (4)

Ghusli zinazowahusu wanawake

8. Ghusli zinazowahusu wanawake ni

a. Hedhi

- i. Damu aionayo binti kabla ya kutimiza miaka tisa haina hukmu ya hedhi.
- ii. Matone ayaonayo mwanamke baada ya kuwa na yakini juu ya utwahara wake, ikiwa si damu hayatakuwa na hukmu ya hedhi, na kama ni damu hata kama imeingia katika rangi ya njano, na haijapita idadi ya siku kumi, matone hayo yana hukmu ya hedhi, na mwanamke mwenyewe ndiye atakayethibitisha hilo.
- iii. Wanawake wanaotumia madawa ya kuzuia ujauzito, ikiwa wataona matone ya damu, haitakuwa hedhi mpaka athibitishie, na damu hiyo itakuwa ni istihadha.
- iv. Mwanamke aliye na idadi maalumu ya siku za hedhi ikiwa ataweka kizuizi cha ujauzito na akapata damu kwa zaidi ya siku kumi, damu ya idadi ya siku zake ni hedhi na zilizozidi itakuwa ni istihadha.
- v. Mjamzito akiona damu ikiwa ina masharti ya hedhi itakuwa na hukmu ya hedhi na kama haikuwa na sifa hizo itakuwa ni istihadha.

Hukmu za hedhi ni

- i. Mambo yote yaliyokuwa haramu kwa mwenye janaba ni haramu pia kwa mwenye hedhi.
- ii. Si haramu kwa mwanamke aliye katika hedhi kukaa juu ya ukuta

Ghusli

unaotenganisha baina ya Masjidul-Haram na sehemu ya kufanyia Sa'i baina ya Safa na Marwa isipokuwa endapo kama itathibitika kuwa ukuta huo unaungana na Masjidul-Haram.

- iii. Mwanamke aliye na hedhi kisha akapata janaba au aliye na janaba kisha akapata hedhi anatakiwa kufanya ghusli ya janaba baada ya ile ya hedhi, ila kwa ihtiyat mustahab atafanya ghusli moja kwa nia ya zote.
- iv. Mwanamke hawezi kufanya ghusli ya janaba hali ya kuwa ana hedhi.
- v. Mwanamke akifunga swaumu siku maalum kwa nia ya nadhiri, ikiwa atapata hedhi akiwa na swaumu, swaumu yake itabatilika na atatakiwa kulipa baada ya kumalizika kwa hedhi yake.

b. Istihadha

Damu aipatayo mwanamke baada ya umri wa kukoma hedhi ina hukmu ya istihadha. Kwa hiyo mwanamke ambaye baba yake hatokani na Bani Hashim hata kama mama yake ni katika ukoo wa masharifu (Sayyida), baada ya kutimiza miaka hamsini, damu atakayopata ina hukmu ya istihadha.

c. Nifas - damu ya uzazi

Mwanamke aliyeharibu mimba damu itakayotoka baada ya hapo ina hukmu ya nifas. Kila jambo lililo haramu kwa mwenye hedhi ni haramu pia kwa mwenye nifas.

Maswali

1. Je, mwanamke akiona matone baada ya kujitwahirisha na ikiwa hayakuwa na sifa yoyote ya damu wala kuchanganyika na damu, matone hayo yatakuwa na hukmu gani?
2. Je, mama mjamzito akipata damu ambayo haitampelekea kutokwa na ujauzito, damu hiyo itakuwa na hukmu gani?
3. Mwanamke mwenye hedhi kisha akapata janaba, au mwanamke mwenye janaba kisha akapata hedhi baada ya kujitwahirisha na hedhi,

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Je, atawajibikiwa na ghusli zote mbili?

4. Je, kwa mwanamke mwenye hedhi inajuzu kufanya ghusli ya janaba wakati bado ana hedhi?
5. Damu aipatayo mwanamke baada ya kukoma umri wa kupata hedhi ina hukmu gani?
6. Je, mwanamke aliyetoa mimba ana hukmu ya nifas au la?

Changamoto

Inajuzu kuzuwia damu ya hedhi ili kufunga mwezi wa Ramadhani?

Hukmu za Maiti

Somo la Ishirini na Mbili

HUKMU ZA MAITI (1)

1. Ghusli baada ya kugusa maiti
2. Hukmu za muhtadhar
3. Mambo yaliyo wajibu baada ya kifo

1. Ghusli ya kugusa maiti

Mtu akigusa maiti ambayo imeshapoa na haijaoshwa itamlazimu kufanya ghusli ya kugusa maiti.

Kugusa kiungo cha maiti kilichojitenga na kiwiliwili ikiwa kimeshapoa kina hukmu ya kufanya ghusli ya kugusa maiti.

Kugusa kiungo cha mwanadamu aliye hai ikiwa kimejitenga na kiwiliwili, haina hukmu ya ghusli ya maiti.

Baadhi ya maiti zikiguswa hazihitaji ghusli ya kugusa maiti, hizo ni:

- a. Maiti ya shahidi aliyekufa katika vita vya jihad (katika njia ya Allah.
- b. Maiti ambayo haijapoa.
- c. Maiti ambayo imeshaoshwa kwa ghusli tatu.

Ikiwa kuna shaka kuwa maiti ilioshwa au la, basi mtu akiigusa atakuwa na wajibu wa kufanya ghusli ya kugusa maiti.

Ikiwa aliigusa hali ya kuwa maiti imekwishapoa, bila kufanya ghusli ya kugusa maiti hiyo, swala yake itakuwa si sahihi.

Mtu akifanya ghusli ya kugusa maiti ana wajibu wa kufanya wudhu ikiwa anataka kuswali.

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

2. Hukmu za mtu anayekaribia kufa (muhtadhar)

Mwislamu anayekaribia kufa ni vizuri akalazwa chali na miguu yake kuelekezwa kibla. Kitendo hiki kinaweza kufanywa hata na mwenyewe ikiwa anaweza. Maulama wakubwa wamesema hilo ni wajibu; kwa hiyo kwa ihtiyat ya wajib kisiachwe.

3. Wajibu baada ya kifo

Mtu akifa kuna mambo yanakuwa ni wajibu kufanywa juu yake. Mambo hayo ni:

- a. Anatakiwa kuoshwa ghusli tatu.
- b. Hunut: Ni kupakwa Karafuumaiti katika sehemu saba zinazogusa chini wakati wa kusujudu.
- c. Kuvikwa sanda.
- d. Kuswaliwa swala ya maiti.
- f. Kuzikwa - kufukiwa ndani ya udongo (kaburini).

Katika Uislamu, Mwislamu akifa bado anastahiki heshima kama alivyokuwa hai, na kumkirimu maiti wa Kiislamu kunaendana na matendo ambayo yamo katika sheria ya Kiislamu.

Kuosha, kuvika sanda, kuswalia na kuzika ni katika wajibu wa kutoshelezana (Wajib kifai), na wajibu juu ya kila mukallaf, isipokuwa kama baadhi ya mukallaf wakilitenda jambo hilo, wajibu unaondoka kwa wengine. Na kama hakuna mukallaf atakayetekeleza wajibu huu, basi watu wote watakuwa wamefanya maaswi.

Ikijulikana moja kati ya mambo ya wajibu kwa maiti yamefanywa kimakosa, lazima wajibu ule urudiwe, isipokuwa kama ikidhaniwa kuwa ilikosewa, si lazima kurejea tena.

Hukmu za Maiti

Wajibu wowote unaotakiwa kutekelezwa juu ya maiti, ni lazima ipatikane idhini kutoka kwa walii wake, akiwa ni baba, mama, au watoto na kwa mke idhini inatoka kwa mume wake.

Maswali

1. Je, kugusa kiungo cha maiti kilichokatika kutoka kwenye kiwiliwili kunahitaji kufanya ghusli ya maiti?
2. Je, kugusa kiungo cha mtu kilichokatika akiwa hai kuna hukmu ya ghusli?
3. Taja, ni katika njia gani mtu akigusa maiti anawajibikiwa na ghusli?
4. Je, Mwislamu anayekaribia kufa anapaswa kulazwa na kugeuzwa kuelekea kibla?
5. Je, ni mambo gani yanakuwa ya wajibu kuyafanya baada ya Mwislamu kufa?
6. Ghusli ya maiti ni wajibu unao muwajibikia kila mtu kwa nafsi yake au ni wajibu wa kutosheleza?

Changamoto

Je, ikiwa wakati wa kung'oa jino kipande cha fizi kikang'oka pamoja na jino, kikishikwa kinahitajika ghusli?

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Somo la Ishirini na Tatu

HUKMU ZA MAITI (2)

4. Ghusli ya maiti

Maiti anawajibikiwa kuoshwa (ghusli), kwa maji yaliyochanganywa na majani ya Mkunazi, maji yaliyochanganywa na Karafuumaiti na kisha maji halisi yaliyokuwa Mutlaq.

Mtu anayefanya ghusli ya maiti anatakiwa awe

- a. Mwislamu mfuasi wa Maimamu kumi na mbili.
- b. Balegh.
- c. Mwenye akili timamu.
- d. Mjuzi wa mas'ala ya kuosha.
- e. Awe ni jinsia moja na maiti.
- f. Mke ana ruhusa ya kuosha maiti ya mumewe na kadhalika mume ana ruhusa kumwosha mkewe.

Katika kuosha maiti kama ilivyo kwa ibada nyingine ni wajibu kuweka nia na iwe ni kwa ajili ya kujiweka karibu zaidi na Allah (s.w.t).

Maiti ambayo ni wajibu kuoshwa ni lazima iwe ya

- a. Mwislamu mwanamke au mwanaume.
- b. Mtoto wa Kiislamu.
- c. Mtoto wa miezi minne ikiwa mimba iliharibika.

Ikiwa moja ya sehemu ya maiti ilikuwa na najisi italazimika kuondolewa kwanza kabla ya kufanyiwa ghusli.

Ikiwa maiti ina jeraha ambalo damu haikatiki itawajibika kutumia njia yoyote ili kuizuia ile damu isiendelee kutoka hata kama ni kwa njia za

Hukmu za Maiti

kitabibu.

Ni haramu kuangalia sehemu za siri za maiti na mwoshaji akiangalia sehemu hizo atahesabika amefanya maasi lakini ghusli itabaki kuwa sahihi.

Ikiwa maji hayakupatikana au kuna kizuizi katika utumiaji wa maji italazimika maiti afanyiwe tayammam badala ya kila ghusli.

5. Hunut

Ni wajibu kwa maiti baada ya kuoshwa afanyiwe hunut, yaani kumpaka kafur katika sehemu ambazo hugusa chini wakati wa kusujudu, ambazo ni paji la uso, viganja na magoti pamoja na ncha za vidole gumba vya miguu.

Kafur ni lazima iwe mpya yenye kuweza kutoa harufu, kafur ya zamani iliyopoteza harufu haitafaa kutumika.

Mtu aliye katika Ihram hatawajibikiwa na hukmu hii ya hunut.

6. Sanda (kaffan)

Maiti ya Mwislamu inatakiwa kuvikwa sanda kwa kutumia vitambaa vitatu:-

- a. Msuli unaoanzia kiunoni hadi miguuni.
- b. Kanzu ivaliwayo kuanzia mabegani hadi chini ya magoti.
- c. Shuka litakalofunika mwili mzima kuanzia kichwa hadi miguu kiasi cha kuweza kufunga ncha zake, na lazima iwe pana kiasi kwamba pande zake mbili ziweze kupishana.

Iwapo sanda ya maiti imenajisika kutokana na najisi itokayo kwa maiti au nje ya hapo inalazimika kukatwa kwa sehemu hiyo ikiwa sanda haitaonyesha, au yawezekana kuibadilisha sanda hiyo na kama ikishindikana basi inajuzu kwa maiti kuzikwa akiwa na sanda iliyonajisika.

Mtu anaweza kujinunulia sanda na pia kuiweka mahali pa wazi wakati wa kuswali swala za wajib au sunna na hata wakati wa kusoma Qur'an.

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Mtu aliyenunua sanda kwa ajili yake anaweza kuitumia kumvika mzazi wake au jamaa yake wa karibu.

Maswali

1. Taja ghusli tatu anazotakiwa kufanyiwa maiti.
2. Taja masharti ya mtu anayeosha maiti.
3. Je, ni wajibu kuosha mwili wa mtoto aliyekufa tumboni akiwa na miezi minne?
4. Nini maana ya hunut kwa maiti?
5. Vitambaa anavyovalishwa maiti kwa maana ya sanda ni vitatu. Je, ni vipi hivyo?
6. Je, mtu aliyejinunulia sanda inajuzu kuitumia kwa maiti nyingine?

Changamoto

Nini hukmu ya mtoto aliye tumboni kwa mama mjamzito aliyefariki?

Hukmu za Maiti

Somo la Ishirini na Nne

HUKMU ZA MAITI (3)

7. Swala ya Maiti

- a. Baada ya kufanyiwa hunut na kuvikwa sanda, maiti ya Mwislamu inawajibika kuswaliwa kulingana na taratibu zilizowekwa kisheria.
- b. Mtoto aliyekamilisha miaka sita akifa ana wajibu wa kuswaliwa hata kama mmoja wa wazazi wake si Mwislamu.
- c. Swala ya maiti inaambatana na nia na takbira tano ambazo ndani yake kuna dua na kumswalia Mtume (s.a.w.w) kama hivi:

- i. Baada ya takbira ya kwanza atasema:

Ash-hadu an Laa ilaaha illa-Llahu wa Ash-hadu anna Muhammadan Rasulallah

- ii. Baada ya takbira ya pili: Atamswalia Mtume (s.a.w.w) kwa kusema:

Allahumma Salli alaa Muhammadin wa Aali Muhammadin

- iii. Baada ya takbira ya tatu: Atawaombea maghfira Waislamu atasema:

Allahumma ighfir lil-Muuminina Wal-Muuminaat

- iv. Baada ya takbira ya nne: Atamuombea maghfira maiti kwa kusema:

Allahumma ighfir Lihadhal-Mayyit (Ikiwa maiti ni mwanaume)

na akiwa mwanamke atasema:

Allahumma ighfir Lihadhihil-Mayyitah

- v. Kisha atasoma takbira ya tano, na swala ya maiti itakuwa imekamilika.

Baadhi ya vitabu vimeeleza swala hii kwa urefu zaidi.

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

- a. Swala ya maiti inaswaliwa katika hali ya kusimama na kuelekea kibla na maiti ilazwe chali huku kichwa kikiwa upande wa kulia wa wanaoswalia na miguu kuwa upande wa kushoto.
- b. Kusiwe na kizuizi chochote hata pazia baina ya maiti na wanaomswalia. Hakuna ubaya kama itakuwa ndani ya jeneza.
- c. Hakuna sharti ya kuwa na wudhu au twahara katika mavazi na mwili katika swala ya maiti.
- d. Ikiwa kwa sababu mbalimbali maiti haikuswaliwa au baada ya kuzikwa ikagundulika kuwa aliswaliwa kimakosa, inabidi kuswali juu ya kaburi lake ikiwa bado mwili haujaribika kabisa.
- e. Katika swala ya maiti hakuna masharti kama yale yaliyopo katika swala ya jamaa na Imam anayeswalisha swala ya jamaa na mengineyo, ingawa ni vema masharti hayo yakazingatiwa.

8. Kuzikwa

- a. Baada ya kukamilisha majukumu yote juu ya maiti kama tulivyoona, maiti inatakiwa kuzikwa kwa kufukiwa ndani ya udongo, na kaburi linatakiwa kuwa refu kiasi kwamba harufu isiweze kusikika wala wanyama wakali wasiweze kufukua.
- b. Maiti anatakiwa kulazwa kwa ubavu wa kulia na sehemu ya mbele ya mwili wake ielekee kibla.
- c. Mfupa wa mwanadamu aliyekufa si najisi lakini ni wajibu kuuzika tena.
- d. Fuvu la mwanadamu linatakiwa kuzikwa haraka na hajuzu kuliweka kama maonyesho.
- e. Inajuzu kujengea kaburi la Mwislamu ikiwa jambo hili halitapelekea kuvunja kwa kaburi wala kuvunja hadhi ya Mwislamu.

Hukmu za Maiti

- f. Kama mtu ametumbukia kisimani na kufariki, na maiti yake ikashindikana kutolewa, hapo ndipo patakuwa kaburi lake na ni wajibu kisima hicho kifukiwe.
- g. Ni mustahabu kunyunyiza maji juu ya kaburi baada ya kuzika.

9. Hukmu za kuvunja kaburi

- a. Haijuzu kuvunja kaburi la maiti iliyozikwa kwa kufuata sheria za Kiislamu hata ikiwa kwa ajili ya kutanua mtaa au barabara.
- b. Ikiwa italazimika kuvunja kaburi basi ni wajibu kuzika mwili wa Mwislamu au mifupa ambayo bado haijahiribika.
- c. Inajuzu kuvunja kaburi na kuzikwa maiti nyingine ikiwa ya mwanzo imeshakuwa mchanga.
- d. Kunyunyiza maji juu ya kaburi siku ya kuzikwa maiti ni jambo la mustahabu, ama baada ya maziko jambo hilo halina tatizo kwa lengo la kufanya wema.
- e. Ijaza ya marjaa taqliid haitakuwa na athari katika mambo ambayo haijuzu kwayo kubomoa kaburi.

10. Hukmu ya shahidi

- a. Hukmu ya ghusli na sanda haihusiani na shahidi.
- b. Shahidi ni yule ambaye amekufa katika uwanja wa vita, hivyo kukiwa na vita baina ya makundi mawili kundi la haki na kundi la batili, watakaokufa kutoka upande wa haki watakuwa mashahidi. Lakini watu wanaokufa nje ya uwanja wa vita hata kama watakuwa na malipo sawa na shahidi, hawatakuwa na hukmu ya shahidi.

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Mfano ni yule mtu aliyekufa akiwa anatekeleza hukmu za Kiislamu.

11. Hukmu za kunyonga

- a. Mwislamu aliyehukumiwa kunyongwa ana hukmu zote za Mwislamu, na hukmu zote za maiti wa Kiislamu zinamstahiki, mfano swala ya maiti n.k.
- b. Sharti la kijinsia linasimama katika hukmu ya kuosha maiti, kinyume na hilo ghusli itakuwa batili (ila kama ni baina ya mke na mume). Ama katika kuvika sanda na kuzika hakuna ulazima wa kijinsia.
- c. Inajuzu kwa mwanamke kusindikiza jeneza na hata kulibeba.

Maswali

1. Eleza namna ya swala ya maiti inavyoswaliwa.
2. Mtu ambaye hajatimiza masharti ya kuwa Imam wa jamaa anaruhusiwa kuwa Imam wa swala ya maiti ya muumini?
3. Je, inajuzu kujengea kaburi kwa zaidi ya tabaka mbili?
4. Ni shahidi gani anayeondokewa na hukmu ya joshu na sanda?
5. Ikiwa mahakama imetoa hukmu ya kunyongwa kwa mtu aliyekamatwa na madawa ya kulevya, Je, maiti hiyo itaruhusiwa kuswaliwa?
6. Je, hukmu ya jinsia inaingia katika suala la kuosha, kuvika sanda, na kuzika?

Changamoto

Je, inajuzu kuzika wakati wa usiku?

Tayammam

Somo la Ishirini na Tano

TAYAMMAM (1)

1. Yanayohusu tayammam

Kuna Mambo ambayo ikiwa mtu yatamtokea atatayammam badala ya ghusli au wudhu, mambo hayo ni:

- a. Ikiwa ni vigumu kupata maji, au hakuna maji au maji yako mbali mfano chini kabisa ya kisima ambapo mtu hana chombo cha kuweza kuyachota.
- b. Ikiwa maji yana madhara kwa mtumiaji. Kwa mfano mtu akitumia maji kuna uwezekano wa kupata maradhi au maradhi aliyonayo yatachelewa kupona iwapo atatumia maji hayo, basi ana wajibu wa kutayammam. Na ikiwa atatumia maji na yakamdhuru, wudhu au ghusli itakuwa ni batili.
- c. Kama atatumia maji kwa ajili ya wudhu au kuoga, kutakuwa na hofu ya kiu cha nafsi yake mwenyewe au nafsi ya kiumbe ambacho ni wajibu wa kukihifadhi.
- d. Endapo atataka kuyatumia maji yaliyopo kwa kutwahirishia mwili wake au nguo zake kutokana na najisi ili aswali na hakuna maji mengine isipokuwa hayo.
- e. Ikiwa ni haramu kutumia maji hayo au chombo kama vitakuwa ni vya ghasbi. Kwa maana hiyo haijuzu kuvitumia.
- f. Ikiwa wakati utakuwa hautoshi kiasi kwamba lau atataka kutawadha au kuoga, basi swala yake au sehemu fulani ya swala hiyo itaingia nje ya wakati.

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Mwenye kuitakidi kwamba lau atatumia maji kutawadha au kuoga maji kwa ajili ya ghusli, maji hayo yatamdhuru (kwa maana ya kuwa atapatwa na maradhi fulani), basi hakuna tatizo kwake kutayammamu na swala yake itaswihi.

Lakini, ikibainika kabla ya kuswali kwa tayammamu hii kwamba hakuna madhara juu yake basi tayammamu yake itabilika na itambidi aswali kwa twahara ya wudhu.

Ama kama itamdhihirikia kwamba hakuna madhara juu yake baada ya kuswali kwa tayammamu ile, basi ni ihtiyaat wajibu kutawadha au kuoga na kisha kuilipa swala ile.

Mukallafu atakapatwa na janaba na nguo zake au mwili wake ukawa na najisi, na wakati ukawa hautoshi kutwahirisha mwili au nguo au kubadili nguo hizo na wala hakuna uwezekano wa kuswali bila nguo kutokana na baridi au jambo jingine, basi itamuwajibikia kutayammamu badala ya kuoga na ataswali na nguo hizo na mwili huo wenye najisi na si wajibu juu yake kuilipa swala hiyo.

2. Vinavyofaa kufanyia tayammam

Ni sahihi kutayammam katika kitu chochote kinachotokana na ardhi, kama vile mchanga wa kila aina, mawe ya kila aina, chokaa na mfano wa hivyo.

Haijuzu kutayammam juu ya madini ambayo hayazingatiwi kuwa sehemu ya ardhi.

Inawezekana kutayammam katika marumaru ingawa ni vema kuepuka hilo.

3. Jinsi ya kutayammam.

a. Nia

b. Kupiga viganja viwili katika sehemu inayofaa kutayammam.

Masharti ya Tayammam

- c. Kupaka kwa viganja vyote juu ya paji la uso na pande zake mbili kuanzia maoteo ya nywele hadi juu ya nyusi na juu ya pua.
- d. Kupaka nyuma ya kiganja cha kulia kwa kutumia kiganja cha kushoto na kupaka nyuma ya kiganja cha kushoto kwa kutumia kiganja cha kulia.
- e. Kwa ihtiyat wajib kupiga kwa mara ya pili viganja katika sehemu iliyo sahihi kutayammam kisha kupaka nyuma ya viganja kwa kuanza kulia kisha kushoto.

Taratibu ya kutayammam haina tofauti iwe ni badala ya wudhu au ghusli.

Kama sehemu ndogo tu ya paji la uso au viganja haikupakwa basi tayammamu itabatilika, iwe kwa kusahau, kutokujua au hata kwa makusudi.

4. Tayammam ya Jabira

Mtu anayewajibikiwa kufanya tayammam ikiwa katika maeneo ya kufanyia tayammam au mkono wenyewe kuna jabira atatayammam kwa hali hiyo hiyo.

Maswali

1. Taja mambo yanayokuwa wajibu katika kutayammam.
2. Je. Mtu ambaye hakufanya ghusli kwa itikadi ya kuwa maji yanamduru ana hukmu gani?
3. Ikiwa mtu anahisi tabu kwenda bafuni Je, anaweza kutayammam kwa ajili ya ibada za mustahab.
4. Je, mwenye janaba anaruhusiwa kuswali kwa tayammam akiwa na nguo au mwili wenye najisi au baada ya kutwahaisha na kufanya ghusli arudie tena swala yake?
5. Nini hukmu ya kutayammam juu ya mawe, chokaa na mfano wa hayo?

Changamoto

Je, Inajuzu kutayammam katika vitu ambavyo kimsingi ni sahihi kufanyia tayammam lakini viko katika ukuta au mfano wake?

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Somo la Ishirini na Sita MASHARTI YA TAYAMMAM

5. Masharti ya Tayammam ni

- a. Kitu kinachofanyia tayammam kiwe twahara
- b. Kitu cha kufanyia tayammam kiwe cha halali. Ikiwa mtu hakujua au alisahau kuhusiana na uhalali wa kitu hicho, hapo tayammam itakuwa sahihi.
- c. Tayammam lazima ianzie juu kuja chini.
- d. Lazima kuzingatiwa utaratibu.
- e. Tayammam ifanywe kwa kufuatanisha.
- f. Mtu asisaidiwe katika tayammam.
- g. Kusiwe na kizuizi katika sehemu zinazofanyiwa tayammam, hata kama ni pete. Vinyweleo vya mikononi si kizuizi katika tayammam, lakini nywele za kichwa zikiteremka juu ya paji la uso ni wajibu kuzinyanyua wakati wa kutayammam.
- h. Inajuzu kutayammam juu ya sehemu iliyofungwa bendeji kutokana na jeraha ikiwa kufungua kuna madhara.
- i. Viungo vya tayammam si lazima kuwa twahara ingawa kwa ihtiyat ni bora zaidi.

6. Hukmu za tayammam ni

- a. Ikiwa hakikupatikana kitu cha kufanyia tayammam inawezekana kufanyika katika vumbi linalotoka katika zulia au nguo. Na ikishindikana hivyo basi itafanyika hata katika udongo ulioroa. Ikishindikana, basi mtu ataswali bila wudhu kisha baadaye atatawadha au kufanya ghusli (kwa mfano mtu anaye safiri kwa ndege) na kuilipa tena swala ile.
- b. Mtu aliye na wajibu wa kutayammam hawezi kutayammam kabla ya kuingia kwa muda wa swala, ila kama alitayammam kabla ya swala kwa ajili ya ibada za mustahab ataweza kuswali kwa tayammam hiyo

Masharti ya Tayammam

- hiyo.
- c. Kama dharura ya mtu inaisha wakati wa mwisho wa swala italazimu asubiri na swala yake aiswali mwisho wa wakati badala ya kuswali kwa tayammam mwanzo wa wakati.
 - d. Mtu anayetayammam badala ya ghusli, kama udhuru wake bado unaendelea na akatokwa na hadathi ndogo kama vile mkojo, italazimu kwa ihtiyat wajib atayammam tena na kisha atawadhe na ikiwa kutawadha pia ni kugumu basi ni lazima atayammam tena badala ya wudhu.
 - e. Tayammam hubatilika pindi tu udhuru unapomalizika.
 - f. Vinavyobatilisha wudhu na ghusli pia vinabatilisha tayammam badala ya wudhu na ghusli.
 - g. Taratibu zote za kisheria kuhusu ghusli, zinafaa kutekelezwa katika tayammam iliyofanywa badala ya ghusli, isipokuwa tu kama tayammam ilifanyika kutokana na uchache wa muda. Hakuna tatizo kuingia msikitini, kuswali, kugusa maandiko ya Qur'an tukufu na kufanya matendo mengine ambayo yana sharti ya twahara inayotokana na janaba.

Maswali

1. Taja masharti ya tayammam.
2. Je, ni lazima kuvua pete na mfano wake katika tayammam?
3. Je, nywele za mwili ni kizuizi katika tayammam?
4. Je, viungo vya tayammam ni lazima kuwa twahara?
5. Kama mukallaf hawezi kutawadha na pia ni vigumu kwake kutayammam nini wajibu wake?
6. Je, tayammam badala ya ghusli ina athari na hukmu sawa na ghusli ya kawaida?




Changamoto

Kama mtu ameloa kwa manii akiwa msikitini na baada ya kuamka ikawa ni vigumu kutoka humo, Je, mtu huyo ana wajibu gani?



Sehemu ya Tatu

SWALA



Aina za Swala

Somo la Ishirini na Saba

AINA ZA SWALA

Swala za wajib na mustahab

1. Swala za Wajib ni:

- a. Swala za kila Siku.
- b. Swala baada ya twawaf.
- c. Swala ya majanga.
- d. Swala ya maiti.
- d. Swala ya qadhaa ya baba na mama ambayo ni wajibu juu ya mtoto mkubwa wa kiume.
- f. Swala iliyo wajibu kwa nadhiri au kiapo au ujira.

Swala za mustahab ziko nyingi sana na huitwa **nafila**. Swala hizo za nafila za mchana na usiku zimesisitizwa sana.

2. Nafila za kila siku (mustahab)

Kila swala moja ya wajibu katika swala tano ina swala ya nafila. Kuswali nafila hizi ni muhimu na zina thawabu nyingi.

Nafila ya usiku ni kuanzia nusu ya usiku hadi adhana ya alfajiri. Ni bora zaidi ikasaliwa wakati wa robo ya mwisho ya usiku yaani karibu na alfajiri.

Swala za nafila ni

- a. Rakaa nane kabla ya swala ya adhuhuri.
- b. Rakaa nane kabla ya swala ya alasiri.
- c. Rakaa nne baada ya swala ya maghrib.
- d. Rakaa mbili baada ya swala ya isha ambazo huswaliwa kwa kukaa.
- e. Rakaa mbili kabla ya swala ya asubuhi.

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

f. Rakaa kumi na moja za swala ya tahajjud.

Jumla ya rakaa za swala za mustahabu ni mara mbili ya idadi ya rakaa za swala za wajibu.

Swala za nafila za usiku huswaliwa rakaa mbili mbili na salaam, na haisihi kuziswali kama swala mbili zenye rakaa nne. Inafaa kuswali swala za nafila kwa kukaa, lakini ni bora zaidi kuziswali kwa kusimama.

Na iwapo mtu yuko safarini nafila ya swala ya adhuhuri, alasiri na isha kwake itasimama. Maelezo zaidi ya swala za nafila yamo katika vitabu vya swala na dua.

Nafila ya swala ya adhuhuri na alasiri zikiswaliwa baada ya kutekeleza swala za adhuhuri na alasiri ndani ya nyakati zake, ihtiyaat wajib ziswaliwe kwa kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu, na wala si kwa niya na kuziswali kwa wakati na wala si qadhaa.

Maswali

1. Swala za wajibu ni zipi?
2. Swala za nafila zina jumla ya rakaa ngapi?
3. Nafila ya swala ya adhuhuri na alasiri huswaliwa kwa nia gani?
4. Swala ya usiku (tahajjud) inaswaliwa vipi?
5. Ni wajibu kuswali swala ya tahajjud katika giza au sehemu ambayo mtu asionekane?
6. Nafila gani haziswaliwi wakati wa safari?

Changamoto

Swala za nafila huswaliwa kwa sauti au kimyakimya?

Vazi la Mwenye Kuswali

Somo la Ishirini na Nane


VAZI LA MWENYE KUSWALI (1)

1. Kiwango cha kujifunika wakati wa swala

- a. Mwanaume anatakiwa kufunika sehemu yake ya siri kutoka kitovuni hadi mapajani hata kama hakuna anayemuona.
- b. Mwanamke anatakiwa kufunika mwili wake wote na nywele zake. Si wajibu kufunika uso kwa kiasi kile cha eneo analopaswa kuliosha katika wudhu, kama ambavyo si wajibu kufunika viganja na nyayo zake.
- c. Kidevu ni sehemu ya uso kwa hiyo si wajibu kwa mwanamke wakati wa kuswali kufunika kidevu, bali ni wajibu juu yake kufunika chini ya kidevu.
- d. Ni wajibu juu ya mwanamke kufunika nyayo ikiwa kuna mtu anayemwona na. siyo maharimu yake
- e. Ikiwa katikati ya swala mwanamke akagundua kuwa nywele zake zinaonekana na kwa haraka akazifunika swala yake itakuwa sahihi ila kama alifanya makusudi.
- f. Kama mtu aligundua baada ya swala kuwa hakuwa na vazi la wajibu wakati wa swala, basi swala yake ni sahihi.

2. Masharti ya vazi la mwenye kuswali

- a. Liwe twahara
Mtu akiswali kwa kukusudia na nguo au mwili ulio na najisi, swala yake ni batili, kama hakujua kuwa ni najisi na akaswali, akaja fahamu baada ya



Mafunzo ya Hukmu za Ibada

swala kumalizika, swala yake itakuwa sahihi lakini kama kwanza alifahamu najisi kisha akasahau na akaswali na najisi swala yake ni batili.

Kama mtu aliswali na najisi katikati ya swala akagundua kama muda bado upo swala yake ni batili, na kama muda ni mchache basi afanye analoweza kuhakikisha anaondoa najisi bila kuharibu mfumo wa swala. Na kama itashindikana basi akate swala na kutwahirisha najisi ile na kisha kuswali tena.

Kama mtu alitwahirisha nguo na kuiswalia kisha akatambua kuwa haikutwahirika swala yake ni sahihi lakini kwa ajili ya swala zinazofuata aitwahirishe tena. Nguo inayotiliwa shaka kuwa ni najisi ina hukmu ya twahara.

b. Lisiwe ghasbi

Kama mtu hakujua au alisahau kama anaswali na nguo ya ghasbi (isiyokuwa halali) swala yake ni sahihi. Vilevile hukmu hii inaingia katika nguo ya haramu ambayo kwa mfano iliwajibikiwa kutolewa khumsi. Ikiwa nguo ilinunuliwa kwa pesa ambazo hazikutolewa khumsi ni haram kuswali na nguo hiyo.

c. Lisitokane na viungo vya mzoga wa mnyama ambaye damu yake huto-ka kwa kuchupa. Kwa ihtiyaat ya wajib, pia swala inabatilika ikiswaliwa na nguo inayotokana na viungo vya mnyama asiyechupa damu.

Ihtiyat wajib swala inabatilika kama mwenye kuswali atakuwa amebeba kitu katika viungo vya mnyama mwenye damu inayochupa. Ama kiungo hicho kama si chenye uhai kama vile nywele, manyoya, sufi, pembe, mfupa na mfano kama huo, na vitu hivyo vikawa vinatokana na mnyama ambaye ni halali kuliwa, basi swala yake haiwezi kubatilika.

d. Lisitokane na mnyama ambaye ni haram kuliwa. Lau sehemu fulani ya viungo vya mnyama huyo itamganda mwenye kuswali, swala yake itabatilika.

Vazi la Mwenye Kuswali

Majimaji yatokayo kwa mnyama najisi yakiingia katika nguo swala inakuwa batili na vile vile swala inabatilika ikiwa nguo iliyoswaliwa ilikuwa na kinyesi cha ndege ambaye ni haram kuliwa.

Maswali

1. Kipi kiwango cha mavazi ya wanawake katika swala?
2. Mwanamke akigundua nywele zake ziko wazi na akazifunika wakati akiswali, Je, anawajibikiwa kuswali tena swala yake?
3. Ni yapi masharti ya nguo za mtu anayeswali?
4. Mtu akigundua kuwa anaswali na nguo yenye najisi au mwili ulionajisika, Je, swala yake itakuwa na hukmu gani?
5. Ikiwa kwa muda kadhaa mtu aliswali na nguo ambayo haikulipiwa khumsi swala yake ina hukmu gani?
6. Kuwepo kwa unyoya wa paka au mate ya paka katika nguo ya kuswalia kunabatilisha swala?

Changamoto

Kuswali na mkanda wa ngozi ambao haujulikani kuwa ni asili au wa kutengeneza kuna hukmu gani?

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Somo la Ishirini na Tisa

VAZI LA MWENYE KUSWALI (2)

Masharti ya nguo za kuswalia

e. Isiwe imeshonwa au kudariziwa na dhahabu (kwa wanaume) lakini kwa wanawake inajuzu katika hali zote. Kwa wanaume ni haramu kuvaa mkufu, pete na saa ya dhahabu, na ni haramu kuswali na vitu hivyo (kwa ihyat wajib).

Uharamu wa dhahabu kwa wanaume si kwa ajili ya mapambo tu bali ni kwa matumizi ya kila aina hata kama ni kwa kuitumia kwa muda tu wakati wa kufunga ndoa.

f. Isiwe ni hariri halisi (kwa wanaume).

3. Wakati gani mtu anaweza kuswali na nguo au mwili wenye najisi

a. Mwili au nguo iliyonajisika kwa damu ya jeraha na ikawa ni vigumu kuondoa damu hiyo. Jeraha ambalo linawezekana kusafishika na hata kutolewa nguo zilizonajisika halihusiani na hukmu hii.

b. Ikiwa damu iliyopo ni ndogo kama ukubwa wa dirham moja (ncha ya kidole) kwa sharti kwamba isiwe ni damu ya hedhi na kwa ihtiyat wajibu (isiwe ni damu ya) nifasi na istihadha. Isiwe damu ya mnyama haramu kama mbwa na nguruwe, mzoga na mnyama haramu kuliwa. Kusiwe na najisi iliyotoka nje ya hapo.

c. Ikiwa nguo iliyonajisika ni ndogo kama soksi, lesa ya mkononi n.k.

d. Ikiwa mtu amelazimika kuswali na nguo au mwili ulio na najisi, kutokana na baridi, au kukosekana maji ya kutwahirishia.

Vazi la Mwenye Kuswali

Maswali

1. Je, Inawezekana mwanamke akatumia dhahabu ikiwa hana nia ya mapambo na akaificha kwa wengine?
2. Je, kuna hukmu gani kwa mwanaume kutumia pete ambayo haina dhahabu?
3. Taja mazingira ambayo mtu anaweza kuswali kwa mwili au nguo iliyo najisi?
4. Je, ni damu gani ambayo ikiwa chini ya ukubwa wa ncha ya kidole inaruhusiwa kuswali nayo?
5. Leso iliyonajisika ikiwa ndani ya mfuko, Je, mtu anaweza kuswali nayo?
6. Ikiwa damu inatoka puani au mdomoni tangu mwanzo wa muda wa swala hadi kukaribia mwisho wa wakati swala, Je, itakuwa na hukmu gani?

Changamoto

Je, inaruhusiwa kuweka chuma cha dhahabu katika meno wakati wa kuyanyoosha?

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Somo la Thelathini

SEHEMU YA KUSWALIA (1)

Masharti ya sehemu ya kuswalia

- a. ghasbi, (yaani imepatikana kwa njia ya kunyang'anya). Lakini kama mtu hajui au amesahau swala yake itakuwa sahihi, hata kuswalia juu ya mswala ambao umenunuliwa kwa pesa ambayo haijatolewa khumsi swala inabatilika.

Kama watu wanashirikiana katika umiliki wa eneo, na mmoja wao hawezi kuswali katika eneo lile bila idhini ya mwenziwe, na ikiwa mahala hapo hapajatenganishwa kuonesha mpaka wa kila mmoja, na vilevile ikiwa kama eneo hilo limenunuliwa kwa pesa ambayo haijatolewa khumsi, ni batili kuswali hapo.

Sehemu ambazo zimetolewa waqfu na kisha serikali ikazichukua kujenga madrasa na shule ikiwa mmiliki yuko radhi swala zitakuwa sahihi. Na mtu ambaye muda wake wa kukaa katika nyumba ya serikali, shirika au kampuni umekwisha, akiendelea kubaki pale bila ridhaa swala zake zitakuwa batili. Serikali dhalimu ikichukua eneo la mtu ikiwa itajulikana kuwa ni ghasbi, haitajuzu kuswali mahala hapo.

- b. Isiwe ni sehemu inayochezacheza (kutikisika).
- c. Isiwe ni sehemu ambayo kusimama mahala hapo ni haramu.
- d. Isiwe mbele ya kaburi la Mtume (s.a.w.w) au Maimamu (a.s)
- e. Sehemu ya kusujudu iwe twahara
- f. Isiwe ni sehemu itakayonajisisha nguo au mwili wa anayeswali
- g. Kuwepo na umbali kiasi baina ya mwanamke na mwanaume, kwa uchache usiwe chini ya shubiri moja.
- h. Iwe tambarare.

Sehemu ya Kuswalia

Maswali

1. Taja masharti ya sehemu ya kuswalia
2. Nini hukmu ya swala ya mtu anayeswali katika eneo la ghasbi lakini juu ya mswala?
3. Nini hukmu ya swala ya mtu anayeswalia mswala ambao umenunuliwa kwa pesa ambazo hazijatolewa khumsini?
4. Nini hukmu ya swala ya mtu anayekaa katika nyumba ambayo muda wake kukaa humo kisheria umekwisha?
5. Nini hukmu ya kuswali katika ardhi ambayo mmiliki wake hayuko radhi kuswalia juu ya ardhi hiyo?
6. Je, inajuzu kukaa, kupita au kuswali katika sehemu ambazo serikali ya kidhalim imezichukua kwa watu (ghasbi)?

Changamoto

Mtu ambaye anasafiri na kula chakula katika hoteli ambayo pembeni yake kuna sehemu ya kuswalia, Je, anaruhusiwa kuswali katika sehemu hiyo bila kupewa idhini.

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Somo la Thelathini na Moja

SEHEMU YA KUSWALIA (2)

- a. Iwe ni sehemu ambayo mtu ataweza kutulia wakati wa kuswali, bila kutikisika, lakini ikiwa kutokana na kutokuwa na muda mtu atalazimika kuswali katika sehemu hizo, mfano ndani ya gari.
- b. Isiwe sehemu ya hatari kwa mwanadamu au juu ya zulia ambalo limeandikwa jina la Allah au kunakshiwa kwa aya za Qur'an.
- c. Isiwe mbele ya kaburi la Mtume (s.a.w.w) au Maimam (a.s) isipokuwa endapo kama inawezekana kuwa katika usawa mmoja.
- d. Sehemu nyingine yaweza kuwa najisi na swala ikawa sahihi lakini sehemu ya kusujudia lazima iwe twahara.
- e. Ikiwa ni sehemu najisi basi isiwe yenye unyevunyevu kuweza kusambaza najisi hiyo kwa wanaoswali imma katika nguo au katika mwili.
- f. Kunaweza kuwa na umbali wa kiasi cha hatua moja, na kama mwanamke atakuwa mbele swala bado ni sahihi.
- g. Sehemu ya kusujudia inatakiwa isivizidi kwa urefu juu au chini viungo vingine vya sijda urefu wa vidole vinne vilivyofungwa.

Ni makruhu kuswali swala ya wajib ndani ya Kaaba na pia kwa ihiyat wajib kutoswali juu ya Kaaba.

Si vibaya kusali juu ya mswala au muh'ri (turba) wenye nakshi. Lakini ikiwa hali hiyo itawapa mwanya watu wanaowatuhmu Mashia au kuleta mgawanyiko wa mawazo, basi ni karaha kutumia katika swala.

Maswali

1. Nini hukmu ya kuswali sehemu ambayo mwili utatikisika bila khiyari

Sehemu ya Kuswalia

- mfano ndani ya gari?
2. Nini hukmu ya swala ambayo nafasi ya kusujudia tu ndio twahara?
 3. Nini hukmu ya kuswali juu ya zulia lililoandikwa jina la Allah au aya za Qur'an?
 4. Je, ni lazima wanaume kusimama kwa mbele zaidi ya wanawake wakati wa swala?
 5. Nini hukmu ya swala ya wajib inayoswaliwa ndani ya Kaaba?
 6. Nini hukmu ya kuswali juu ya turba au mswala wenye nakshi?

Changamoto

Nini hukmu ya kuswali katika eneo ambalo unasikika na kusambaa muziki ambao ni haram?

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Somo la Thelathini na Mbili

HUKMU ZA MSIKITI (1)

Yaliyo haramu:

- a. Kuunajisi msikiti, mahala popote pale na kwa njia yoyote ni haramu. Na ikiwa sehemu yoyote ile ya msikiti imenajisika, basi ni wajibu utwaharishwe haraka hata kama msikiti huo ulibaki kuwa gofu.
- b. Kuupamba na dhahabu ikiwa itatoa sura ya israf, kinyume na hapo inapata hukmu ya makruh.
- c. Kufanya kazi ambazo hazistahili hadhi ya msikiti, mfano kufanya msikiti kuwa ni sehemu ya mafunzo ya michezo au mazoezi ya michezo.
- d. Kuingia kafiri msikitini.
- e. Kubomoa msikiti, isipokuwa kama kuna haja ya dharura na yenye manufaa.
- f. Kufanya kinyume na waqfu wa msikiti, kama kuonyesha picha zisizo na mtazamo wa kidini.

Maswali

1. Taja hukmu zilizokuwa ni haramu kwa msikiti
2. Je, inajuzu kufanya mafunzo ya mazoezi msikitini?
3. Je, inajuzu kurusha nyimbo za furaha kutoka msikitini kama nyimbo za kusifu mazazi ya Mtume (s.a.w.w)?
4. Je, inajuzu kwa kafiri kuingia msikitini?
5. Je, inajuzu kutumia vifaa vya msikiti kama maji na umeme kwa ajili ya majlis au khitma ya mtu?
6. Je, inajuzu kukodisha tabaka la chini la msikiti (ikiwa ni wa ghorofa) ili kufanya kazi zisizohusiana na msikiti?

Changamoto

Nini hukmu ya kuweka picha za Imam Khomeini au picha za mashahidi msikitini ?

Hukmu za Msikiti

Somo la Thelathini na Tatu.

HUKMU ZA MSIKITI (2)

Hukmu mustahab za msikiti ni

- a. Kusafisha msikiti.
- b. Kujiweka manukato na kuvaa nguo safi wakati wa kwenda msikitini.
- c. Kuwa makini na kutokanyaga najisi au uchafu.
- d. Kuwahi kwa kuingia mwanzo msikitini na kutoka mwisho.
- e. Kufanya dhikri na kuweka khofu katika moyo wakati wa kuingia na kutoka msikitini.
- f. Ni makruhu kulala msikitini.
- g. Kuswali msikitini kuna fadhila si kwa wanaume tu bali hata kwa wanawake.

Msikiti wa jamaa ni ule uliotengwa katika mji ili kufanyia ibada za jamaa katika msikiti huo na huitwa **Masjid Jaamia**.

Kutanua msikiti ikiwa ni kutokana na mali ya mtu binafsi hakuna haja ya kutaka idhini ya **Haakim shar'ii** (Hakimu wa sharia za dini).

Inajuzu kuswali katika msikiti uliojengwa na kafiri na pia kuchukua mali kutoka kwa kafiri kwa ajili ya kujenga msikiti.

Madrasa na kumbi zinazoungana na msikiti hazina hukmu za msikiti. Inawezekana kubadilisha jina la msikiti kama jina la mwanzo halikuwa katika *sigha* ya msikiti. (*sigha* ni kisomo maalum kinachosomwa ili kuthibitisha jengo kuwa msikiti)

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Maswali

1. Taja hukmu ambazo ni mustahabu kwa msikiti
2. Nini hukmu ya kulala msikitini?
3. Ni bora mwanamke kuswali msikitini ama nyumbani?
4. Nini maana ya msikiti wa jamia?
5. Je, ni wajibu kupata idhini ya hakim shar'ii katika kuukarabati msikiti?
6. Je, kumbi za starehe zinazojengwa pembezoni mwa msikiti zina hukmu gani?

Changamoto

Nini hukmu ya kufanyia harusi msikitini pamoja na chakula ingawa sherehe zinafanyika nyumbani?

Kibla

Somo la Thelathini na Nne

KIBLA

Hukmu za kibla

Ni wajibu kwa Waislamu kuelekea kibla wakati wa kuswali, kwani huko ndiko iliko Al-Kaba, katika mji wa Makka.

Inajuzu kuswali swala za mustahabu hali ya kuwa unatembea au ukiwa kwenye kipando. Katika hali hii hakuna wajibu wa kuelekea kibla wakati wa kuziswali swala hizo.

Mwislamu anatakiwa kuwa na yakini juu ya muelekeo wa kibla kwa njia yoyote ile, na ikishindikana basi ataswali kuelekea upande ambao anadhani kuwa waweza kuwa kibla. Ikishindikana ataswali kwa kuelekea pande zote nne.

Kibla pia yawezekana kutambulika kwa kuangalia mihrab za msikiti au makaburi ya Waislamu, na ikishindikana basi mtu atatumia kivuli kwa maana kwamba mnamo tarehe ishirini na tano ya mwezi wa tano na tarehe kumi na saba ya mwezi wa saba Miladiya, wakati wa adhuhuri jua hupiga juu kabisa ya Kaaba kwa sura ya kuinama. Kipindi hicho mtu anaweza kuchukua kitu mfano wa mti na kuusimamisha ardhini, upande utakaotoa kivuli ni upande uliyo kinyume na kibla kwa maana upande usio na kivuli utakuwa ndio kibla.

Maswali

1. Nini maana ya kuelekea kibla?
2. Je, kuna ulazima wa kuelekea kibla katika swala za Mustahab?
3. Mtu akishindwa kutambua kibla wajibu wake ni upi?
4. Mtu ataswali kuelekea upande gani ikiwa hata dhana haikumuwezesha kutambua kibla?
5. Ni sahihi kutegemea kiashiria kuhusu kibla?
6. Nini maana ya kutumia kivuli katika kutambua kibla?

Changamoto

Vipi itatambulika kibla kwa upande wa Kusini na Kaskazini na swala itaswaliwa vipi?

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Somo la Thelathini na Tano

SWALA ZA KILA SIKU (1)

1. Swala tano ni moja kati ya nguzo muhimu za dini, na ni ibada yenye nafasi ya kipekee kiasi kwamba kuiacha au kuidharau ni haram na kunapelekea kuadhibiwa kwa mwenye kuiacha. Hakuna sababu yoyote ya kuiacha swala hata kama ni katika vita.

2. Swala za kila siku ziko tano

- a. Swala ya asubuhi, rakaa mbili
- b. Swala adhuhuri rakaa nne
- c. Swala ya alasiri rakaa nne
- d. Swala ya magharibi rakaa tatu
- e. Swala ya isha rakaa nne.

Swala za rakaa nne huswaliwa rakaa mbili katika safari. Tutaeleza baadaye kwa ufasaha.

3. Wakati wa swala

- a. **Asubuhi** ni kuanzia kuchomoza kwa alfajiri ya kweli hadi mwanzo wa kuchomoza kwa jua, na vema mtu akaswali dakika tano au sita baada ya adhana.
- b. **Adhuhuri** ni kuanzia pale jua linapopanda na kuwa la utosi kiasi kwamba kivuli kinaanza kurejea mashariki na unaendelea hadi unapobaki muda makhsusi wa swala ya alasiri ambapo ni dakika chache tu kabla ya kuingia magharibi.
- c. **Swala ya alasiri** inaanza muda mchache tu tangu kuisha kwa swala ya adhuhuri na inaendelea hadi kuingia swala ya magharibi.
- d. **Magharibi** huanzia tangu kuzama kwa mawingu mekundu upande wa mashariki baada ya kuzama jua na huendelea hadi unapobaki muda

Swala za kila Siku

makhsusi wa swala ya isha ambapo ni dakika chache kabla ya nusu ya usiku. Tofauti ya muda kati ya kuzama kwa jua na kuzama kwa mawingu mekundu kunaendana na mabadiliko ya majira ya mwaka.

- e. **Isha** inaanza muda mchache tu tangu kuisha kwa swala ya magharibi na huendelea hadi nusu ya usiku. Nusu ya usiku kisheria ni mtu kuhesabu muda uliopo tangu kuzama kwa jua na adhana ya alfajiri kisha akaugawa mara mbili muda upatikanao ndio nusu ya usiku kisheria.

Maswali

1. Je mtu anayeacha kuswali kwa makusudi au anayedharau swala ana hukmu gani?
2. Elezea muda wa swala ya asubuhi unavyoisha
3. Je, mwisho wa muda wa swala ya alasiri ni hadi kufika adhana ya swala magharibi au kuzama kwa jua?
4. Ni muda gani tangu kuzama kwa jua na adhana ya swala ya magharibi?
5. Ni ipi nusu ya usiku kisheria?
6. Wakati gani swala ya alasiri unaingia?

Changamoto

Shia wana dalili gani juu ya kuunganisha swala (swala ya adhuhuri na alasiri) na (swala ya magharibi na isha).

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Somo la Thelathini na Sita SWALA ZA KILA SIKU (2)

4. Hukmu za wakati wa swala

Mwanadamu atajua wakati wa swala kwa kuwa na yakini juu ya kuingia kwa wakati wa swala, au watu wawili waadilifu waeleze juu ya kuingia kwa wakati wa swala au itoke adhana kwa muadhini anayeaminiwa kujua muda wa swala.

Mtu haruhusiwi kuanza kuswali bila kuwa na uhakika wa kuingia kwa muda wa swala. Kama mtu alikuwa na yakini ya kuingia kwa muda wa swala na baina ya swala akagundua kuwa muda haujaingia swala yake ni batili, isipokuwa tu kama mtu aliswali na baina ya swala akajua muda umeingia sehemu ya mwanzo wa swala yake ni sahihi.

Mtu anaweza kutegemea vyombo vya habari kama vinaaminika kumtangazia muda wa swala na kama muadhini anayeaminika akiadhini si lazima kungoja hadi amalize kuadhini. Na katika suala la nyakati, mukallaf anatakiwa kuangalia mawio na machweo ya eneo alilopo na siyo kutegemea eneo jingine.

Kuwa na wakati mmoja katika maeneo tofauti hakupelekei kuwa sawa katika machweo na mawio wala kuingia kwa adhuhuri.

Mtu hatakiwi kwa makusudi kuacha kuswali hadi kufikia mwisho wa wakati wa swala, na kama ana muda mchache wa kumuwezesha kuswali walau raka moja ikawa ndani ya wakati ataswali kwa nia ya adaa. Na kama ana shaka kwa muda uliobaki ataswali kwa nia ya kutekeleza kili-chomo ndani ya dhimma.

Mtu ana hiyari ya kuswali kwa kutenganisha swala au kuziswali katika wakati mmoja swala ya adhuhuri na alasiri na swala ya maghribi na isha.

Swala za kila Siku

Ni mustahabu kuswali mwanzo wa wakati lakini kama mtu anachelewesha ili kuipata jamaa, au kama anadaiwa na mdai yuko karibu yake ni vema kwanza akalipa deni ikiwa anacho cha kulipa kisha aende kuswali lakini kama muda ni mchache, italazimu aswali kwanza.

5. Taratibu baina ya swala

Swala zinatakiwa ziswaliwe kwa utaratibu. Kwa mfano haiwezekani kuswali swala ya alasiri kabla ya swala ya adhuhuri na wala swala ya Isha kabla ya swala ya magharibi. Na kama kwa makusudi mtu akaondoa utaratibu huu, swala yake inakuwa batili. Ikiwa ni kwa kusahau mtu alifanya hivyo na kugundua baada ya kumaliza kuswali, basi swala yake ni sahihi.

Kama mtu ameweka nia kwa ajili ya swala ya adhuhuri na akiwa kati kati ya swala akagundua kuwa tayari alishaswali adhuhuri anatakiwa kukatisha swala na kuweka nia ya swala ya alasiri na kisha aswali.

Kama mtu alijua ameshaswali adhuhuri na akaweka nia ya swala ya alasiri na kuanza kuswali kisha akagundua kuwa hakuswali swala ya adhuhuri. Kama yuko katika wakati unaoshirikiana mara moja atabadili nia na kuwa ya swala ya adhuhuri, kisha akimaliza ataswali swala ya alasiri. Na ikiwa ulikuwa ni katika wakati makhsusi wa adhuhuri atatakiwa kumaliza swala kwa nia ya adhuhuri kisha ataswali tena swala zote kwa utaratibu.

Maswali

1. Je, ni kwa njia gani muda wa swala utagundulika?
2. Je, muda wa swala huanza kwa kuanza kwa adhana au baada ya adhana?
3. Je, yawezekana kuswali kwa kuzingatia mawio ya sehemu nyingine ambayo haipishani na sehemu uliopo katika nyakati?
4. Je, ni kiasi gani cha swala kikiswaliwa ndani ya muda swala itakuwa ni adaa na kama itakuwa shaka swala itaswaliwa kwa nia gani?

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

5. Nini wajibu wa mtu anayeswali adhuhuri na kisha akagundua kuwa alishaswali adhuhuri?
6. Mtu akiwa anaswali swala ya isha kisha akagundua kuwa hakiswali magharibi ana wajibu gani?

Changamoto

Je, waweza kuamini nyakati za nchi mbalimbali zilizowekwa katika balozi mbalimbali?

Swala za kila Siku

Somo la Thelathini na Saba

SWALA ZA KILA SIKU (3)

6. Adhana na iqama

Ni mustahabu kusoma adhana na iqama kabla ya swala za kila siku za mchana na usiku, na imesisitizwa sana katika swala ya asubuhi na magharibi hasa ikiswaliwa jamaa, ila katika swala kama ya majanga hali-jaelezea jambo hili.

Adhana ina sentensi kumi na nane

Allahu Akbar

(Mara nne)

Ashahadu anlaa ilaaha illa llah

(Mara mbili)

Ash hadu anna Muhammadan Rasuulu llaah

(Mara mbili)

Hayya 'ala Swala

(Mara mbili)

Hayya alal Falaah

(Mara mbili)

Hayya 'alaa khayril amal.

(Mara mbili)

Allaahu Akbar

(Mara mbili)

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Laa ilaaha illa llaah

(Mara mbili)

Iqama iko kama adhana kwa sharti kwamba *Allahu Akbar* ya mwanzo inasomwa mara mbili na *Laa ilaaha illa llaah* ya mwisho inasomwa mara moja, na baada ya kusema *hayya alaa khayril amal* mara mbili husemwa *qad qaamati swalaa mara mbili*.

Ash hadu anna Aliyyan Waliyyu llaah si sehemu ya adhana. Adhana huwa ni alama ya kuashiria kuingia kwa muda wa swala na wasikilizaji wanatakiwa kuitikia kwa sauti.

Si vibaya kutoa adhana kwa pamoja kama haitawaudhi wengine, ila sauti ya Qur'an au dua kuiweka kwa sauti kubwa kuna mushkil ikiwa inawaudhi majirani.

Si vibaya kusoma adhana kwa sauti hasa kwa swala ya alfajiri hata kama majirani wataudhika.

Adhana ya mwanamke inatosheleza kwa mwanaume kama atavisikia vipengele vyake vyote.

Maswali

1. Nini hukmu ya adhana na iqama?
2. Nini tofauti ya adhana na iqama?
3. Je, shahada ya Imam Ali ni wajibu katika adhana?
4. Je, ni sahihi kusimama hata kwa neno hayya ala swalaat?
5. Nini hukmu ya kutoa adhana kwa kikundi?
6. Je, mwanaume anatoshelezwa na adhana ya mwanamke.

Changamoto

Inajuzu kwa swala ya asubuhi ya mwezi wa Ramadhani kutolewa mapema adhana kabla ya muda wa swala ili watu wamalizie kula na kunywa.

Swala za kila Siku

Somo la Thelathini na Nane SWALA ZA KILA SIKU (4)

Wajibu wa Swala (1)

7. Yaliyo wajibu katika swala

1. Nia
2. Takbiratul ihram
3. Qiyam
4. Kisomo
5. Rukuu
6. Sajda
7. Dhikri
8. Tashahud
9. Salaam
10. Tariib
11. Muwalaat

Baadhi ya mambo ya wajibu katika swala ni nguzo, yaani ikiwa hayatafanywa katika swala kwa kupunguzwa au kuongezwa, iwe kwa makusudi au kwa kusahau swala inakuwa batili. Ila wajibu ambazo sio nguzo ikiwa zitaongezwa au kupunguzwa kwa makusudi swala inabatilika na kama ni kwa kusahau swala inabaki kuwa sahihi.

Wajibu ambazo ni nguzo ni hizi zifuatazo:

1. Nia

Ni kukusudia kufanya ibada kwa ajili ya Mwenyei Mungu (swt), na kutekeleza wajibu wake. Si lazima nia kutamkwa kwa ulimi, bali mtu anayeswali anatakiwa kufahamu anaswali swala gani, na haitakiwi kuwa na ria katika swala yaani kufanya kitendo kwa ajili ya kujionesha kwa watu.

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Mtu anawajibikiwa kubadili nia ikiwa:

- a. Wakati anaswali swala ya alasiri atagundua hakuwali swala ya adhuhuri atabadili nia ikiwa si katika wakati makhsusi wa swala ya alasiri, vile vile kati ya swala ya magharibi na swala ya isha.
- b. Ikiwa anawajibikiwa qadhaa ya swala mbili mfano: swala ya adhuhuri na swala ya alasiri na kwa kusahau akatanguliza swala ya alasiri kabla ya swala ya adhuhuri, ni mustahabu kubadili nia.
- c. Mtu anapowajibikiwa na qadhaa ya wajibu na swala ya adaa anaweza kubadili nia na kuanza qadhaa ikiwa muda wa adaa hautapotea.

Ni mustahabu kubadili nia ikiwa:

- a. Kama anaswali swala ya Adaa, atabadili kuwa qadhaa iwapo wakati bora wa swala hiyo ya adaa hautampita.
- b. Kubadili nia ya swala ya wajibu kuwa suna kwa ajili ya kuzidiriki thawabu za swala ya jamaa.
- c. Kubadili nia ya swala ya wajibu na kuwa nafila katika adhuhuri ya mchana wa siku ya Ijumaa kwa yule aliyesahau kusoma Suratul-Jumua na akasoma Sura nyingine na kufikia nusu yake au zaidi yake. Ni mustahabu kwake kubadili nia ya swala ya wajibu kwenda kwenye swala ya nafila ili aanze upya kuswali swala ya wajibu na kusoma Suratul Jumua.

Maswali

1. Taja wajibatu za swala
2. Kuna tofauti gani kati ya wajibatu rukni na ghairi rukni?
3. Taja wajibatu rukni
4. Je, ni lazima kuitamka nia kwa ulimi au kuweka moyoni?
5. Ni wakati gani mtu anaweza kubadili nia katika swala?

Swala za kila Siku

6. Ni wakati gani inakuwa ni mustahabu kubadili nia katika swala?

Changamoto

Mtu amejigundua kuwa anafanya ria katika swala, na mara akaanza kupambana na nafsi yake katika kuiondoa ria Je, mapambano hayo yatahesabika pia kuwa ni ria?

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Somo la Thelathini na Tisa

SWALA ZA KILA SIKU (5)

Wajibu wa Swala (2)

2. Takbiratul Ihram

Makusudio ya kutamkwa mwanzo wa swala ni kuashiria kuanza kwa ibada ya swala, na kutotamkwa kwa sura yoyote ile, iwe kwa makusudi au kwa kusahau pamoja na kuzidisha katika kutamka kunamaanisha kubatilika kwa swala.

Takbira lazima itamkwe kwa kiasi kwamba mtamkaji ajue au asikie kuwa anatamka neno hilo. Takbira ni lazima kutamkwa kwa kiarabu kilicho sahihi kabisa na kutamka kwa makosa au kwa lugha nyingine isiyokuwa kiarabu kunabatilisha swala hiyo.

Lazima mtu ajifunze utamkaji sahihi wa Takbira isipokuwa kama ana udhuru. Mtu anatakiwa awe ametulia wakati wa kutamka Takbira na kama atajitikisa kwa makusudi itabatilika.

Shaka katika takbira

Ikiwa mtu atakuwa na shaka katika Takbira kama aliitamka au hapana, kama alishaanza kisomo, basi asijali shaka hiyo na aendelee na swala yake, na kama alikuwa hajaanza kisomo basi ataitamka tena takbira. Na ikiwa mtu atakuwa na shaka juu ya usahihi wa utamkaji wa Takbira hatatakiwa kushughulishwa na shaka yake.

3. Qiyam (kisimamo) cha wajib

Katika qiyamu kuna visimamo ambavyo ni nguzo na visivyokuwa nguzo. Kisimamo ambacho ni nguzo ni kile kinachosimamwa wakati wa kutamka takbira na wakati wa kwenda katika rukuu, na kisimamo kisichokuwa

Swala za kila Siku

nguzo ni kile kinachosimamwa wakati wa kusoma na baada ya rukuu.

Mtu mwenye uwezo wa kusimama anatakiwa kuswali katika hali ya kusimama hadi kukamilisha swala kama utaratibu ulivyo.

Ni wajibu pia kusimama wakati wa kutamka takbira na kabla ya kwenda katika rukuu ambapo kwa hali zote ni rukni.

Ikiwa mtu baada ya kisomo atakwenda sijda moja kwa moja kwa kusahau rukuu, itamlazimu kurudi na kusimama kidogo kisha kwenda rukuu, na akirukuu bila ya kusimama swala yake itabatilika.

Mtu akiwa katika kisimamo ni wajibu atulie asiegemeo popote ila kwa kusahau au kwa dharura.

Ikiwa mtu amelazimika kutikisika wakati akiwa katika swala itamlazimu aache kusoma dhikri, afanye harakati anazohitaji na kisha atulie na kuen-delea na dhikri.

Yafuatayo ni mustahabu kuyafanya katika kusimama

- a. Kunyooka
- b. Kushusha mabega
- c. Kuweka mikono juu ya mapaja
- d. Kubana vidole
- e. Kuangalia sehemu ya kusujudia
- f. Kuelekeza uzito wa mwili kwenye miguu yote
- g. Kuwa mtulivu na mnyenyekevu
- h. Miguu isipishane.

Mtu asiyeweza kusimama anatakiwa kuswali kwa hali ya kukaa, lakini kama anaweza kuegemea kwenye kitu na kuswali kwa kusimama atataki-wa kufanya hivyo na kuswali hali ya kusimama.

Mtu asiyeweza kuswali kwa kukaa anatakiwa aswali kwa hali ya kulala hasa kwa ubavu wa kulia, na kuelekeza uso kibra, ikishindikana alale kwa ubavu wa kushoto. Akishindwa kabisa alale kwa mgongo na miguu yake

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

kuelekea kibla.

Mtu anayeswali kwa kukaa ikiwa baada ya kusoma akagundua kuwa ana uwezo wa kusimama inamlazimu kusimama na kutekeleza rukuu kwa hali ya kusimama. Hukmu hii vilevile inatumika kwa mtu anayeswali kwa kulala ikiwa ataona ameweza kukaa au kusimama.

Mtu anaweza kuswali kwa kukaa au kulala ikiwa anahofia kuwa kusimama kutampa madhara.

Kama mtu anajua wakati wa mwisho wa wakati wa swala ataweza kuswali kwa kusimama, itamlazimu kusubiri hadi muda huo na kuswali kwa kusimama, kwa ihtiyat wajib. Na kama aliswali mwanzo wa wakati kwa kukaa kutokana na udhuru swala yake itakuwa sahihi hadi mwisho wa wakati udhuru wake unapoendelea.

Kama mtu alikuwa na udhuru na akaswali kwa kukaa, kama udhuru utaondoka kabla ya kumalizika wakati wa swala, italizimu kuiswali tena swala hiyo kwa kusimama.

Maswali

1. Nini hukmu ya swala mbayo takbiratul ihram haikutamkwa kwa usahihi ?
2. Je, ikiwa mtu ana shaka kama alitamka takbira au la nini wajibu wake?
3. Qiyam ya wajibu iko katika sehemu ngapi?
4. Je, mtu anaweza kujitikisa au kusogea mbele na nyuma wakati anaswali?
5. Taja mambo ambayo ni mustahabu katika qiyam
6. Kama mtu hawezi kusimama mwanzo wa wakati wa swala, Je, anaweza kuswali kwa kukaa?

Changamoto

Takbiratul ihram katika swala ya adhuhuri na swala ya alasiri husomwa kimyakimya au kwa sauti?

Swala za kila Siku

Somo la Arobaini

SWALA ZA KILA SIKU (6)

Wajibu wa Swala (3)

4. Kisomo

Katika swala za wajibu za kila siku kisomo kinasomwa kwa namna mbili:

- a. Katika rakaa ya kwanza na ya pili husomwa Suratul Fatiha na kwa ihtiyat wajibu pamoja na Sura nzima, kusoma baadhi ya aya hakutoshelezi kisomo katika swala.
- b. Katika rakaa ya tatu na ya nne husomwa Suratul Fatiha au tasbihat arbaa (*Sub-hana llah, alhamdulillah laa ilaaha illa llah Allaahu Akbar*). mara moja au kwa ihtiyat wajib mara tatu.

Hukmu za kisomo katika rakaa ya kwanza na ya pili

Surat Fiil na Quraish zina hukmu ya Sura moja kwa maana mtu asomapo anatakiwa kuzisoma kwa pamoja, vile vile hukmu hii inatumika katika Surat Dhuhaa na Inshiraah.

Ikiwa mtu alizisoma katika swala Sura hizi bila kuziunganisha swala zake zitakuwa sahihi ikiwa hakufanya uzembe katika kujifunza.

Mtu anaweza kusoma baadhi ya aya za Qur'an baada ya kumaliza Surat Fatiha na Sura nyingine kamili kwa lengo la kuongeza thawabu na si kama ni sehemu ya swala.

Kama mtu anaswali na muda ni mchache wakati au ana hofu ya kuibiwa au kushambuliwa na wanyama wakali, hatalazimika kusoma Sura (atasoma Suratul Fatiha tu na kuendelea na swala).

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Kama mtu ametangulia kusoma Sura kabla ya Fatiha na akagundua hilo kabla hajaenda rukuu itamlazimu asome tena Sura baada ya kumaliza Surat Fatiha na kama aligundua hilo wakati akisoma Sura atalazimika kuacha Sura na kusoma Fatiha na kisha kusoma tena Sura.

Kama mtu alisahau kusoma Suratul Fatiha au Sura au zote pamoja na akaligundua hilo baada ya kuwa katika rukuu, swala yake itakuwa sahihi. Na kama aligundua kabla ya kwenda katika rukuu italazimu asome kile alichokisahau kisha arukuu, na kama alisahau Suratul Fatiha ataisoma na kisha atasoma tena Sura na kurukuu, hukmu hii inatumika hata kwa yule ambaye alishainama katika rukuu ila hajafikia rukuu ya kisheria.

Haijuzu kusoma moja katika Sura zilizo na sijda ya wajib. Ikiwa alisoma na akfika aya ya sijda kwa ihtiyat ya wajib italazimu afanye sijda kwa ajili ya aya hiyo kisha aimalize Sura na kuendelea na swala ambapo baadaye inatakiwa kuswaliwa tena. Ikiwa hakuifikia aya ya sajda, kwa ihtiyat ya wajib ni lazima aiache sura na kusom nyingine, kisha akamilishe swala na airudie tena kuiswali.

Ikiwa mtu yuko katika swala na akasikia imesomwa aya ya sijda ataweza kuendelea na swala lakini afanye ishara kwa ajili ya sijda ya aya ya wajib.

Ikiwa baada ya kusoma Surat Fatiha mtu akaanza kusoma Surat Ikhlas au Kaafirun hataweza kubadili na kusoma Sura nyingine, kama ni swala ya Ijumaa inajuzu kuacha Sura hizi na kusoma Surat Munaafiquna au Surat Jumuat.

Sura nyingine isiyokuwa hizi mbili inawezekana kuacha na kuanza Sura nyingine kabla ya kufika katikati.

Kama mtu amesahau kiasi cha Sura anayoisoma au akahofia kutoikamilisha kutokana na uchache wa muda au udhuru mwingine, inawajibika kuiacha na kusoma Sura nyingine na hakuna tofauti ikiwa alishafika katikati ya Sura au hajafika.

Swala za Kila Siku

Si wajibu kusoma Sura baada ya Suratul Fatiha katika swala za mustahabu hata kama swala hiyo itawajibika kama swala ya nadhiri na mfano wa hiyo. kwa swala za mustahabu zenye utaratibu maalumu kama swala ya wazazi lazima kusoma Sura maalumu iliyopangwa ili kutimiza utekelezaji wa swala hiyo.

Hukmu ya kisomo katika rakaa mbili za mwisho

Inatosha kufanya *tasbihatul arbaa* mara moja katika rakaa mbili za mwisho ingawa kwa ihtiyati ni bora kuirudia kusoma mara tatu. Kama mtu hajui idadi ya tasbihi alizofanya kama ni mara tatu au zaidi au pungufu hawajibikiwi na chochote, lakini inawezekana akazidisha juu ya uchache huo na kisha kuongeza idadi ya tasbihi ikiwa hana yakini juu ya kufanya tasbihi tatu.

Kama mtu alipanga kufanya tasbihi katika rakaa za mwisho na kwa kughafilika akasoma Suratul Fatiha swala yake ni sahihi. Vile vile kwa mtu ambaye alitaka kusoma Suratul Fatiha na badala yake akafanya Tasbih.

Kama mtu alikosea na kusoma Sura baada ya Suratul Fatiha katika rakaa za mwisho na akagundua hilo baada ya kumaliza swala, swala yake ni sahihi na hana hukmu yoyote juu yake.

Mtu anayeswali akitia shaka kuwa amesoma Fatiha au tasbihi au hajasoma chochote atatakiwa kusoma kimojawapo.

Kama mtu ameshaingia katika rukuu akawa na shaka kuwa alisoma Fatiha au Tasbihi katika rakaa hiyo ya tatu au ya nne basi asishughulishwe na shaka yake, na kama shaka hiyo aliitatu kabla ya kufikia kiwango cha rukuu kisheria basi kwa ihtiyat wajib, atasimama na kusoma kisha atarukuu.

Maswali

1. Taja aina za kisomo katika swala za wajibu za kila siku
2. Kama mtu amesoma Suratul Fiil au Inshiraah peke yake katika swala

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

kwa kuwa hajui mas-ala nini hukmu yake?.

3. Nini hukmu ya kusoma Sura zilizo na sajda ya wajibu katika swala ya wajib?
4. Mtu ambaye hajui kuwa tasbihaat arbaa husomwa katika rakaa ya tatu na ya nne mara tatu au zaidi au kwa upungufu ana hukmu gani?
5. Kama mtu alighafilika na katika rakaa ya tatu na ya nne akasoma Suratul Hamdu na Sura Je, atawajibikiwa kurudia swala?
6. Taja hukmu ya kusoma Sura katika swala ya mustahab

Changamoto

Kama mtu alisahau na akasoma tasbihaatul arbaa mara nne, swala yake itakuwa na matatizo?

Swala za kila Siku

Somo la Arobaini na Moja

SWALA ZA KILA SIKU (7)

Wajibatus Swalaat (4)

Kusoma kwa sauti au kimyakimya katika rakaa mbili za mwanzo.

Inapaswa kwa mwanaume kusoma kwa sauti Suratul Fatiha na Sura katika swala ya asubuhi, maghribi na isha. Kwa mwanamke inajuzu kusoma kwa sauti au kimyakimya, na kama kuna mtu asiyekuwa maharimu wake, ambaye ataisikia sauti yake, ni bora akasoma kimyakimya.

Katika swala ya adhuhuri na alasiri ni wajibu kusoma kimyakimya kwa mwanamke na mwanaume isipokuwa katika Bismillaah husomwa kwa sauti.

Suratul Fatiha au tasbihi katika rakaa mbili za mwisho

Inajuzu kusoma kimyakimya kwa mwanamke na mwanaume, ila inajuzu kusoma Bismillaah kwa sauti kama inasomwa katika swala ya furada (sio jamaa) ingawa kwa ihtiyat mustahabu ni kuisoma Bismillaah kimyakimya, na kufanya hivi ni ihtiyat wajibu katika swala ya jamaa.

Ulazima wa kusoma kwa sauti katika swala ya asubuhi, magharibi na isha na kusoma kimyakimya katika swala ya adhuhuri na alasiri hii ni kunahusika na fatiha na Sura tu. Dhikri, sujud, tashahud na salaam na dhikri nyingine za wajibu ni khiyari kwa anayeswali kuzisoma kwa sauti au kimyakimya.

Hakuna tofauti katika usomaji kwa sauti au kimyakimya katika swala za wajibu za adaa (ziswaliwazo katika wakati) au qadhaa (ziswaliwazo nje ya wakati) hata kama itakuwa ni swala ya ihtiyat.

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Hakuna kiwango maalumu cha ukimya wa kusoma ila ni kuhakikisha kwamba sauti haitosikika.

Kama mtu kwa makusudi atasoma kwa sauti sehemu ya kusoma kimyakimya au akasoma kimyakimya sehemu ya kusoma kwa sauti, swala yake itabatilika. Lakini kama alisahau au alikuwa hajui swala yake itakuwa sahihi, na kama atagundua katikati ya kusoma kuwa amesoma kinyume na anavyotakiwa kufanya hatatakiwa kurudia sehemu aliyokwisha isoma.

Ikiwa mtu ataswali kwa sauti ambayo itazidi kiwango cha kawaida swala yake itabatilika.

Wajibu wa kisomo

Ni wajibu katika kusoma kutamka maneno kwa kiasi kwamba itambulike kuwa huu ni usomaji. Kusoma kwa moyo hakutathibitisha usomaji, na haijuzu katika swala. Na alama ya kusoma ni mtu kujisikia mwenyewe ayasemayo, na jinsi ayatamkavyo katika ulimi wake.

Mtu ambaye kwa sababu kadhaa anashindwa kutamka labda ana matatizo ya kuongea (bubu) na akili na hisia zake ni salama anaweza kuswali kwa ishara na swala yake inakubaliwa.

Inatakiwa kusoma kuwe sahihi bila ya makosa. Mtu ambaye hawezi kutamka wala haiwezekani kujifunza kwa usahihi itamlazimu kutamka kwa kiasi awezacho, na kwa ihtiyat mustahabu ni bora akaswali pamoja na imam (akawa maamuma) yaani akaswali swala zake kwa jamaa.

Maana ya kusoma kwa usahihi ni kuchunga kanuni za lugha ya kiarabu, na kuzisoma herufi katika makharij yake. Si wajibu kuchunga hukmu za tajwid katika kusoma.

Kama mtu hajui baadhi ya maneno katika Suratul Fatha au akatamka herufi tofauti na itakiwavyo, au akabadili haraka moja kati ya zilizopo au haku-

Swala za kila Siku (7)

tamka shadda, swala yake itabatilika.

Mwenye kukosea katika kusoma, ikiwa amefanya makusudi au hakujiifunza kutokana na uzembe, swala yake itabatilika, vinginevyo swala yake itakuwa sahihi.

Ikiwa kabla ya kumaliza aya mtu akawa na shaka kama aya hiyo ameiso-ma sahihi au hapana basi asishughulishwe na shaka hiyo, au akawa na shaka juu ya usahihi wa kusoma neno katika aya asishughulishwe na shaka hiyo.

Wakati wa kusoma Sura au Tasbihat, mwili unatakiwa uwe katika hali ya utulivu, na ikilazimu mtu kusogea mbele au nyuma itatakiwa wakati wa kusogea aache kusoma.

Adabu za qiraa (usomaji)

a. Adabu za mustahabu katika kusoma ni :

- ◀ Kusoma *a'udhu billah* kabla ya kusoma Sura katika rakaa ya kwanza.
- ◀ Kusoma *bismillaah* kwa sauti katika rakaa ya kwanza na ya pili ya swala ya adhuhuri na alasiri.
- ◀ Kusimama kila mwisho wa aya na siyo kuunganisha na aya inayofuata.
- ◀ Kuzingatia maana ya yanayosomwa.
- ◀ Kusema *alhamdu lillah* baada ya kusoma Suratul-Fatiha katika swala ya jamaa au isiyokuwa ya jamaa.
- ◀ Kusema "*kadhaalika llahu rabbi*" baada ya kusoma Sura Ikhlas.
- ◀ Kupumzika kidogo baada ya kusoma Alhamdu na baada ya Sura.

b. Mambo ambayo ni makruhu katika kusoma

- ◀ Kutosoma Sura Ikhlas hata mara moja katika swala za siku nzima.
- ◀ Kurudia Sura moja katika rakaa mbili tofauti katika swala moja.

Maswali

1. Je, wanawake wanaweza kusoma Sura kwa sauti katika swala ya subhi,

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

magharibi na Isha?

2. Swala ya qadhaa ya asubuhi inaswaliwa kwa sauti au kimyakimya?
3. Nini hukmu ya swala ambazo kisomo chake hakikuwa kwa sauti?
4. Mtu aliyeswali kulingana na jinsi alivyofundishwa na wazazi au madrasa kisha baadaye akagundua kuwa alifundishwa kimakosa, nini hukmu yake kwa swala hizo?
5. Kisomo kinaswihi kwa hali gani?
6. Taja adabu za mustahabu katika kisomo

Changamoto

Je, ni wajibu kusema Bismillah kwa nia ya Sura maalum (yaani kabla ya kusoma unaweka nia ya Sura utakayo kusoma na kisha ndio unasoma Bismillah)

Swala za kila Siku

Somo la Arobaini na Mbili

SWALA ZA KILA SIKU (8)

Wajibu wa Swala (5)

5. Rukuu

a. Maana yake

Katika kila rakaa ni wajibu kufanya rukuu baada ya kisomo. Na maana ya rukuu ni kuinama kiasi cha kuweza kuweka mikono katika magoti. Baada ya kufika katika rukuu na kutulia haiwezekani kwa mtu kuinua kichwa na kisha kuinama tena kwa ajili ya rukuu kufanya hivyo kutabatilisha swala yake. (Rukuu ni guzo na kwa kuizidisha swala inabatilika).

b. Wajibu wake

Kuinama hadi mikono kugusa magoti. Katika kila rakaa baada ya kisomo ni wajibu kuinama kiasi cha kuweza kuweka mikono katika magoti, na haitoshi kuweka ncha tu za vidole. Kwa ihtiyat wajibu ni kuweka mikono magotini wakati mtu akiwa katika hali ya rukuu, kuinama huko ni lazima kuwe na nia ya rukuu na si kwa ajili ya jambo jengine. Akiinama kwa ajili ya kuchukua kitu au kuuwa mnyama hakuwezi kuhesabiwa kuwa ni rukui.

Mtu anayeswali kwa kukaa inatosheleza kuinamisha sura yake kukabiliana na magoti kwa nia ya rukuu.

Kusoma dhikri

Dhikri iliyo wajibu katika rukuu ni kusema "*Subhaana Rabbiyal Adhiimi wa Bihamdihi*" mara moja au "*Subhaana Ilaah*" mara tatu. Katika rukuu inajuzu kusoma dhikri nyingine zisizo kuwa hizi kama vile kusema "*Alhamdulillah au Allahu Akbar*"

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Kutuliza mwili wakati wa kusoma dhikri

Wakati wa kusoma dhikri mwili unatakiwa kuwa katika hali ya utulivu hata kama inasomwa dhikri ya mustahabu. Na kama mtu alitikisika ghafla na kupoteza utulivu inatakiwa baada ya kurejea katika utulivu arudie kusoma dhikri.

Mtu anayejua kuwa utulivu ni wajibu wakati wa kusoma dhikri, kama kabla ya kufikia katika rukuu ataanza kusoma dhikri kwa makusudi, swala yake ni batili. Na kama alisahau inabidi baada ya kufika katika rukuu atulie na arudie tena kusoma dhikri. Na kama kabla ya kumaliza kusoma dhikri ya rukuu aliinua kichwa chake kwa makusudi swala yake itabatilika. Na kama alisahau na akagundua kabla ya kutoka kabisa katika rukuu atarudi na kumalizia dhikri na kama alishatoka kabisa swala yake ni sahihi.

Mtu asiyeweza kusoma sentensi "*Subhaanallah*" mara tatu katika rukuu kwa sababu ya maradhi na kadhalika, itatosha kuisoma mara moja, na hata kama ataweza kurukuu mara moja tu basi ni ihtiyaat wajib aanze kusoma hiyo dhikri katika muda huo na aimalizie wakati wa kuinua kichwa chake kutoka kwenye rukuu.

Kusimama na kutulia baada ya rukuu

Baada ya rukuu mtu anatakiwa kusimama na baada ya kuwa ametulia aende sijda. Kama atafanya makusudi kutosimama au kutotulia baada ya kusimama swala itabatilika.

c. Mtu aliyesahau rukuu na kisha akakumbuka

Kama atakumbuka kabla ya kusujudu sijda ya kwanza, atasimama kisha atarukuu. Kusimama hali ya kuwa amejipinda au ameinama kutabatilisha swala yake. Ikiwa atakumbuka hali ya kuwa ameingia katika Sijda ya pili, swala yake itabatilika, kwa kuwa tayari atakuwa ameacha nguzo na ameingia katika nguzo nyingine.

Swala za kila Siku

Kabla ya kuanza Sijda ya pili (yaani akiwa katika sijda ya kwanza au kabla hajaleta sijda ya pili) atatakiwa kusimama na kuleta rukuu kisha atasujudu na baada ya swala kwa ihtiyat atatakiwa kuleta sijda ya kusahau.

d. Mustahab katika rukuu

- ▼ Kutoa Takbira katika hali ya kusimama kabla ya kwenda rukuu
- ▼ Kwa mwanaume kurudisha magoti nyuma yake.
- ▼ Kichwa kuwa sawa na mgongo asikitikise.
- ▼ Kuweka viganja katika magoti.
- ▼ Atazame katikati ya miguu yake.
- ▼ Kusema "*samiyallahu liman hamida*" baada ya kunyanyuka kutoka rukuu.
- ▼ Kuweka viganja juu kidogo ya magoti kwa mwanamke
- ▼ Kumswalia Mtume na watu wa nyumba yake kabla ya kurukuu au baada yake.

Maswali

1. Taja wajibu katika rukuu
2. Je, ni wajibu kuweka mikono juu ya magoti?
3. Mtu anayeswali kwa kukaa atainama kiasi gani kutimiza rukuu?
4. Nini hukmu ya mtu aliye katika rukuu na akatikisika bila khiyari?
5. Nini wajibu wa mtu aliyesahau rukuu na akakumbuka kabla ya kuingia sijda ya pili?
6. Taja mustahab katika rukuu.

Changamoto

Kutikisika kidogo kunaondoa utulivu wa swala?

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Somo la Arobaini na Tatu

SWALA ZA KILA SIKU (9)

Wajibu wa Swala (6)

6. Sajda

a. Maana yake

Katika kila rakaa baada ya rukuu inatakiwa kufanya sijda mbili. Na maana ya kusujudu ni kuweka paji la uso katika ardhi. Sijda mbili kwa pamoja ndiyo nguzo kwa maana kwamba kuzidisha au kupunguza kunabatilisha swala.

Kama mtu alisahau na kuzidisha sijda moja au kupunguza swala haiwi batili lakini kuna hukmu zake za kuzizingatia kama tutakavyozieleza hapo baadaye.

b. Wajibu wake

Kugusisha viungo saba katika ardhi:

Wakati wa sijda ni wajibu viungo saba viguse katika ardhi navyo ni paji la uso, viganja viwili, magoti na ncha mbili za vidole vikubwa vya miguu.

Hakuna ubaya kwa vidole vingine pia kugusa chini wakati wa kusujudu, ikiwa paji la uso halitagusa chini sajda haitakuwa sahihi hata kama viungo vingine viligusa chini. Lakini ikiwa paji la uso litagusa chini sajda itakuwa sahihi hata kama mtu alisahau kugusisha viungo vingine au kusoma dhikri.

Mtu asiyeweza kusujudu anatakiwa kuweka kitu kirefu na kuweka turba juu yake na kusujudu au kuiinua na mkono na kuiweka katika paji la uso. Haijuzu kuinua moja kati ya viungo saba wakati wa kusoma dhikri, lakini kama si katika kusoma dhikri inawezekana kuinua sehemu zingine na kure-

Swala za kila Siku

jesha isipokuwa paji la uso. Mtu akiinua paji la uso kwa kusahau kabla ya kumaliza dhikri hataweza kurejesha tena na itahesabika kuwa ni sijda moja.

Hakuna ubaya wakati wa kusujudu kuweka mikono miwili kwenye msala wenye matundu madogo madogo.

Mtu asiyeweza kusujudu juu ya turba na mfano wake hata kwa kuiinua analazimika kusujudu kwa kuashiria kwa kichwa na iwapo hatoweza ataashiria kwa macho yake.

Mtu mwenye hali maalum ya kiafya, kwa kiasi cha kutoweza kuweka viungo saba wakati wa sijda, na anatomia kiti chenye kutikisika, akiweza kuweka turba na mfano wake kwenye mkono wa kiti au juu ya kitu kingine kama meza na mfano wake na kusujudu basi atawajibika kusujudu kwa njia hii na swala yake itakuwa sahihi. Na kama hatoweza basi atasujudu kwa namna yoyote inayowezekana hata kama ni kwa kuashiria kwa kichwa au macho wakati wa sijda na rukuu na swala yake itakuwa sahihi.

Iwapo ataswali kwenye ardhi yenye udongo, ikiwa kuchafuka mwili wake au mavazi yake kutakuwa na tabu sana au madhara makubwa anaruhusiwa kuswali akiwa amesimama na kuashiria kwa kichwa wakati wa sijda na rukuu, na atatoa tashahhud na salaam akiwa amesimama.

Kusoma dhikri

Dhikri ya wajibu katika sijda ni kusema "*Subhaana rabbial aa'laa wabihamdihi*" mara moja au kusema "*Subhaana llaah*" mara tatu. Inawezekana pia kusema dhikri yoyote ile badala ya hiyo; kama kusema "*Alhamdulillah*" au "*Allahu akbar*."

Kutulia wakati wa kusoma dhikri za sijda mbili:

Mtu anatakiwa kuwa na utulivu wakati wa kutamka dhikri hata zikiwa za

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

mustahabu.

Mtu anatakiwa kujua kuwa utulivu ni wajibu wakati wa kusoma dhikri katika sijda. Kama kabla ya kufikisha kichwa katika ardhi na kutulia akaanza kusoma dhikri kwa makusudi swala yake ni batili.

Na kama alisahau inabidi baada ya kufika katika sijda atulie na arudie tena kusoma dhikri. Kama alikumbuka wakati ameshatoka katika sijda swala yake itakuwa sahihi. Kama kabla ya kumaliza kusoma dhikri ya sujud akainua kichwa chake kwa makusudi swala yake itabatilika. Na kama alisahau swala yake ni sahihi.

Iwapo atasujudu juu ya godoro na mfano wa vitu ambavyo mwili wake hauwezi kutulia katika hatua ya mwanzo, iwapo mwili wake utatulia baadaye hakuna tatizo katika sijda yake.

Iwapo kabla ya kumaliza dhikri ya sijda atainua paji lake la uso kwa kusahau basi hatoweza kulirejesha tena ardhini, bali kufanya hivyo itahesabiwa kuwa ni sijda nyingine. Lakini iwapo atainua viungo vingine kwa kusahau analazimika kuviweka tena ardhini na kuleta dhikri.

Iwapo paji la uso litagongana na ardhi wakati wa kusujudu na likainuka kwa lazima basi analazimika kulirejesha tena ardhini na kusoma dhikri na itahesabiwa kuwa ni sijda moja.

Kuweka paji la uso sehemu iliyo twahara

Paji la uso linatakiwa kuwa juu ya kitu kilicho twahara, lakini iwapo ataweka turba au kitu kingine kwenye sehemu iliyonajisika kama vile busati na mfano wake au sehemu mojawapo ina najisi na akaweka paji lake kwenye eneo twahara basi sijda yake haina tatizo.

Kutokuwa na kitu baina ya paji la uso na panapotumika kusujudu

Haijuzu kuwa na kitu mfano nywele, nguo, kofia baina ya paji la uso na

Swala za kila Siku

sehemu inayokuwa wajibu kufanyia sijda juu yake.

Iwapo mwenye kusali akiwa katika sijda atagundua kuwa paji lake la uso halifiki kwenye turba kutokana na kuwepo kwa kizuizi kama vile kilemba au kitambaa au kitu kingine, anatakiwa kulitikisa paji lake mpaka lifike kwenye turba bila kukinyanyua kichwa chake. Iwapo atainua kichwa chake kwa kutojua au kwa kusahau na ikawa kitendo kimefanyika kwenye sijda mojawapo ya sijda mbili za rakaa moja, basi swala yake itakuwa sahihi na wala hatolazimika kuirudia. Ama kama akifanya hivyo kwa kujua na kwa makusudi au kitendo hicho kilikuwa katika sijda zote mbili za rakaa moja swala yake itakuwa batili na atalazimika kuirudia.

Kuweka paji la uso katika kitu ambacho ni wajibu kusujudu juu yake

Ni lazima iwe juu ya kitu ambacho ni sahihi kusujudu juu yake, kama vile udongo na kila kitu kinachomea toka ardhini kisichofaa kuliwa wala kuvaliwa.

Kuinuka na kutulia baina ya sijda mbili

Baada ya sijda ya kwanza anatakiwa kukaa. Na baada ya kutulia ataenda katika sijda ya pili.

Paji la uso linatakiwa kuwa sawa na sehemu nyingine zinazogusa ardhi wakati wa kusujudu na tofauti isizidi urefu wa vidole vinne vilivyofungwa. Ni ihtiyat ya wajib baada ya kumaliza rakaa ya kwanza na ya tatu kabla ya kusimama kwa rakaa nyingine mtu akae kidogo ili kupata utulivu, kisha ataendelea na rakaa inayofuata.

Maswali

1. Nini hukmu ya kuzidisha au kupunguza sijda moja katika swala?
2. Je, inajuzu kugusisha vidole vingine vya mguu chini wakati wa kusujudu?

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

3. Nini wajibu wa mtu asiyeweza kuweka paji la uso chini?
4. Je, inajuzu kusujudu juu ya turba (udongo) iliyo na mafuta mafuta?
5. Je, ni wajibu kukaa katika rakaa ya kwanza baada ya sijda ya pili?
6. Taja viungo saba ambavyo vinatakiwa kugusa chini wakati wa kusujudu.

Changamoto

Turba za siku hizi zinatengenezwa kiasi cha kuweza kuonyesha idadi ya rakaa wakati wa kusujudu hudidimia chini. Nini hukmu ya sijda juu ya turba ya aina hiyo?

Swala za kila Siku

Somo la Arobaini na Nne

SWALA ZA KILA SIKU (10)

Wajibu wa Swala (7)

Vitu vilivyo wajibu kusujudu juu yake

Ni wajibu kusujudu juu ya ardhi au juu ya kitu kinachomea katika ardhi, kwa sharti kwamba:

- ▼ Si chenye kuliwa kama ngano.
- ▼ Si chenye kuvaliwa kama pamba.
- ▼ Si madini kama bati.

Inajuzu kusujudu juu ya:

- ▼ Mawe ya kupambia kama marumaruru.
- ▼ Majani ambayo yanaliwa na wanyama pekee kama nyasi.
- ▼ Majani ambayo yanatumika kama dawa na hayatumiki kwa chakula.
- ▼ Chokaa na saruji.
- ▼ Karatasi zilizotengenezwa kwa mbao au majani yasiyokuwa katani wala pamba.

Inaruhusiwa kusujudu juu ya mauwa yasiyoliwa na dawa za mimea zitokanazo na ardhi na ambazo hutumika kutibu wagonjwa tu, kama vile uwa la mmea wa banafsanji na mmea wa khatmi. Amma mimea inayotumiwa katika matumizi yasiyokuwa ya kimatibabu kutokana na kuwa na sifa za kutibu kiasi kwamba huliwa pia, kama vile mmea wa khaksher (mmea wa asili wenye mbegu nyekundu zinazoshabihiana na Khashkhash) hairuhusiwi kusujudu juu yake.

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Kama mtu hana kitu cha kufanyia sijda anaweza kusujudu juu ya nguo iliyotokana na pamba au katani na kama hana nguo ya aina hiyo inajuzu asujudu nyuma ya kiganja.

Iwapo atakosa kitu kinachofaa kusujudu juu yake katikati ya swala na hana kitu kinachofaa kusujudu juu yake, ikiwa muda unatosha atakatisha swala. Ama kama muda hautoshi atatumia utaratibu uliotajwa katika mas'ala yaliyotangulia.

Iwapo atakuwa katika mazingira yanayomlazimu kufanya taqiyyah anaruhusiwa kusujudu juu ya zulia na mfano wake, na wala halazimiki kuswali sehemu nyingine. Lakini hapo alipo kama ataweza kusujudu juu ya kitu kinachofaa kusujudu juu yake, kama vile mkeka, jiwe na mfano wake basi atatakiwa kufanya hivyo, na iwapo hatoweza basi atasujudu juu ya zulia kwa taqiyyah.

Iwapo katika sijda ya kwanza turba ikaganda juu ya paji lake la uso anatakiwa kuitoa kwa ajili ya sijda ya pili, na iwapo hatoitoe na akasujudu mara ya pili basi usahihi wa swala yake utakuwa na matatizo.

kitu bora kinachofaa kusujudu juu yake ni udongo na ardhi ambayo ni alama ya unyenyekevu na utii kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu na udongo bora ni turba ya udongo wa Bwana wa Mashahidi (a.s).

Mustahab katika sajda:

- ▼ Kutoa Takbira kabla ya kusujudu
- ▼ Kusema "*Astaghfirullaaha rabbii wa atuubu ilayh*" baina ya sijda mbili
- ▼ Kurefusha sijda na kuomba dua na kumswalia Mtume s.a.w.w.
- ▼ Baada ya sijda kukalia paja la mguu wa kushoto, na sehemu ya juu ya unyayo wa kulia kuwa juu ya unyayo wa kushoto.
- ▼ Ni makruhu kusoma Qur' an katika hali ya sijda, pia ni haramu kumsujudia asiyekuwa Allah (s.w.t).

Swala za kila Siku

Mambo mawili yanayohusiana na kusujudu:

1. Ni haramu kumsujudia asiyekuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Na yale yanayofanywa na baadhi ya watu kama vile kuweka paji la uso kwenye nguzo ya mlango wa kaburi la Maimamu (a.s.), iwapo itakuwa imekusudiwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu hakutakuwa na tatizo, la sivyo ni haramu.

2. Aya za sijda ya wajibu

- a. Aya ya kumi na tano ya Sura ya thelathini na mbili (Sajda).
- b. Aya ya thelethini na saba ya Sura ya arobaini na moja (Fuswilat).
- c. Aya ya sitini na mbili ya Sura ya hamsini na tatu (Najm).
- d. Aya ya kumi na tisa ya Sura ya tisini na sita (Alaq).

Hizi ni aya ambazo msomaji na msikilizaji wanawajibikiwa kuleta sijda mara wasomapo au wasikiyapo hata kama inasomwa katika redio, televisheni au compyuta. Wanaweza kusujudu hata kabla ya kuisha kusomwa kwa aya hiyo.

Endapo atasahau basi atatakiwa kuitekeleza sijda hiyo wakati wowote akikumbuka. Sajda hii inatakiwa kufanyika juu ya kitu kinachofaa kusujudu juu yake wakati wa swala, lakini masharti mengine kama kuelekea kibla na kuwa na wudhu hayana nafasi kubwa katika sijda za Qur' an.

Hakuna dhikri ya wajibu inayopaswa kusomwa wakati wa kufanya sajda ya Qur' an ila ni bora ikasomwa dhikri ifuatayo:

"Laa ilaaha illa llahu haqqan haqqan, laa ilaaha illa llaahu iimaan wa taswidiqan, laa ilaaha illa llaahu ubuudiyatan wa riqqan, sajadtu laka yaa rabbi taabbudan wa riqqan, laa mustankifan wala mustakbiran, bal anaa abdun dhaliilun dhaiifun khaaifun mustajirun"

Maswali

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Maswali

1. Taja vitu ambavyo ni wajibu kusujudu juu yake
2. Nini hukmu ya kusujudu juu ya karatasi?
3. Nini wajibu wa mtu alipoteza kitu sahihi cha kusujudu juu yake akiwa kati kati ya swala?
4. Ni yapi masharti ya vitu vya wajibu kusujudu juu yake?
5. Je, ni sahihi kusujudu katika milango ya haram takatifu?
6. Nini hukmu ya kusoma au kusikia aya ya sijda ya wajibu ya Qur' an?

Changamoto

Nini hukmu ya kusujudu juu ya zulia?

Swala za kila Siku

Somo la Arobaini na Tano

SWALA ZA KILA SIKU (11)

Wajibu wa Swala (8)

7. Dhikri

a. Maana yake, ni mkusanyiko wa ibara za kumtaja Allah (s.w.t) kama vile *Subhaana llaah, Allaahu Akbar, na Alhamdulillah*.

Na miongoni mwa dhikri zilizo bora ni kumswalia Mtume na watu wa nyumba yake.

b. Mambo ya wajibu katika dhikri

-Lazima dhikri isomwe kwa kutamka kwa ulimi kiasi kwamba msomaji atambue kuwa anasoma.

-Isomwe kwa kiarabu sahihi.

-Isomwe katika hali ya utulivu wa mwili.

Haijuzu kubadili dhikri ya rukuu na sujud kwa makusudi. ikiwa alibadilisha kwa makosa au kusahau, akikumbuka akiwa bdo yuko kwenye sijda atasahihisha, ikiwa ni baada ya sijda basi swala yake ni sahihi.

Ni mustahabu kusoma Takbira kabla na baada ya ya rukuu na sijda, kuso ma dhikri ya "*Bihaulillaahi wa Quwwatihii Aquumu wa Aq'ud*" katika hali ya kusimama kwa ajili ya rakaa nyingine.

Nii bora kuikariri dhikri ya wajibu katika rukuu na sijda bora zaidi ni kuihitimisha kwa witiri. Vile vile ni mustahab katika sijda, pamoja na yaliyo otajwa, kumsalia Mtume (s.a.w) na Ahli zake (a.s) na kuomba kutekeleze wa mahitaji mbalimbali ya dunia na Akhera.

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

8. Tashahud

a. Maana na hukmu yake.

Katika rakaa ya pili ya kila swala na rakaa ya tatu ya swala ya magharibi na rakaa ya nne ya swala ya adhuhuri, alasiri, na isha mtu anatakiwa baada ya sijda ya pili kukaa, na baada ya kutulia atatamka maneno ambayo ndio yanaitwa Tashahud.

b. Dhikri ya tashahud

Dhikri ya wajibu katika tashahudi ni kusema:

"Ash-hadu anlaa ilaaha illa llaahu wahdahuu laa shariika lahu, wa ash-hadu anna Muhammadan abduhu wa rasuuluhu, Allaahumma swalli ala Muhammadin wa aali Muhammadin"

Ni mustahabu kabla ya dhikri ya Tashahud kusema:

"Bismillaah wa Billaahi wal Hamdu lillaah wa Khayrul Asmaail Husnaa Lillaah"

Ni mustahabu kusimama kwenye neno "Muhammad" (s.a.w.w) katika sentensi ya "Allahumma swalli alaa Muhammad wa Aali Muhammad" na kisha kuendelea na sentensi ya "Waali Muhammad" ikiwa haitokuwa na madhara kwa muungano wa sentensi hakuna tatizo. Na pia baada ya kumaliza kumswalia Mtume ni mustahabu kusema:

"Wataqabbal Shafaa'atahu Fii Ummatihi War-Fa'a Darajatahu".

Mtu aliyesahau tashahud

Mtu akisimama kwa ajili ya rakaa ya tatu na kabla ya rukuu akakumbuka kuwa hakufanya tashahud atatakiwa kukaa na kufanya tashahud, na kisha kuendelea na swala. Baada ya swala ataleta sijda mbili za kusahau kwa sababu ya kusimama mahala pasipotakiwa.

Swala za kila Siku

Kama mtu baada ya rukuu ya rakaa ya tatu atagundua kuwa hakufanya Tashahud atamaliza swala na baada ya salaam ataleta sajda mbili za kusahau kwa sababu ya tashahud iliyosahaulika na kwa ihtiyat wajibu ataleta qadhaa ya tashahud iliyosahaulika.

9. Salaam:

a. Lengo la salaam na hukmu yake

Kitendo cha mwisho cha swala ambacho kwa kukitekeleza humaanisha kuwa imefika mwisho, kinaitwa Salaam. Na Salaam ya wajibu ni kutamka: "*Assalaamu Alaykum*"

Na ni bora kuongezea kwa kusema:

"Warahmatullahi wa Barakaatuh"

au kusema: *"Assalaamu 'Alaynaa wa 'Alaa 'Ibaadillaahi Swaalihiina"*.

Ni mustahabu kabla ya kutoa salaam hizo kusema:

"Assalaamu Alayka Ayyuha Nnabiyyu Warahmatulaahi Wabarakaatuh"

b. Mtu aliyesahau kutoa Salaam.

Mtu akisahau kutoa salaam na akakumbuka wakati ambao hajafanya jambo ambalo kwa makusudi au kusahau linabatilisha swala kama kugeuka upande usiokuwa kibla, basi mtu huyo atatakiwa kutoa salaam na swala yake itakuwa sahihi.

Maswali

1. Nini maana ya dhikri?
2. Je, inajuzu kubadili dhikri za rukuu na sujud?
3. Je, swalawat (kumswalia Mtume) ni moja ya dhikri?
4. Je, inawezekana kusoma "*bihaulillaah...*" hali ya kuwa mtu anafanya harakati?

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

5. Nini wajibu wa mtu aliyesahau salaam ya mwisho wa swala?
6. Ni ipi tashahud ya wajibu?

Changamoto

Je, inajuzu kutamka shahada ya "*Aliyyu waliyyu llaah*" katika tashahud?

Swala za kila Siku

Somo la Arobaini na Sita

SWALA ZA KILA SIKU (12)

Wajibu wa Swala (9)

10. Tartib.

a. Maana na hukmu yake

Ni jambo la wajibu kwa mwenye kuswali kufuata mpangilio uliowekwa katika swala, na kila kitendo cha swala lazima kifanywe kwa mujibu wa mahala pake.

Ikiwa mtu atabadili utaratibu huu kwa makusudi swala yake itabatilika. Mfano kusoma Sura kabla ya Sura Fatiha au kusujudu kabla ya kurukuu.

b. Kuacha taratibu kwa kusahau

Ikiwa mtu atavunja utaratibu kwa kusahau mfano: Kutanguliza rukni (nguzo) kabla ya rukni nyingine; kama kusahau kusujudu wakati ameshaingia katika rukuu ya raka nyingine swala yake itabatilika.

Kutanguliza isiyokuwa rukni badala ya rukni; kwa mfano akisoma tashahud akagundua kuwa hakufanya sijda mbili atatakiwa kufanya sijda mbili kisha aendelee na swala.

Kutanguliza rukni badala ya isiyokuwa rukni; mfano mtu akisahau kusoma Sura Fatiha na kuingia katika rukuu na akagundua baada ya kufikia rukuu swala yake itakuwa sahihi.

Kutanguliza isiyokuwa rukni juu ya isiyokuwa rukni; mfano mtu akisahau kusoma Sura Fatiha na akasoma Sura na akagundua kabla ya kurukuu; kwa

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

hali hii atatakiwa kusoma Fatiha na na sura na aendelee na utaratibu wa swala.

11. Muwaalaat

Mtu anayeswali lazima ahakikishe anafuatanisha vitendo vya swala, kwa maana kusiwe na mwanya mrefu kati ya kitendo na kitendo.

Kunut

Katika kila swala iwe swala ya wajibu au ya mustahabu, ni mustahabu (sunnah) baada ya kusoma Sura na kabla ya rukuu ya rakaa ya pili, ainuwe mikono na kusoma dua ambapo kitendo hicho huitwa kunut. Katika swala ya Ijumaa kunut hufanyika katika rakaa ya kwanza kabla ya rukuu na katika rakaa ya pili baada ya rukuu.

Kunut katika swala za Idi zote huwa ni mara tano katika rakaa ya kwanza na mara nne katika rakaa ya pili. Katika kunut husomwa dua yoyote kutoka kwa Maasumiin (a.s) au hata aya ya Qur'an, ila ni bora kusoma dua zilizo katika Qur'ani kama kusema: "*Rabbanaa Aatinaa Fid Duniyaa Hasanatan Wafil Aakhirati Hasanatan Waqinaa 'Adhaaban-Naari*. Au kutoka mwa maimau maasumu (as); kama: *Laa Ilaaha Illa Llaahul Haliimul Kariimu, Laa Ilaaha Illa Llaahul-A'liyul 'Adhiimu, Subhaanallaahi Rabbis-Samaawaatis-Sab'i Wa Rabbil Ardhiinas-Sab'i, Wamaa Fii Hinna Wamaa Bainahunna Wa Rabbil 'Arshil Adhiim, Wal Hamdu Lillaahi Rabbil Aalamiin*".

Ta'aaqib, (dua baada ya swala).

Taaqib katika swala si lazima kufanyika kwa kiarabu ingawa ni bora kama zitatumika dua zilizopatikana kutoka kwa Maasumin (a.s) na kunakiliwa katika vitabu mbalimbali vya dua.

Na taaqib iliyo bora ni taaqib maarufu kama tasbeeh Zahra (a.s), ambayo ni: *Allah Akbar x34, Alhamdulillah x33 na Subhanallah x33*.



Swala za kila Siku

Katika vitabu vya dua zimenukuliwa taaqibaat zenye maudhui za hali ya juu na ibara nzuri kutoka kwa Maimamu (a.s).

Ni mustahabu baada ya swala kuleta sijdatus-shukru, yaani sijda ya Kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa neema zake zote ikiwemo neema yake ya kukupa taufiq ya kusali. Nayo ni kuweka paji la uso wako juu ya ardhi. Na ni bora kusema mara 3 au zaidi *Shukran Lillaah*

Maswali

1. Nini hukmu ya mtu aliyesahau na kutanguliza rukni kabla ya rukni nyingine?
2. Nini tofauti ya tartiib na muwalat katika swala?
3. Nini hukmu ya kuacha muwalat katika swala?
4. Swala za Idi zina kunut ngapi?
5. Je, yawezekana kusoma **swalawat** ndani ya kunut?
6. Nini hukmu ya mtu kutanguliza kwa kusahau ghairi rukni badala ya ghairi rukni?

Changamoto

Je, inajuzu kusoma dua katika kunut kwa lugha isiyokuwa kiarabu?

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Somo la Arobaini na Saba

SWALA ZA KILA SIKU (13)

Tarjuma ya matendo ya swala

Ni vizuri kwa mtu anayeswali kutambua anachokitamka pamoja na kuwa na utulivu ili kuweza kupata utakaso wa nafsi na kujikurubisha zaidi kwa Allah (s.w.t).

a. Tarjuma ya Sura Fatiha.

Bismillaahir Rahmaanir Rahiim

Kwa jina la Allah Mwingi wa Rehma Mwenye kurehemu.

Alhamdu Lillaahi Rabbil 'Aalamiin

Shukrani zote anastahiki Allah (s.w.t) Mola wa viumbe wote.

Ar-Rahmaanir-Rahiim

Mwingi wa Rehma Mwenye Kurehemu.

Maaliki Yaumid-Diin

Mwenye Kumiliki Siku ya Malipo.

Iyyaaka Na'budu Wa Iyyaaka Nasta'iin

Wewe tu ndiye tunayekuabudu na wewe tu ndiye tunayekutaka msaada.

Ihdinas-Siraataal Mustaqiim

Tuongoze njia iliyonyooka.

Swala za kila Siku

Siratal-Ladhiina An 'Amta Alayhim

Njia ya wale ulio waneemesha.

Ghayril Maghdhuubi Alayhim Wala Dhwaalliin

Sio ya wale waliokasirikiwa wala ya waliyo potea.

b. Tarjuma ya Sura Ikhlas.

Bismillaahi Rahmaani Rahiim

Kwa jina la Allah Mwingi wa Rehma Mwenye kurehemu.

Qul Huwa Llaahu Ahad

Waambiye Yeye Mwenyezi Mungu ni wa pekee.

Allaahu Swamad

Mwenyezi Mungu Mkusudiwa.

Lam Yalid Walam Yuulad

Hakuzaa wala hakuzaliwa.

Walam Yakun Lahu Kufuwan Ahad

Na wala hana anayefanana naye hata mmoja.

c. Tarjuma ya Dhikri mbalimbali za Rukuu na Sujud

Subhaanallaah

Utakasifu ni wa Allah.

Subhaana Rabbiyal Adhiimi Wabihamdihi

Utakasifu ni wa Mola wangu ambaye ni mkuu na Anayehimidiwa.

Subhaana Rabbial a' laa wa Bihamdihii

Utakasifu ni wa Mola wangu aliye Mtukufu kabisa na Anayehimidiwa.

Samiallahu Liman Hamidah

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Allah (s.w.t) anamsikia kila anaye mhimidi.

Astaghfirullaaha Rabbii wa atuubu Ilayhi

Naomba msamaha kwa Allah (s.w.t) Mola wangu na ninatubia kwake.

Bihaulillaahi Aquwwaihi Aquumu wa aq'uud

Kwa nguvu na uwezo wa Allah ninasimama na ninakaa.

d. Tarjuma ya Dhikri ya Kunut

Rabbanaa Aatinaa Fid Duniyaa Hasanatan Wafil Aakhirati Hasanatan

Mola wetu tupe kheri za dunia na kheri za akhera.

Waqinaa 'Adhaaban Naari

Na utuepushe na adhabu ya moto.

Laa Ilaaha Illa Llaahul Haliimul Kariimu

Hakuna mola isipokuwa Allah (s.w.t) Aliye Mpole na Mkarimu.

Laa Ilaaha Illa Llaahul a'liyul 'adhiim

Hakuna mola isipokuwa Allah (s.w.t) Mtukufu aliye Mkuu.

Subhaanallaahi Rabbis-Samaawaati Ssab'i

Ametakasika Allah (s.w.t) Mola wa mbingu saba.


Wa Rabbil Ardhiinas Sab'i

Na Mola wa ardhi saba.

Wamaa Fii Hinna Wamaa Bainahunna

Na Mola wa kila kilichomo ndani ya (mbingu saba na ardhi saba) na kilichomo baina ya (mbingu saba na ardhi saba).

Wa Rabbil 'Arshil Adhiimu



Swala za Kila Siku

Na Mola wa arshi Tukufu
Wal Hamdu Lillaahi Rabbil 'Alamiin
Na kila sifa njema ni za Allah Mola wa viumbe

e. Tarjuma ya tasbihatu arbaa

Subhaanallaah
Utakasifu ni wa Allah

Wal Hamdu Lillaah
Na kila sifa njema ni za Allah.

Walaa Ilaaha Illallaah
Na hakuna Mola ila Allah

Wallaahu Akbar
Na Allah (s.w.t) ni mkubwa.

f. Tarjuma ya Tashahud na Salaam

Al Hamdu Lillaah
Kila sifa njema ni za Allah.

Ash-Hadu anlaa Ilaaha Ilaa Llaahu
Nashuhudia hakuna Mola ila Allah.

Wahdahuu Laa Shariika Lahu
Peke yake hana mshirika.

Wa Ash-hadu anna Muhammadan 'abduhu wa Rasuuluhu
Na ninashuhudia hakika Muhammad ni mja wake na ni Mtume wake.

Allaahumma Swalli Alla Muhammadin wa Aali Muhammadin
Ewe Mola mswalie Muhammad na kizazi cha Muhammad.

Wataqabbal Shafaa'atahu Fii Ummatihi war-fa'a Darajatahu
Na Umkubalie maombezi yake kwa umati wake na Umnyanyue daraja

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

yake.

Assalaamu Alayka Ayyuha Nnabiyyu Warahmatullaahi Wabarakaatuh
Amani iwe juu yako ewe Nabii na rehma za Allah (s.w.t) na baraka zake.

Assalaamu 'Alaynaa wa 'Alaa 'Ibaadillaahi Swaalihiina
Amani iwe juu yetu na juu ya waja wa Allah (s.w.t) walio wema.

Assalaamu Alaykum Warahmatullahi Wabarakaatuh
Amani iwe juu yenu na rehma za Allah (s.w.t) na baraka zake.

Maswali

1. Elezea tarjumu ya Sura Fatiha
2. Elezea tarjumu ya Sura Ikhlas
3. *Samiillaahu liman hamida* maana yake nini?
4. *Bihaulillaah...*ina maana gani?
5. *Wataqabbal.....*ina maana gani?
6. Bainisha tarjuma ya salaam.

Changamoto

Nini maana ya *Kadhaalika llahu Rabbi?*

Swala za kila Siku

Somo la Arobaini na Nane

SWALA ZA KILA SIKU (14)

Vinavyobatilisha swala

Vitu vinavobatilisha swala ni

1. Kuondoka kwa moja ya vitangulizi vya swala mfano mtu akagundua kuwa anaswali sehemu ya ghasbi au hana vazi la wajibu katika swala.
2. Kubatilika kwa wudhu mfano akapatwa na usingizi au kutokwa na haja. Iwapo atakuwa ndani ya swala kisha akatokewa na mojawapo ya mambo yanayobatilisha wudhu au ghusl, kwa mfano kulala ndani ya swala au akatokwa na mkojo na mfano wake, basi swala yake itabatilika.
3. Kukiacha kibla mfano kuelekea sehemu ambayo sio kibla au kuangalia sehemu nyingine wakati wa swala.

Iwapo kwa makusudi atageuka kwa mwili wake au uso wake au kimojawapo kiasi kwamba anaweza kuuona upande wake wa kulia au kushoto kwa urahisi, swala yake itabatilika. Na iwapo atakuwa amefanya hivyo kwa kusahau basi kwa mujibu wa ihtiyaat wajib swala yake itabatilika pia. Lakini kama atageuka kidogo kwa uso wake kuelekea mojawapo ya pande mbili swala yake haitabatilika.

4. Kuongea.

Iwapo ataongea ndani ya swala hata kwa neno moja swala yake itabatilika. Iwapo wakati wa kusoma Aya au dhikri akainua sauti yake kwa ajili ya kuwazindua watu wengine, ikiwa kufanya hivyo hakutapelekea kumtoa katika hali ya swala hakutakuwa na tatizo, kwa sharti kwamba afanye kiso-mo au dhikri kwa nia ya Qiraa au dhikri.

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Hairuhusiwi awapo ndani ya swala kuitika maamkuzi ambayo hayako katika tamko (sighah) la salaam. Ama kama hatokuwa ndani ya swala ni ihtiyaat wajib kuitika iwapo yatakuwa ni maneno ambayo kwa kawaida yanatambulika kuwa ni maamkuzi.

Baadhi ya mambo yanayohusu salaamu:

Ni wajibu kuitika salaam ya watoto wenye utambuzi, wakiwa wa kiume au wa kike. Vile vile ni wajibu kuitika salaam ya wanaume na wanawake.

Iwapo mtu ametoa salam kwa kusema "Salaam" badala ya "Salaam Alaykum", ikiwa inakubalika na watu kuwa ni salam basi atatakiwa kuitikia.

Ikiwa mtu ametoa salam mara nyingi kwa wakati mmoja itatosha kujibu moja kwa niaba ya zote. Na kama ni watu wengi wametoa salam kwa pamoja kwa wakati mmoja itatosha kujibu salam moja kwa niaba ya zote ikiwa itakuwa ni kwa swigha inayozijumuisha zote na kwa nia ya kuitika salam yao.

5. Kufunga mikono.

Iwapo atafanya makusudi kufunga mikono ndani ya swala kama yafanyavyo baadhi ya makundi ya Kiislam swala yake itabatilika, labda awe amefanya kwa kusahau. Lakini haizuiliwi kafanya hivyo katika hali ya taqiyyah.

6. Kusema amiin baada ya Sura-Fatiha.

Hairuhusiwi kusema neno "Amiin" baada ya surah Alhamdu. Kama atafanya hivyo kwa makusudi swala yake itabatilika, isipokuwa kama taqiyyah itamlazimu kufanya hivyo.

7. Kucheka kwa sauti.

Iwapo atafanya hivyo kwa makusudi ndani ya swala itabatilika.

8. Kulia (ikiwa ni kwa ajili ya mambo ya kidunia).



Swala za kila Siku

Kilio kinachokusudiwa hapa ni kulia kwa sauti. Iwapo atalia kwa makusudi kwa jambo la kidunia swala yake itabatilika.

9. Kuvunjika kwa sura ya swala kama kupiga makofi, kurukaruka, ila kama mtu ana nia ya kumfahamisha mtu jambo fulani akatumia ishara ya macho au nyusi bila kuondoa utulivu wa swala, hapo swala haitobatilika.

10. Kula au kunywa.

Akila au kunywa chochote ndani ya swala kwa mujibu ihtiyaat swala yake itabatilika, hata kama itakuwa kidogo.

11. Shaka zinazobatilisha swala kama shaka katika swala ya raka mbili au tatu.

12. Kupunguza au kuzidisha rukni (nguzo za swala).

Kupitwa na baadhi ya mambo ambayo ni wajibu kuyachunga wakati wa swala: iwapo ndani ya swala akakosa mojawapo ya mambo ya wajibu kuyazingatia katika swala basi swala yake itabatilika. Kwa mfano akigundua kuwa sehemu anayoswalia ni ya ghasb au kwamba mavazi aliyiovaa si yenye kumsitiri.

Ni makruhu kufunga macho wakati wa swala, na kujifuta kwa mikono usoni baada ya kumaliza kunut.

Mtu anayeswali hana wajibu wa kuitikia salamu ikiwa kuna watu ambao wanaweza kuitikia. Kama mtu alighafilika kujibu salamu na ukapita muda mrefu hatakuwa na wajibu tena wa kujibu salamu hiyo.

Hairuhusiwi kuonyesha husda, uadui na chuki dhidi ya watu wengine. Lakini mambo haya hayapelekei kubatilika kwa swala.

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Maswali

1. Taja vitu vinavyobatilisha swala
2. Je, ni wajibu kujibu salamu ya watoto walio mumayyiz?
3. Mtu akitoa salamu kwa zaidi ya mara moja inatosha kujibu mara moja tu?
4. Je, mtu akitabasamu swala itabatilika?
5. Ni mambo gani ambayo ni makruhu wakati wa swala?
6. Vipi wudhu utabatilika wakati wa swala?

Changamoto

Je, kuwekeana kinyongo kwa zaidi ya siku tatu kunabatilisha swala?

Swala za kila Siku

Somo la Arobaini na Tisa

SWALA ZA KILA SIKU (15)

Shaka za swala

Shaka za swala ziko ishirini na tatu, na zimegawanyika katika makundi matatu, nayo ni:

- i. Shaka zinazo batilisha nazo ni nane
- ii. Shaka ambazo mtu hatakiwi kuzijali nazo ziko sita
- iii. Shaka zilizo sahihi ziko tisa

a. Shaka zinazo batilisha swala

1. Shaka katika idadi ya rakaa katika swala ya rakaa mbili mfano asubuhi au swala ya msafiri.
2. Shaka katika idadi ya rakaa katika swala ya rakaa tatu kama magharibi.
3. Shaka katika swala ya rakaa nne kuwa ameswali rakaa moja au tatu.
4. Shaka katika swala ya rakaa nne kabla ya kumaliza sajda ya pili kuwa ameswali rakaa mbili au tatu.
5. Shaka baina ya rakaa mbili na tano au zaidi ya tano.
6. Shaka baina ya rakaa tatu na sita au zaidi ya sita.
7. Shaka baina ya rakaa nne na sita au zaidi ya sita.
8. Shaka katika idadi ya rakaa ambayo mtu hajui yuko rakaa ya ngapi.

b. Shaka ambazo hapaswi kuzijali

1. Shaka baada ya kupita tendo la swala, mfano katika rakaa ya tatu mtu akatia shaka kama alifanya Kunut.
 2. Shaka baada ya salaam.
 3. Shaka baada ya kupita muda wa swala.
- Iwapo baada ya kupita miaka mingi akatokewa na shaka ya kama swala zake zilikuwa sahihi au zilikuwa batili? Hatoizingatia shaka yake, (kwa sababu haizingatiwi shaka baada ya kukamilika kwa amali).

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

4. Shaka za mtu mwenye shaka nyingi (*kathirush shakk*)

Mtu mwenye kutokewa na shaka sana atajengea kutokea kwa kile alichokitilia shaka isipokuwa kama kutokea kwake kutapelekea kubatilika kwa swala kwani katika hali hii atajengea kutotokea. Na katika hilo hakuna tofauti kati ya rakaa na matendo au maneno katika swala (Kama vile akitilia shaka ya kwamba alisujudu au kurukuu au la, atajengea kuwa amali hiyo imetokea hata kama hajavuka sehemu husika. Ama akitilia shaka ya kama aliswali swala ya alfajiri rakaa mbili au tatu atajengea kwenye rakaa mbili).

5. Shaka baina ya Imam na maamuma.

6. Shaka katika swala za mustahab.

Hukmu ya shaka katika maneno na matendo ya swala za sunna ni kama hukmu ya maneno na matendo ya swala ya faradhi. Kwa maana kwamba ikiwa hajavuka sehemu husika ataizingatia shaka yake. Ama kama atakuwa ameshavuka eneo husika hatoizingatia shaka hiyo. Kwa mfano kama ametia shaka kwamba alisoma Alhamdu au rukuu au la, ikiwa atakuwa hajapita eneo husika basi atatekeleza kile kilichotiliwa shaka, na kama ameshapita eneo hilo hatoizingatia shaka yake.

c. Shaka zilizo sahihi

Shaka hizi zote katika idadi ya rakaa hupatikana katika swala za rakaa nne ikiwa:

1. Baina ya rakaa mbili na tatu baada ya kuinuka kutoka sijda ya pili.
2. Baina ya rakaa mbili na nne baada ya kuinuka kutoka sijda ya pili.
3. Baina ya rakaa mbili, tatu na nne baada ya kuinuka kutoka sijda ya pili.
4. Baina ya rakaa nne na tano baada ya kuinuka kutoka sijda ya pili.
5. Baina ya rakaa tatu na nne mahala popote katika swala.
6. Baina ya rakaa nne na tano katika hali ya kusimama.
7. Baina ya rakaa tatu na tano katika hali ya kusimama.
8. Baina ya rakaa tatu, nne na tano katika hali ya kusimama.

Swala za kila Siku

9. Baina ya rakaa tano na sita katika hali ya kusimama.

Mas'ala mbili zinazohusu shaka katika swala:

1. Idadi ya rakaa katika swala ya ihtiyat (swala ya kuondoa shaka) huswaliwa kulingana na dhana ya rakaa zilizotiliwa shaka, kwa hiyo katika shaka baina ya rakaa mbili na nne swala ya ihtiyat itaswaliwa rakaa mbili na katika shaka baina ya rakaa tatu na nne itaswaliwa ihtiyat kwa rakaa moja kwa kusimama au rakaa mbili kwa kukaa.

2. Iwapo atasoma neno katika dhikri za swala au katika aya za Qur'an au katika dua za qunuti kimakosa kwa bahati mbaya au kwa kusahau, hatosujudu sajda Sahw (sijda ya kusaha).

Maswali

1. Taja shaka zenye kubatilisha swala.
2. Taja shaka ambazo mtu hatakiwi kuzijali.
3. Nini wajibu wa *kathiiru shakk* akitoka na shaka katika swala?
4. Nini hukmu ya shaka katika swala ya mustahabu katika sijda kama imefanyika moja au mbili?
5. Taja shaka zilizo sahihi
6. Vipi mtu ataweza kujua kuwa wajibu wake katika swala ya ihtiyat ni rakaa ngapi?

Changamoto

Kama mtu akiwa katika rakaa ya kwanza akadhani yuko rakaa ya pili, baada ya kuswali rakaa ya tatu na nne akagundua kuwa alikuwa ameruka rakaa moja wajibu wake utakuwaje?

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Somo la Hamsini

SWALA ZA KILA SIKU (16)

Swala ya Ijumaa

a. Hukmu ya swala ya Ijumaa

Swala ya Ijumaa ambayo huswaliwa badala ya swala ya adhuhuri katika zama hizi ni amri ya khiari. Hii ina maana kwamba, mukallaf anaweza kuswali swala ya adhuhuri au swala ya Ijumaa, ila katika nchi ya Kiislamu haijuzu kuacha kuswali swala ya Ijumaa kwani swala hii ina thawabu na athari nyingi nzuri kijamii na mukallaf kwa kukosa mazuri hayo atakuwa hakufaidika na Ijumaa.

Wanawake pia wana *ijaza* (ruhusa) ya kushiriki katika swala ya Ijumaa na hupata thawabu kwa kufanya hivyo.

Swala ya Ijumaa inaitoshelezea swala ya adhuhuri. (Kwa maana nyingine swala ya Ijumaa inakuwa badala ya Adhuhuri).Japokuwa swala ya Ijumaa inakuwa badala ya swala ya Adhuhuri, kuswali adhuhuri baada ya swala ya Ijumaa katika namna ya ihtiyaat haina tatizo, hata kama imam anayeswalisha Ijumaa asiposwali Adhuhuri baada ya Ijumaa. Lakini iwapo atataka kuchunga ihtiyaat ataswali adhuhuri baada ya Swala ya Ijumaa kisha ataswali Alasiri kwa Jamaa. Ihtiyaat kamili hapa ni katika swala ya Alasiri kumfuata yule yaliyekwisha swali adhuhuri kwa ihtiyaata baada ya swala ya Ijumaa.

Si lazima kwa mtu anayetaka kuswali adhuhuri kusubiri kumalizika kwa swala ya Ijumaa bali anaweza kuswali mwanzo tu wa wakati.

Mtu anaweza kuswali swala ya adhuhuri kwa ihtiyat baada ya kumalizika kwa swala ya Ijumaa, ila haijuzu kuiswali kwa jamaa.

Swala za kila Siku

Hakuna tatizo kushiriki katika swala ya ijumaa inayoendeshwa na wanafunzi wa vyuo vikuu katika nchi za Ulaya na kwingineko, ambapo wengi wa washiriki pamoja na imam ni watu wa madhehebu ya sunni, kama itakuwa kwa ajili ya kulinda umoja wa Kiislamu na muungano wa Waislamu, na hivyo haitolazimu kuswali Swala ya Adhuhuri baada ya Ijumaa.

Msafiri pia ana ijaza ya kuswali swala ya Ijumaa badala ya adhuhuri.

b. Sharti za swala ya Ijumaa

- 1- Iswaliwe kwa jamaa, yaani haijuzu kuswali furada swala ya Ijumaa hata kama anayeswali yuko karibu na sehemu inayoswaliwa swala ya Ijumaa.
- 2- Kusipungue watu watano akiwamo na Imam.
- 3- Kuchunga masharti yote ya swala ya jamaa kama kupanga swafu pamoja na masharti mengine.
- 4- Kuwe na umbali angalau wa farsakh moja baina ya Ijumaa mbili yaani ikiwa umbali utakuwa pungufu ya farsakh moja Ijumaa ya mwanzo itakuwa sahihi na ya pili itakuwa batili na ikiwa zinaswaliwa pamoja zote mbili zitakuwa batili.

Imam wa swala ya Ijumaa anatakiwa kuwa mwadilifu na kama mtu atagundua kutokuwapo uadilifu kwa Imam hana ijaza (ruhusa) ya kuwashawishi watu kutokwenda swala ya Ijumaa. Kiongozi wa Waislamu ndiye aliye na mamlaka ya kuteua maimamu wa Ijumaa kila mahala.

Imam anatakiwa kuwa na naibu wake na kuswali nyuma ya naibu kunojuzu.

c. Wakati wa swala ya Ijumaa

Wakati wa swala ya Ijumaa huanzia tangu mwanzo wa wakati wa adhuhuri na haitakiwi kuchelewesha kwa zaidi ya masaa mawili kwa ihtiyat.

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

d. Jinsi ya kuswali swala ya Ijumaa

Ina rakaa mbili na kabla ya kuswali hutanguliwa na hotuba mbili. Ni mustahabu kusoma Fatiha na Sura kwa sauti; kama amabvy ambapo katika rakaa ya kwanza husomwa Sura Jumua'na na rakaa ya pili Sura Munafiquun.

Swala ya Ijumaa ni sahihi hata kama mtu hakuwahi hutuba zote mbili. Hotuba za Ijumaa ni vema zikafanyika kabla ya kuingia wakati wa adhuhuri ingawa si vibaya kuzisoma baada ya kuingia adhuhuri.

Baadhi ya mambo yanayoambatana na swala ya Ijumaa:

Hairuhusiwi kufanya jambo lolote linalopelekea kuleta mzozo baina ya Waislamu na kutenganisha umoja wao. Itakuwaje afanye hivyo kwa swala ya Ijumaa ambayo ni miongoni mwa alama za Uislam na mambo ya kuwaunganisha Waislamu, hivyo hairuhusiwi kuweka Swala nyingine ya Ijumaa katika mji unaoswaliwa Ijumaa.

Hakuna tatizo kumfuata Imam asiyekuwa wa Swala ya Ijumaa wakati wa kuswali Swala ya Alasiri ya siku ya Ijumaa. Kuna tatizo katika usahihi wa mtu anayeswali swala nyingine ya wajibu isiyokuwa swala ya Ijumaa kumfuata Imam wa Ijumaa.

Maswali

1. Nini maana ya amri ya khiyari katika Ijumaa?
2. Je, inajuzu kuswali adhuhuri sambamba na Ijumaa katika sehemu zilizo karibu?
3. Kutokuwapo uadilifu kwa imam kunabilisha swala ya Ijumaa?
4. Taja masharti ya swala ya Ijumaa
5. Je, swala ya Ijumaa ya mtu ambaye hakuwahi hutuba ni sahihi?
6. Je inajuzu kusoma hutuba za Ijumaa kabla ya kuingia adhuhuri?

Changamoto

Mtu anayetaka kuswali adhuhuri na Ijumaa ana wajibu gani, na Je, swala zake zote zitakuwa sahihi?

Swala za kila Siku

Somo la Hamsini na Moja

SWALA ZA KILA SIKU (17)

Swala ya msafiri (1)

Katika safari mtu anatakiwa kupunguza swala za rakaa nne na kuswali rakaa mbili kulingana na masharti tutakayoyaeleza baadaye. Kitendo cha kupunguza rakaa katika safari huitwa *qasri*.

A. Sharti za swala ya msafiri

Kutokana na masharti manane msafiri atawajibika kuswali qasri:

i. Safari isipungue farsakh nane kwenda na kurudi, na inabidi kwenda au kurudi kusipungue farsakh nne, masafa ya safari yanaanza kuhesabiwa mwisho wa mji wa msafiri.

Ni lazima kuhesabu Farsakh nane kuanzia mwisho wa nyumba za mji husika. Uainishaji wa mwisho wa mji utategemea kawaida, na hivyo kama kwa kawaida maduka, makampuni na viwanda sio sehemu ya mji basi masafa hayatohesabiwa kuanzia kwenye maeneo hayo bali yatahesabiwa kuanzia mwisho wa nyumba za mji.

ii. Tangu mwanzo wa safari kuwepo na nia ya kutimiza farsakh nane. Mtu aliyekusudia kusafiri farsakhi tatu, lakini tangu mwanzo akakusudia kupita njia ndogo kwa kiwango cha farsakhi moja kwa ajili ya kazi maalum kisha akarejea katika njia ya asili na kuendelea na safari yake, katika hilo hatokuwa na hukmu ya msafiri na wala kupetuka kwake katika njia asili kisha akarudi hakutojumuishwa kwenye masafa.

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

iii. Nia ya kukamilisha farsakh nane isibadilike katikati ya safari.

Iwapo mtu atasafiri kutoka mahali pa makazi yake kwenda mahali pengine pasipokuwa na umbali wa masafa ya kisheria, na kwa muda wa siku za wiki akawa anakwenda huko mara kadhaa kutoka mahali hapo kwenda mahali pengine kiasi cha kufikia jumla ya zaidi ya farsakhi nane, basi ikiwa wakati wa kutoka nyumbani hakuwa amekusudia kufikia umbali wa masafa ya kisheria na wala hakukuwa na kitenganisho kati ya mahali alipokusudia mwanzo na mahali pengine kwa kiasi cha masafa ya kisheria hatowajibikiwa na hukmu ya msafiri.

Iwapo atakusudia kusafiri umbali wa masafa ya kisheria lakini kabla ya kufikia farsakhi nne akabadili uamuzi au akasita kuendelea na safari, hatohusika na hukmu ya msafiri bali ataswali swala kamili.

iv. Safari isipite katika mji wa msafiri au sehemu atakayokaa zaidi ya siku kumi. Iwapo mtu atakusudia kusafiri umbali wa masafa ya kisheria lakini katikati ya safari akapita katika mji wake basi hapa safari yake itakuwa imekatika na ataswali swala kamili. Vile vile ikiwa atasafiri umbali wa masafa ya kisheria na akafika mahali aliponua kukaa siku kumi basi ataswali swala kamili.

v. Safari iwe inaswihi kisheria isiwe ya haram au kwa lengo la haram.

Mtu mwenye kufanya safari isiyokuwa ya maasi lakini akiwa njiani akakusudia kuikamilisha safari yake kwa ajili ya maasi, basi ni lazima aswali swala kamili kuanzia muda aliokusudia kuendelea na safari kwa ajili ya maasi. Na ni lazima arudie kuswali swala alizoswali baada ya kuendelea na safari kwa nia ya maasi, ataziswali upya zikiwa kamili.

Iwapo atajua kwamba katika safari yake anayokusudia kuifanya atakumbana na maasi na mambo ya haramu, basi ikiwa safari yake sio kwa lengo la kuacha wajibu au kufanya jambo la haramu hukmu yake itakuwa sawa na hukmu ya wasafiri wengine, kwa maana atapunguza swala yake.

Swala za kila Siku

Akijua kwamba atakutana na hali ya kuacha baadhi ya wajibu wa swala, ni ihtiyaat waajib kuacha kufanya safari kama hiyo. Isipokuwa labda kama akiicha atapata madhara au tabu kubwa. Vyovyote iwayyo haruhusiwi kabisa kuacha swala.

vi. Msafiri asiwe katika watu wanao hama hama. Makabila yanayohama kwa kipindi cha mwezi au miezi miwili kutoka sehemu wanayoishi lakini siku nyingine za mwaka wanaishi katika maeneo ya joto na maeneo ya baridi; basi ikiwa ujenzi wao ni wa kuendelea katika hii hali na wakayafanya maeneo ya joto na ya baridi kuwa makazi yao ya kudumu basi wataswali swala kamili.

vii. Safari isiwe ndiyo kazi ya msafiri kama dereva na rubani ambapo kwa hali hiyo safari yake ya kwanza na ya pili itakuwa sahihi kuswali qasri ila kuanzia safari ya tatu ataswali kamili.

Kadhalika mtu ambaye kazi yake si msafiri lakini kusafiri ndio hufanikisha kazi yake atatakiwa kuswali (swala) kamili. Ama kwa mtu ambaye kazi yake ni kusafiri ikiwa atasafiri kwa nia nyingine na si katika kazi (yake) atafuata hukmu za msafiri kama kawaida. Na kama atakaa sehemu kwa muda wa siku kumi, safari yake ya mwanzo ataifanya kuwa na hukmu za msafiri.

Kutafuta elimu sio shughuli, na kwa hivyo wanafunzi wa vyuo vikuu ambao husafiri kila siku au kila wiki kwa ajili ya masomo wataswali pungufu safarini mwao. Lakini iwapo mhusika atakuwa ameamriwa kutafuta elimu kama vile mwalimu anayefanya kazi ya kufundisha akawa anatakiwa kusafiri kwenda sehemu kwa ajili ya kusoma, basi hapo ataswali kamili safarini mwake.

Ziyaarah sio shughuli, na hivyo mtu anayesafiri kwa ajili ya kumzuru Sayyidat Maasuma (a.s.) au kwenda Qum kwa ajili ya kufanya A'mal za msikiti wa Jamkaraan, basi hukmu yake katika safari yake hii ni sawa na

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

hukmu ya wasafiri wengine hivyo ataswali pungufu.

viii. Msafiri lazima afike mipaka ya ruhusa ya kufanya qasri (kupunguza), yaani sehemu ambayo adhana ya mji wake haisikiki wala kuonekana kuta za majumba ya mji wake.

Maswali

1. Taja masharti ya swala ya msafiri.
2. Nini maana ya safari ya haram?
3. Nini maana ya **hadu tarakhus**?
4. Kusema msafiri asiwe kazi yake ni safari kunamaanisha nini?
5. Nini hukmu ya mtu anayehamama katika safari?
6. Je, hadu tarakhus inatosheleza kwa alama moja tu?

Changamoto

Vipi hadu tarakhus itagundulika katika miji ambayo nyumba zake zimeungana?

Swala za kila Siku

Somo la Hamsini na Mbili

SWALA ZA KILA SIKU (18)

Swala ya msafiri (2)

B. Mambo yanayovunja safari

- i. Kupita katika mji wa msafiri.
- ii. Kupita sehemu atakayokaa kwa siku kumi.
- iii. Kukaa sehemu mwezi mmoja bila nia.

C. Mji

Mji umegawanyika aina mbili:

1. Mji wa asili ambao ni mahala mtu alipozaliwa na kukulia, kuzaliwa tu katika mji bila kukulia hapo hautakuwa mji wa asili wa mtu huyo.
2. Mji wa kuchagua (mji wa pili) ambao ni mahala mtu alipopachagua kwa ajili ya kuishi, mahala hapo patahesabika kuwa ni mji wake wa pili ikiwa mtu ameweka nia ya kuishi hapo daima.

Kuzaliwa tu hakuwezi kuhakikisha kuwa ni mji asili wa mtu; ispokuwa pale alipokulia kwa wazazi wake. kwa mfano kama mtu amezaliwa Tehran, lakini akakulia Qum kwa wazazi wake, basi mji wake wa asili utakuwa ni Qum

iv. Idadi ya miji

Mtu anaweza kuwa na mji zaidi ya mmoja kulingana na alivyochagua, ila kama umbali wa mji mmoja hadi mwingine unatimia masafa ya safari kwa muda atakaokuwa safarini atafanya hukmu za msafiri njiani ila akiingia katika mji wake ataswali kamili.

v. Kuuhama mji

Maana ya kuuhama mji ni kutokaa katika mji fulani kwa lengo la kutorudi

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

hapo kwa ajili ya makazi, na kama hajauhama kwa nia hiyo bado utahesabika kuwa ni mji wake na ataswali kamili akiwa hapo.

e. Kufuata mji wa wazazi au mume

Mke akiolewa na kwenda kuishi mji mwingine na mume wake, hiyo haimpelekei mke kuuhama mji wake wa asili, na si lazima kwa mke kufuata mji wa mume. Mtoto ambaye hajafikia kujitegemea anafuatana na wazazi wake ikiwa watahama mji na kuchagua mji wa kuishi, huo utakuwa ni mji wake pia.

Maswali

1. Taja mambo yanaovunja safari
2. Nini tofauti ya mji wa asili na mji wa kuchagua?
3. Je, yawezekana mtu akawa na mji zaidi ya mmoja? Elezea
4. Taja masharti ya mji wa kuchagua
5. Nini maana ya kuhama mji?
6. Mke aliyeolewa mji mwingine na anapokwenda kwa wazazi wake ataswali kwa wajibu gani? (kamili au atapunguza?)

Changamoto

Je, mahala pa kazi pana hukmu ya mji?

Swala za kila Siku

Somo la Hamsini na Tatu

SWALA ZA KILA SIKU (19)

Swala ya msafiri (3)

D. Nia ya kukaa siku kumi

Msafiri akiwa na nia ya kukaa mahala kwa muda wa siku kumi mfululizo au akajua analazimika kukaa siku kumi atawajibikiwa kuswali kamili, na ni lazima siku hizo kumi ziwe katika mji mmoja.

E. Kukaa mwezi mzima bila nia

Msafiri ambaye hajui kama atakaa mahala kwa siku kumi au pungufu ataswali swala ya msafiri, na ikifika siku thalathini atawajibikiwa kuswali kamili hata kama ataondoka siku hiyo hiyo.

F. Mji mkubwa

Hukmu ya msafiri haitofautishi baina ya miji mikubwa wala midogo. Kwa kuweka nia ya kukaa siku kumi ndani ya mji haina haja ya kubainisha ni eneo gani katika mji utakaokaliwa.

Maswali

1. Nini hukmu ya mtu ambaye anajua kuwa atakaa sehemu fulani kwa siku zisizozidi kumi?
2. Ikiwa mtu anasafiri kwa siku zisizozidi kumi na akaweka nia ya siku kumi ili aswali kamili nini itakuwa hukmu yake?
3. Je, mtu akiweka nia ya kukaa siku kumi analazimika kuweka nia ya kutoka mahala hapo kwa pungufu ya masafa kisheria?
4. Ili kuwa mkazi (Iqama) inakubalika kwa njia ngapi?
5. Nini hukmu ya swala ya mtu ambaye hajui atakaa sehemu siku ngapi?

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

6. Nini tofauti ya mji mkubwa na mdogo katika swala ya msafiri?

Changamoto

Nini wajibu wa mtu ambaye kwa muda alikuwa akiswali qasri katika mji mkubwa?

Swala za kila Siku

Somo la Hamsini na Nne

SWALA ZA KILA SIKU (20)

Swala ya qadhaa

Mtu ambaye aliacha kuswali swala za wajibu, anawajibikiwa na qadhaa ya swala hizo, lakini mtu ambaye alikuwa hana fahamu hawajibikiwi na qadhaa.

Kadhalika kafiri aliyeingia katika Uislamu na mwanamke aliye katika hedhi na nifasi hawajibikiwi na qadhaa. Baada ya kupita muda wa swala mtu akagundua kuwa swala yake ilikuwa batili anawajibikiwa na qadhaa.

Kama mtu hajuwi kuwa anadaiwa swala ngapi, ataswali qadhaa zile alizo na yakini nazo.

Vile vile sio lazima kuzunguka katika kuswali kwa maana ya kurudiarudia swala kwa lengo la kuchunga utaratibu, na hivyo mtu anayetaka kulipa swala za mwaka mzima anaweza kuswali kwa utaratibu ufuatao:

Mfano, ataswali swalatus-subh mara ishirini kisha adhuhuri na Alasiri mara ishirini na kisha Magharibi na Isha mara ishirini, na ataendelea hivyo mpaka akamilishe swala za mwaka mzima. Vile vile anaweza kuanza na swala mojawapo na kuswali kwa utaratibu anaotumia katika swala za kila siku.

Mtu ambaye anatakiwa kulipa swala lakini akawa hajui kiwango chake, kwa mfano akawa hajui kuwa alipitwa na swala mbili au tatu, inatosha kulipa kiwango cha chini kabisa

Iwapo kwa mfano atafanya ghusli tatu za joshu la janaba katika siku ya 20, ya 25 na ya 27 kisha akagundua kuwa mojawapo ya ghusli hizo ilikuwa batili, basi kwa mujibu wa ihtiyaat wajib atalipa swala atakazokuwa na

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

uhakika wa kutakiwa kuzilipa.

Swala za sunna na za mustahab hazihesabiwi kuwa mbadala wa swala ya qadhaa, na hivyo ikiwa ana dhimma ya swala ya qadhaa anatakiwa aiswali kwa nia ya swala ya qadhaa.

Watu wasiokuwa na uwezo wa kulipa swala zote katika wakati wa sasa, wanatakiwa kulipa swala husika kwa kiasi chochote watakachoweza, na zitakazobaki watatakiwa kutoa wosia wa kulizilipa.

a. Swala ya ujira

Mtu hana ruhusa ya kuswali swala za mtu aliye hai hata kama ni kwa kua-jiriwa. Lakini baada ya kufa jambo hili linaruhusiwa.

Katika swala ya malipo hakuna sharti la kutaja mambo makhsusi ya marehem. Lakini kinachotakiwa ni kuchunga tu mpangilio baina ya swala za Dhurain na Ishaain (Adhuhuri na Alasiri, na Magharibi na Isha). Na iwapo katika mkataba wa malipo mwajiriwa hakuwekewa sharti maalum (kwa mfano haikutajwa katika mkataba kwamba swala inatakiwa ifanyike msikitini au wakati fulani) na ikawa haikutajwa namna maalum katika mkataba huo, basi mwajiriwa anatakiwa aswali pamoja na mustahab kwa utaratibu uliozoeleka, isipokuwa hatolazimika kuleta adhana kwa kila swala.

b. Swala ya qadhaa ya wazazi

Ni wajibu kwa mtoto mkubwa wa kiume kulipa swala za wazazi wake baada ya kufariki kwao, ikiwa swala hizo hawakuziacha kwa makusudi ya kumuasi Allah (s.w.t) Mtukufu. Pamoja na hali hiyo kwa ihtiyat mustahab-bu anaweza kuzilipa hata kama wazazi hao hawakuswali katika mazingira ya kumuasi Allah (s.w.t).

Mtoto mkubwa wa kiume ni yule ambaye ndiye wa kwanza kwa watoto wa kiume hata kama alitanguliwa na watoto wa kike na wa mwisho akawa wa

Swala za kila Siku

kiume.

Iwapo mtu atalipa swala za baba au mama basi hapo wajibu wa mtoto mkubwa kuzilipa huondoka.

Mtoto mkubwa anatakiwa kulipa kiwango ambacho ana uhakika nacho katika swala zilizowapita baba au mama. Na iwapo hajui kama walipitwa na swala au la, hatolazimika kuulizia na kulitafiti swala hilo.

Ni lazima kwa mtoto mkubwa kulipa swala za baba au mama kwa namna yoyote inayowezekana, na ikiwa atashindwa kufanya hivyo hata kwa kumuajiri mtu mwingine basi atakuwa ni mwenye kusamehewa.

Mtu anayewajibikiwa qadhaa ya wazazi hali ya kuwa mwenyewe ana qadhaa ya wajibu anaweza kutanguliza kulipa yoyote. Ikiwa mtoto mkubwa wa kiume atafariki kabla ya wazazi au baada ya wazazi, qadhaa hizo hazitamuwajibikia mwanawe mkubwa wala ndugu yake.

Maswali

1. Je, Kafiri aliyeingia katika Uislamu ana wajibu wa kuswali qadhaa?
2. Je, swala ya mustahabu inatosheleza swala ya qadhaa?
3. Swala ya ujira ni ipi?
4. Wazazi ambao hawajawahi kuswali kabisa, Je wajibu wa qadhaa kwa mtoto wa kiume unaondoka?
5. Mtoto mkubwa wa kiume ni yupi?
6. Baina ya swala ya qadhaa ya mzazi na swala ya qadhaa ya mtu anayewajibikiwa na qadhaa, Je ipi itatangulia?

Changamoto

Mtu aliyepoteza fahamu na kushindwa kuswali, Je, mtoto wake wa kiume atawajibikiwa na qadhaa?

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Somo la Hamsini na Tano

SWALA ZA WAJIBU

1. Swala ya majanga

Swala ya majanga (swalatul-ayat) inakuwa wajibu katika hali nne:

- a. Kupatwa kwa jua hata kama ni kidogo
- b. Kupatwa kwa mwezi hata kama ni kidogo
- c. Tetemeko la ardhi
- d. Tukio lolote linaloleta hofu kwa watu kama kudidimia kwa ardhi, kuan-guka kwa mlima, upepo mkali, kiza kinene n.k.

Wajibu wa swala ya majanga unawahusu wale tu wakazi wa mji au eneo lililotokea janga hilo pamoja na maeneo ya karibu na hapo.

Kituo cha usajili wa matetemeko kikitangaza mara nyingi kutokea kwa matetemeko mepesi ya ardhi katika mji fulani, lakini watu waishio katika eneo husika wakawa hawakuyasikia hata kidogo wakati yanatokea wala moja kwa moja baada ya muda mfupi, basi katika hali hii hawatolazimika kuswali swala ya majanga.

Kila tetemeko - liwe zito au jepesi - likihesabiwa kuwa ni lenye kujitege-meza lina swalatul-ayaat ya pekee yake.

Jinsi ya kuswali swala ya majanga

Swala ya majanga ina rakaa mbili na kwa kila rakaa ina rukuu tano na sijda mbili na inaweza kuswaliwa katika njia tofauti kama:

- a. Nia, Takbiratul Ihram, Sura-Fatiha na Sura nyingine, kurukuu, kusima-ma, Sura-Fatiha na Sura nyingine, kurukuu, kusimama na kuendelea kati-ka hali hiyo hadi kuhakikisha kwamba imesomwa Sura-Fatiha na Sura mara tano na rukuu tano kabla ya kusimama na kusujudu, na kufanya hivyo kwa rakaa ya pili na baada ya hapo kusoma tashahud na kisha Salaam.

Swala za Wajibu

- b. Nia, takbiratul ihram, Sura-Fatiha na aya chache za Sura, rukuu, kusimama, kuendelea na ile sura aliyoianza kwenye kisimamo cha kwanza, rukuu, kusimama, na kuendelea na hali hiyo hadi kufikia mara tano; yaani atakuwa amesoma Alhamdu moja na sura moja iliyogawanywa mara tano, kisha atasujudu na kusimama kwa rakaa ya pili ambapo itafanyika kama hivyo kisha ni kusujudu, kusoma tashahud na kisha salaam.
- c. Kuswali rakaa mbili kwa njia mbili tofauti; rakaa moja iswaliwe kwa mfumo wa sura tano na rakaa nyingine kuswaliwa kwa mfumo wa aya tano.
- d. Kuswali kwa njia ambayo sura moja inagawanywa, lakini inakamilika kabla ya kumaliza rukui tanokwenye rakaa ya kwanza, ya pili, ya tatu au ya nne; hapa ataanza tena Sura Fatiha na sura nyingine aikamilshe ikiwa ni kisimamo cha tano au baadhi ikiwa si kisimamo cha tano.

Ni ihtiyat ya wajib kuwa "*Bismillaah*" isihisabiwe kuwa ni sehemu ya Sura

2. Swala ya Idil Fitri na Idil Adh' ha

Swala za Idi katika zama hizi za ghaiba ya Imam wa Zama (a.s.) ni mustahabu na si wajibu.

Katika swala za Idi kila moja ina rakaa mbili ambapo katika rakaa ya kwanza baada ya kusoma Sura Fatiha na Sura nyingine zitasomwa takbira tano ambapo kila takbira itafuatiwa na qunut na baada ya qunut ya tano itasomwa takbira na atarukuu, halafu atasujudu sijda mbili na kisha kusimama kwa ajili ya rakaa ya pili.

Na katika rakaa ya pili baada ya kisomo cha Sura-Fatiha na Sura nyingine atasoma takbira nne zitakazofatiwa na qunut na baada ya qunut ya nne atasoma takbira kisha atarukuu, kisha atasujudu Sijda mbili, halafu atakaa kwa ajili ya kusoma tashahud na hatimaye kutoa Salaam.

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Hakuna tatizo qunuti kuwa ndefu au fupi na wala haipelekei swala kubatiliika. Ama kuizidisha au kuipunguza kutoka kwenye idadi iliyotangulia kumetajwa kuwa ni jambo lisiloruhusiwa.

Wawakilishi wa Waliyyul Faqiih waliopewa ruhusa kutoka kwake wanaruhusiwa kuweka swala ya Id. Vilevile maimamu wa jama'ah walio-teuliwa kutoka kwake wanaruhusiwa kuswali swala ya Id kwa jamaa katika wakati wa sasa (yaani katika zama za ghaiba ya Imam a.f). Ama watu wengine ni ihtiyat kuswali mmoja mmoja. Lakini hakuna tatizo kuswali kwa jamaa kwa kutarajia thawabu na sio kwa kutekeleza wajibu. Hata hivyo iwapo maslahi yatalazimisha kuswali Id moja katika mji basi ni bora asiisimamie mtu mwingine tofauti na imam wa jumu'a aliyeteuliwa na Waliyyul- Faqiih.

Swala za Idi hazina iqama, lakini kama imam ataleta iqama kwa ajili ya swala ya Id, hilo halitadhuru swala

Pia swala za id hazina qadhaa (kuzilipa wakati mwingine).
Kuna mushkeli kukaririka swala ya Id kwa jamaa kwa ajili ya wengine.

Maswali

1. Swala ya majanga inakuwa wajibu kwa Sura ngapi?
2. Je, likitokea tetemeko zaidi ya moja hukmu ya swala ya majanga itakuwaje?
3. Swala ya majanga huswaliwa vipi?
4. Nini hukmu ya swala za Idi katika zama za ghaiba?
5. Swala za Idi zina qunut ngapi?
6. Je, swala za Idi zina qadhaa?

Changamoto

Nini hukmu ya mtu ambaye wakati wa kutokea kwa tetemeko alikuwa amezimia na akazinduka baada ya kumalizika kwa tukio hilo?

Swala ya Jamaa

Somo la Hamsini na Sita

SWALA YA JAMAA (1)

1. Umuhimu wa swala ya jamaa

Swala ya jamaa ni moja katika mustahabu muhimu na ni jambo lililo na faida sana katika Uislamu. Swala ya jamaa huswaliwa kwa kuanzia watu wawili, yaani imamu na maamuma mmoja.

Inajuzu kwa Imamu kufuatwa katika swala ya jamaa hata kama hakuweka nia ya kuswalisha jamaa, na haijuzu kuswalisha jamaa kwa nia ya ihtiyat. Si sahihi kumfuata maamuma hali ya kuwa bado yumo katika swala ya jamaa.

Inajuzu kwa mtu kufuata swala ya jamaa tofauti na swala anayoswali imamu, mfano imamu anaswalisha swala ya isha, maamuma anaweza kumfuata kwa swala ya magharibi.

Wanawake wanaruhusiwa kuswali swala ya jamaa na suala hili lina thawabu sana.

Haijuzu kuswali jamaa mbili katika sehemu zilizo karibu ikiwa suala hilo litasababisha mtafaruku na ikhtilafu kwa waumini.

Tofauti katika taqliid sio kizuizi cha kumfuata mtu. Hivyo mtu anayemfuata Marja' fulani katika swala ya msafiri anaweza kumfuata mtu anayefanya taqliid kwa marja'a mwingine ndani ya swala husika. Lakini haisihi kumfuata mtu ambaye kwa mujibu wa fat'wa ya marja'a wa maamuma anatakiwa kuswali pungufu wakati kwa mujibu wa fat'wa ya marja'a wa imam anatakiwa kuswali kamili au kinyume chake.

Hairuhusiwi kuswali swala ya pekee yake wakati inaposwaliwa jamaa iwapo kufanya hivyo kutachukuliwa kuwa ni kudhoofisha swala ya jamaa au kumvunjia heshima imam wa jamaa ambaye watu wanauamini uadilifu wake.

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Haijuzu kwa mtu kuswali furada katika sehemu inayoswaliwa jamaa ikiwa kufanya hivyo ni kumfanyia khiyana imam na kuonyesha kutoheshimu swala ya jamaa.

Ikiwa mtu ameingia katika jamaa na kukuta imam yuko katika tashahud, ili apate thawabu za jamaa, atatakiwa kutoa Takbira na kukaa katika tashahud pamoja na imam, kwa namna ya kujitofautisha, lakini asitoe salaam, na baada ya imam kutoa salaam mtu huyo atasimama na kuendelea na swala yake.

Haipendezi (inatia mushkel) kusoma dua ndefu na kufanya ibada za mustahabbu za ziyada, kama vile kuswali swala za sunna au kusoma dua ya tawassuli na dua nyinginezo ndefu kabla ya swala au baada ya swala ya jamaa au katikati yake katika maofisi ya serikali. Jambo hili ni miongoni mwa mambo yanayochukua muda mrefu na kupoteza wakati wa kazi za idara na kuchelewesha utekelezaji wa kazi za wajibu katika idara hizo.

Haijuzu kwa imam wa jamaa kuchukua malipo ila ikiwa malipo hayo ni kwa kazi za utangulizi wa yeye kufika katika sehemu ya kuswalisha jamaa.

Maswali

1. Swala ya jamaa inatimia kwa kuwepo watu wangapi kwa uchache?
2. Je, inajuzu kumfuata imam kwa swala tofauti na anayoswali?
3. Je, inajuzu kuswali jamaa mbili katika sehemu zilizo karibu?
4. Nini hukmu ya mtu anayeswali furada katika sehemu ambapo inasimama swala ya jamaa?
5. Je, inajuzu kwa imam wa jamaa kuchukua malipo?
6. Nini hukmu ya kuswali jamaa nyuma ya imam ambaye hajaweka nia ya kuswalisha?

Changamoto

Je, maamuma anaweza kuwa imam kwa wakati ambao yumo katika swala ya jamaa?

Swala ya Jamaa

Somo la Hamsini na Saba

SWALA YA JAMAA (2)

2. Sharti za swala ya jamaa

- a. Kutokuwapo na kizuizi.
- b. Nafasi anayosimama imamu isiwe juu sana kuizidi ile wanayosimama maamuma kwani inapelekea kubatilika kwa jamaa.
- c. Kusiwepo na umbali mkubwa baina ya imamu na maamuma.
- d. Maamuma asintangulie imamu.

Kama safu (mstari) moja imeungwa na watu wanaoswali qasri pekee yao na safu inayofuata ina watu wanaoswali swala kamili itawalazimu wale wanaoswali kamili baada ya rakaa ya pili kuweka nia ya furada na kuen-delea na swala. Hali hiyo ni sawa hata kama wale walioswali safu ya mbele watasimama kwa haraka kuungana upya katika swala ya jamaa katika rakaa mbili zinazofuatia au hawakusimama.

Na kama safu moja wamesimama watu wasiokuwa balegh, safu inayofuata jamaa yake itakuwa sahihi.

Wanawake wanaweza kuswali nyuma ya wanaume hata bila ya kuwa na kizuizi au pazia lakini kama wanaswali pembeni mwa wanaume ni bora kuwapo na pazia.

3. Hukmu za swala ya jamaa

Haijuzu kwa maamuma kusoma Sura-Fatiha na Sura nyingine hata katika swala ya adhuhuri na alasiri.

Imamu akiwa rakaa ya tatu au ya nne, ya swala ya isha, na maamuma akawa rakaa ya pili itawajibika kwa maamuma kusoma Sura Fatiha na Sura

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

kimyakimya.

Kama mtu aliunga jamaa katika rakaa ya pili na kwa kutokujua hukmu hakukaa tashahud katika rakaa iliyofuata swala yake itakuwa sahihi ila itamlazimu kulipa qadhaa ya tashahud na kuleta sijda mbili za kusahau.

Kama mtu aliunga jamaa katika rakaa ya tatu akidhani ni rakaa ya kwanza na hakusoma Sura Fatiha na Sura, akigundua kabla ya rukuu atatakiwa kusoma ila kama alikwisha rukuu swala yake itakuwa sahihi lakini atawajibikiwa na sijda mbili za kusahau kutokana na kusahau kusoma Sura Fatiha na Sura.

Kama imam akisahau na baada ya Takbira akaenda rukuu badala ya kusoma Sura Fatiha na Sura, maamuma akigundua atalazimika kuweka nia ya furada na kusoma Sura Fatiha na Sura.

Inaruhusiwa kufuata swala ya jamaa ya Ahlu Sunna kwa ajili ya kulinda umoja wa Kiislamu. Na iwapo kulinda umoja huo kutamlazimisha mtu kufanya kimatendo yale wanayofanya katika swala, hilo halidhuru usahihi wa swala yake, bali ni jambo sahihi na linaloruhusiwa, hata kama itakuwa ni pamoja na kusujudu kwenye zulia au kitu kingine. Lakini hairuhusiwi kufunga mikono wakati wa kuswali pamoja nao isipokuwa kama dharura italazimisha kufanya hivyo.

4. Masharti ya imam wa swala ya jamaa

a. Awe balegh.

Hairuhusiwi mtu asiye baleghe kuwa Imam hata kama maamuma sio baleghe.

b. Awe na akili.

Swala haisihi kwa kuongozwa na mwendawazimu hata kama hatatokewa na hali hiyo akiwa katikati ya swala.

c. Awe mwadilifu.

Iwapo Imam wa jamaa atazungumza maneno fulani au akafanya jambo la

Swala ya Jamaa

mzaha kwa namna isiyoendana na hadhi na nafasi ya mwanachuoni wa dini, ikiwa kufanya hivyo hakutokwenda kinyume na sheria uadilifu wake hautoondoka.

- d. Awe amezaliwa kwa njia ya halali (asiwe mtoto wa zina).
- e. Awe Shia Ithnaashariya.
- f. Awe anaswali kwa usahihi.
- g. Awe mwanaume.

Baadhi ya mambo yanayohusu masharti ya imam wa Jamaa:

Ikiwa yawezekana kumfikia Alim wa dini hairuhusiwi kumfuata mtu mwingine.

Iwapo imam wa Jamaa atakuwa ni mwenye uwezo wa kutulia sawasawa katika hali ya kawaida wakati wa qiyaam, na akawa na uwezo wa kuilinda hali hiyo wakati wa kusoma Alhamdu na surah pamoja na dhikri na matendo mengine ya swala, na akawa na uwezo wa kurukuu na kusujudu kikamilifu, na akawa na uwezo wa kufanya wudhu sahihi, basi hakuna tati-zo kwa watu wengine kumfuata katika swala baada ya kuthibitisha kuwa ana masharti mengine ya uimamu, na kuswali pamoja naye ni sahihi.

Hata hivyo iwapo mkono au mguu wake utakuwa umekatwa wote au kupooza, basi ni tatizo kwa yeye kuswalisha jamaa. Lakini iwapo kidole gumba cha mguu ndicho kilichokatwa basi ni sahihi kuwa imam.

Iwapo mtu atakuwa na udhuru wa kufanya ghuslu anaweza kufanya tayam-mam badala yake na ni sahihi kuwa imam wa jamaa, na wala hakuna tati-zo watu wengine kumfuata.

Ikiwa hapo kabla watu waliswali nyuma ya mtu asiye na sifa za kufuatwa kutokana na wao kutojua hukmu za kisheria, swala zao ni sahihi na wala hawalazimiki kuzirudia au kuzilipa, kwa mfano: kama watakuwa

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

wameswali nyuma ya mtu aliyekatika mkono wa kulia.

Mas'ala mbalimbali kuhusu swala:

Hakuna njia maalum ya kuwaamsha watu ili watekeleze swala ya alfajiri kwa wakati wake.

Ni mustahab kwa Waliy wa mtoto kumfundisha hukmu za kisheria na za kiibada baada ya kufikia umri wa upambanuzi.

Makusudio ya kuwa mlevi hana swala kwa siku arubaini, ni kwamba ulevi huifanya swala isipokelewe katika kipindi hicho, na wala haina maana kwamba kunywa pombe kunamuondolea mtu wajibu wa kutekeleza swala na kulazimika kuzilipa au kwamba analazimika kufanya yote mawili kwa pamoja yaani kutekeleza na kulipa.

Maswali

1. Je, ni lazima kuweka kizuizi ikiwa wanawake wanaswali nyuma ya wanaume?
2. Nini hukmu ya maamuma kusoma Sura Fatiha na Sura katika swala ya adhuhuri na alasiri?
3. Imamu akisahau na kwenda rukuu badala ya kusoma Sura Fatiha na Sura, Je, maamuma ana wajibu gani?
4. Nini hukmu ya jamaa kwa imamu ambaye hajui kuswali kwa usahihi?
5. Je, inajuzu kwa mwanamke kuwa imam wa jamaa?
6. Taja masharti ya swala ya jamaa.



Changamoto

Wakati wa hija Masuni huswali swala ya magharibi kabla ya kuingia wakati, Je, inajuzu kuwafuata? na Je, swala hiyo itakuwa sahihi?



Sehemu ya Nne

SWAUMU



Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Somo la Hamsini na Nane

SWAUMU (1)

1. Maana ya swaumu

Katika sheria ya Kiislamu, swaumu ni kujizuia mtu kutokana na yale ambayo yanabatilisha swaumu tangu kuchomoza alfajiri ya kweli hadi kuzama kwa mawingu mekundu wakati wa magharibi.

2. Aina za swaumu

- a. Swaumu za wajib, mfano mwezi wa Ramadhani.
- b. Swaumu za mustahabu, mfano mwezi wa Rajab na mwezi wa Shaabani.
- c. Swaumu za makruhu, mfano swaumu ya siku ya Ashura.
- d. Swaumu ambazo ni haramu, mfano swaumu ya siku ya Idil Fitri na Idil Haj.

Mtu kama ana uhakika kuwa akifunga atapata madhara hatakiwi kufunga bali inakuwa ni haramu kwake, iwe kutokana na uzoefu alionao au kutokana na mwongozo wa daktari.

Mtu mwenyewe ndiye mwenye kujua kuwa anaweza kufunga au la. Ikiwa daktari atakataza kufunga hali ya kuwa mwenyewe anaweza kufunga basi swaumu kwake itakuwa wajib.

Kama mtu anajua kuwa swaumu haina madhara kwake baada ya kufunga akapata madhara atawajibikiwa na qadhaa ya siku hiyo.

3. Swaumu za wajib

- a. Swaumu ya Ramadhani.
- b. Swaumu ya qadhaa (kulipa).

Swaumu

- c. Swaumu ya kafara.
- d. Swaumu ya qadhaa ya wazazi.
- e. Swaumu ya mustahab iliyokuwa wajib kutokana na nadhiri au kiapo.
- f. Swaumu ya siku ya tatu ya itikafu.
- g. Swaumu badala ya kuchinja katika hija.

4. Masharti ya wajibu wa swaumu

Swaumu inakuwa wajibu kwa mukallaf ambaye kwa masharti haya pia swaumu yake itakuwa sahihi

- a. Balegh.
- b. Akili.
- c. Mwenye uwezo wa kufunga.
- e. Hajapoteza fahamu.
- f. Hayuko safarini.
- g. Twahara.
- h. Hadhuriki kutokana na swaumu.
- i. Hana mashaka na swaumu.
- j. Mwislamu.
- k. Muumini.
- l. Awe na nia ya kufunga.
- m. Kuacha yale yanayovunja swaumu.

Swaumu inakuwa ni wajibu kwa watu ambao wamekamilisha masharti yaliyotajwa hapa, kwa hiyo mtoto mdogo, mwendawazimu na msafiri si wajibu kwao kufunga. Mtu haruhusiwi kuacha kufunga kutokana na udhaifu isipokuwa kama udhaifu huo utakuwa mkubwa kiasi cha kumuathiri na kwa hali hiyo atalipa baada ya mwezi wa Ramadhani. Na kwa hivyo mabinti ambao wamekamilisha miaka tisa ya kalenda ya mwezi wanawajibika kufunga, na wala hawaruhusiwi kuacha kufunga kwa kisingizio tu cha ugumu au udhaifu wa kimwili na mfano wake. Lakini ikiwa funga itakuwa na madhara kwao au tabu kubwa basi wataruhusiwa kutofunga. Haiwi sahihi kwa mtu ambaye anadaiwa swaumu ya wajibu kufunga swaumu ya mustahabu.

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Maswali

1. Nini maana ya swaumu?
2. Taja swaumu za wajib
3. Nini wajibu wa mtu aliyekatazwa kufunga kwa ajili ya maradhi?
4. Taja masharti ya wajibu katika swaumu.
5. Binti aliyefikia taklif ana hukmu gani ikiwa hana uwezo wa kufunga?
6. Je, ni sahihi kufunga swaumu ya mustahab wakati mtu anao wajibu wa kufunga swaumu ya wajib?

Changamoto

Je, ni sahihi kufunga bila kula daku?

Swaumu

Somo la Hamsini na Tisa

SWAUMU (2)

Nia ya swaumu

1. Maana na ulazima wa nia

Swaumu kama ibada nyingine zote zina lazima ya kuwa na nia kwa maana ya kuwa kutekeleza wajibu huo wa kujizuia kwa muda maalum ili kutimiza amri za Allah (swt). Si lazima kuitamka (nia) kwa ulimi.

2. Wakati wa kuweka nia

Kwa swaumu za mustahab

Ni tangu mwanzo wa usiku hadi kubaki muda mchache kufikia magharibi.

Kwa swaumu za wajib (kama mwezi wa Ramadhan)

Nia inakuwa sahihi hadi kabla ya kuingia kwa alfajiri

Na kama itafika kabla ya adhuhuri na hakuweka nia kwa makusudi nia yake haitakuwa sahihi.

Ikifika kabla ya muda wa adhuhuri na alisahau kuweka nia kwa ihtiyat atanuia na kufunga na baadaye atalipa qadhaa.

Kama itafika baada ya muda wa adhuhuri haitatosheleza nia yake.


Kwa swaumu za wajib ambazo si za mwezi wa Ramadhan (mfano wa qadhaa ya mwezi wa Ramadhan n.k.)

Hadi kabla ya adhuhuri akinuwia nia yake itakuwa sahihi.

Hadi baada ya adhuhuri kama hajanuia nia yake haitakuwa sahihi.

Ni vizuri nia ikawekwa hata kabla ya kuingia kwa alfajiri.

Mtu akiweka nia mwanzo wa usiku kwa swaumu ya kesho na akapitiwa na usingizi na akawa hakuweza kuamka wakati wa alfajiri swaumu yake itakuwa sahihi.



Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Mtu asiyeweka nia kwa makusudi hadi kufikia mchana wa mwezi wa Ramadhani atakuwa hana swaumu lakini atatakiwa kujizuia kwa siku hiyo na atalipa baada ya mwezi wa Ramadhani. Kama mtu alighafilika na hakuweka nia na akagundua katikati ya mchana hali ya kuwa ameshafanya jambo linalovunja swaumu, swaumu yake itakuwa batili lakini atatakiwa kujizuia kwa siku hiyo. Na kama alikuwa hajafanya jambo linalovunja swaumu, ikiwa aligundua baada ya adhuhuri swaumu yake ni batili na kama ni kabla ya adhuhuri kwa ihtiyat wajib atatia nia na atatakiwa kulipa siku hiyo baada ya mwezi wa Ramadhani.

Nia ya swaumu ya mustahab inaweza kuwekwa wakati wowote ikiwa hadi wakati huo mtu hajafanya jambo linalovunja swaumu.

Mtu akifunga swaumu ya mustahabu hali ya kuwa ana qadhaa ya swaumu ya wajib swaumu yake haitachukua nafasi ya qadhaa yake.

Mgonjwa akipata nafuu ndani ya mchana wa Mwezi wa Ramadhani hana wajibu wa kufunga siku hiyo lakini kama ni kabla ya muda wa adhuhuri na ikawa hadi muda huo hajafanya jambo linalovunja swaumu, kwa ihtiyat mustahab anaweza kuweka nia na kufunga na atalipa siku hiyo baada ya Mwezi wa Ramadhani.

3. Nia ya siku ya shaka. (yaumu shakk)

Siku ambayo inawekewa shaka kuwa ni mwisho wa mwezi Shabani au mwanzo wa Mwezi wa Ramadhani si wajibu kufunga, lakini kama mtu atafunga atalazimika kuweka nia ya mustahab au qadhaa, na baadaye ikithibiti kuwa ni mwanzo wa mwezi wa Ramadhani swaumu yake itahesabiwa kuwa ni ya Mwezi wa Ramadhani na hatadaiwa qadhaa.

4. Kuendelea kwa nia

Katika swaumu ni wajibu nia iwe yenye kuendelea.

Swaumu

Mambo yanayoharibu nia ni kama

Kunulia kukata swaumu

Swaumu itabatilika hata kama atanuia tena na kunuia huko hakutasaidia kitu.

Kuwa na shaka juu ya kuendelea na swaumu

Kwa ihtiyat ataendelea na swaumu na atailipa siku hiyo baada ya mwezi wa Ramadhani.

Kutaka kufanya jambo linalovunja swaumu

Kwa ihtiyat ataendelea na swaumu na atalipa siku hiyo baada ya mwezi wa Ramadhani.

Katika swaumu isiyo ya mwezi wa Ramadhani yawezekana kama mtu alitaka kuvunja swaumu ikiwa hatafanya yanayobatilisha swaumu na kabla ya muda wa adhuhuri (au kwa swaumu ya mustahab kabla ya magharibi) akanuia kuendelea na swaumu, swaumu yake itakuwa sahihi.

Maswali

1. Mtu akinuia kisha akapitiwa na usingizi, Je, ataweza kufunga siku hiyo?
2. Ni wakati gani unakuwa mwisho wa kuweka nia ya swaumu ya mustahab?
3. Mtu akifunga mustahab bila kujua kama ana qadhaa akigundua baadae Je, swaumu yake ya qadhaa itahesabika?
4. Bainisha hukmu ya yaumu (siku) shaka.
5. Mtu akinuia kubatilisha swaumu yake ya mwezi wa Ramadhani, lakini akabatilisha nia yake kabla ya kufanya jambo linalovunja swaumu, ni ipi hukmu yake?

Changamoto

Elezea hukmu ya binti ambaye amefikia balegh baada ya alfajiri ya siku ya swaumu.

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Somo la Sitini

SWAUMU (3)

Vinavyobatilisha Swaumu (1)

5. Vitu vinavyobatilisha swaumu ni kama

a. Kula na kunywa.

Hakuna tatizo Iwapo atatumia vidonge vya kutibu shinikizo la damu kwa dharura wakati wa swaumu. Lakini swaumu itabatilika (yaani kutumia vidonge huchukuliwa sawa na kula).

b. Jimaa (kukutana mume na mke kimwili).

c. Istimnaa (kujitoa manii).

d. Kusema uongo dhidi ya Mwenyezi Mungu (na maasumin kwa ihtiyat wajib)

e. Kufikisha vumbi zito hadi kooni (kwa ihtiya wajib)

f. Kuzamisha kichwa kizima ndani ya maji (kwa ihtiyat wajib)

g. Kubaki katika hali ya hedhi nifasi na janaba bila kuoga hadi kuchomoza jalfajiri.

h. Kuingiza kitu chenye umajimaji kwa kutumia sindano au bomba. Jambo hili linabatilisha swaumu hata kama litafanywa kwa ajili ya tiba. Hakuna madhara ya kubatilika swaumu kutokana na matumizi ya dawa maalumu zinazotumika katika tiba ya baadhi ya maradhi ya wananawake ambazo huingizwa ndani.

i. Kujitapisha kwa makusudi.

a. Kula na kunywa

Mtu aliyefunga akila au kunywa kwa makusudi swaumu yake inabatilika, iwe ni kitu kinacholiwa kwa kawaida au kisicholiwa, kiasi kidogo au kingi. Mtu aliyefunga akimeza kwa kukusudia kitu kilichobaki katika meno swaumu yake itabatilika, endapo kama hakujua kuwapo kwa kitu katika

Swaumu

meno au hakumeza kwa makusudi swaumu yake itakuwa ni sahihi. Swaumu haibatiliki kwa kula au kunywa kwa kusahau. Kumeza mate hakuharibu swaumu.

Kwa ihtiyaat wajib mtu anayefunga anatakiwa kujizuia na udungaji wa sindano za kuzidisha nguvu, lakini dawa zinazochomwa kwenye misuli hazina mushkeli. Kama mtu alikuwa anakula na akigundua kuwa asubuhi tayari imeshaingia anatakiwa kutema tonge lililopo mdomoni na kama akilimeza swaumu yake itabatilika.

Makohozi yanayoshuka toka puani moja kwa moja hadi kooni hayabatilishi swaumu ikiwa hayakufika kinywani.

Damu itokayo katika fizi ikiwa itachanganyika na mate haitakuwa najisi na yawezekana kuimeza bila kuharibu swaumu.

b. Jimaa (tendo la ndoa)

Jimaa inabatilisha swaumu hata kama manii hayakutoka. Kama mtu amesahau kuwa amefunga na akafanya jimaa, swaumu yake haitabatilika, ila wakati wowote akigundua kuwa yumo katika swaumu anachotakiwa ni kuacha hali hiyo haraka na kama akiendelea swaumu yake itabatilika.

c. Istimnaa (kujitoe manii)

Mtu akifanya jambo lolote mwenyewe na jambo hilo likasababisha manii kutoka swaumu yake itakuwa batili.

Kutokwa na manii usingizini (ihtilam) mchana wa mwezi wa Ramadhani hakubatilishi swaumu, hata kama mfungaji akijua kuwa akilala atatokwa na manii hana ulazima ya kujizuia na usingizi.

d. Kusema uongo juu ya Allah (s.w.t) na Maasumin

Kusema uongo juu ya Allah (s.w.t) na Mitume na Maasumin kwa ihtiyat wajib kunabatilisha swaumu hata kama baadaye atatubu na kusema kuwa

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

nilisema uongo.

Hakuna shaka kunakili hadithi zilizo katika vitabu vya hadithi ikiwa mtu hajui kuwa hadithi hiyo ni uongo au la ingawa kwa mujibu wa ihtiyaat mustahab anatakiwa kuzinukuu kwa kuzihusisha na kitabu husika, (kwa mfano aseme: imepokelewa katika kitabu fulani kuwa Mtume s.a.w. amesema kadhaa....)

e. Kufikisha vumbi zito hadi kooni

Mtu aliyefunga hatakiwi kufikisha vumbi zito kooni ila kuingia mdomoni au puani kwa vumbi zito hakubatilishi swaumu. Kuvuta moshi wa sigara na misokoto mingine kwa ihtiyat wajib kunabatilisha swaumu.

Mtu anayesumbuliwa na kubanwa na pumzi, na anahitaji kutumia dawa ambayo iko katika hali ya vumbi au gesi ili aweze kupumua vizuri, swaumu yake itakuwa na mashaka lakini kama haiwezekani bila kutumia hiyo dawa basi atatumia bila kufanya jambo lingine lolote linalovunja swaumu na kisha kama kuna uwezekano aliye siku hizo bila kutumia dawa hiyo.

Maswali

1. Nini maana ya vinavyobatilisha swaumu?
2. Nini hukmu ya kuchoma sindano katika hali ya swaumu?
3. Je, vidonge vya mapigo ya moyo vinaweza kutumika bila kuharibu swaumu ya mfungaji?
4. Je, inajuzu swaumu ya mtu ambaye amefanya ihtilam? (ametokwa na manii akiwa usingizini)
5. Kunakili hadithi katika hali ya swaumu kuna hukmu gani?
6. Nini hukmu ya kutumia sigara na misokoto mingine katika hali ya swaumu?

Changamoto

Mtu aliye katika hali ya swaumu anaruhusiwa kutafuna bazoka (chewing gum)?

Swaumu

Somo la Sitini na Moja

SWAUMU (4)

Vinavyobatilisha swaumu (2)

6. Kuzamisha kichwa kizima ndani ya maji

Mfungaji akizamisha kichwa kizima ndani ya maji, iwe pamoja na mwili au kichwa peke yake kwa ihtiyat wajib swaumu yake itakuwa batili na itamlazimu kulipa swaumu hiyo.

Kuzamisha kichwa upande mmoja na kukitoa kisha kuzamisha upande wa pili hakubatilishi swaumu.

Kama mtu ana shaka juu ya kuzama kwa kichwa chote au hapana swaumu yake itabatilika.

Kama mtu ambaye ameangukia ndani ya maji na kichwa chake kikazama swaumu yake haitabatilika ila itamlazimu kwa haraka kukitoa kichwa majini.

Mavazi ya kuzamia majini kwa ihtiyat hayaondoi ubatili wa kuzamisha kichwa ndani ya maji na kwa ihtiyat atalazimika kulipa qadhaa.

Kumwagia maji kichwani kwa kutumia chombo hakubatilishi swaumu.

7. Kubaki katika hali ya hedhi, janaba, na nifasi hadi asubuhi

Mtu akipatwa na janaba usiku wa mwezi wa Ramadhani anatakiwa kabla ya alfajiri ajitwaharishe na kama atabaki kwa makusudi hadi asubuhi swaumu yake itakuwa batili kwa siku hiyo. Ni hivyo hivyo ikiwa mtu anafunga qadhaa ya mwezi wa Ramadhani. Ama kwa swaumu za mustahabu swala hili halivunji swaumu.

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Iwapo mtu katika mwezi wa Ramadhan amefanya ghusli ya janaba kwa kutumia maji yaliyonajisika bila kujua, kisha baada ya siku kadhaa aka-gundua hali hiyo, swaumu yake haitobatilika bali itakuwa sahihi.

Kama mtu amefunga siku kadhaa hali ya kuwa ana janaba swaumu zake zitakuwa batili na hata kama hajui kuwa na janaba kunabatilisha swaumu anatakiwa kulipa idadi ya siku alizofunga akiwa na janaba.

Mtu aliye na wajibu wa kujitwahaisha usiku wa mwezi wa Ramadhani kama atapata dharura atawajibikiwa na tayammam badala ya ghusli.

Mtu akisha kujitwahaisha kabla ya alfajri swaumu yake itakuwa sahihi hata kama atatokwa na manii baada ya asubuhi bila ya hiyari yake.

Kama mtu akiwa usingizini akapatwa na janaba (akatokwa na manii) hata kama ni baada ya asubuhi swaumu yake itakuwa sahihi ila atalazimika kuoga kwa ajili ya swala na inawezekana akachelewesha muda wa kuoga hadi uingie wakati wa swala.

Kama mtu alipatwa na janaba usiku na akajua kuwa ikiwa atalala hataweza kupata muda wa kujitwahaisha, haitajuzu kwake kulala bila ya kujitwahaisha na ikiwa atalala na ikamkuta asubuhi swaumu yake ya siku hiyo itakuwa batili. Lakini kama alijua ataamka na akalala kwa nia ya kujitwahaisha baada ya kuamka ikamkuta asubuhi swaumu yake ni sahihi, isipokuwa tu kama atalala tena na ikiwa muda mchache umebaki kabla ya alfajiri hadi asubuhi, hapo atawajibikiwa na qadhaa ya siku hiyo na kwa ihtiyat mustahab atawajibikiwa na kafara pia.

Mwanamke ambaye alitakiwa kujitwahaisha kutokana na hedhi au nifasi ikiwa atabaki katika hali hiyo hadi asubuhi atawajibikiwa na qadhaa.

Mwanamke aliyefunga ikiwa ataona damu ya hedhi au nifasi katikati ya siku, swaumu yake itakuwa batili hata kama ulibaki muda mchache kuingia magharibi.

Swaumu

8. Imala. (kujiingiza kwa kitu cha maji maji kwenye utupu wa nyuma)

Kufanya imala kwa kitu cha majimaji hata kama ni kwa dharura au mati-babu swaumu inabatilika.

9. Kujitapisha kwa makusudi

Mtu aliyefunga ikiwa atatapika makusudi hata kama ni kwa maradhi swaumu yake itabatilika, lakini kama alitapika bila kukusudia swaumu itabaki kuwa ni sahihi.

Kama mtu alicheua na kitu kikafika hadi mdomoni anatakiwa kukitema ila kama atakimeza bila ya hiyari yake swaumu yake itakuwa sahihi.

Nukta muhimu kuhusiana na vinavyobatilisha swaumu

Mtu aliyefunga ikiwa atafanya moja kati ya yanayobatilisha swaumu kwa makusudi swaumu yake itabatilika, na kama haikuwa kwa makusudi au akalishwa kitu kwa kulazimishwa swaumu yake itakuwa sahihi, na hakuna tofauti kati ya swaumu ya wajibu na swaumu ya mustahab.

Ikiwa mtu alilazimika kula chakula kwa mikono yake ili asidhuriwe na wengine swaumu yake itakuwa batili.

Shaka katika ufanyaji wa yanayovunja swaumu haibatilishi swaumu.

Maswali

1. Nini hukmu ya mtu aliyezamia ndani ya maji akiwa na mavazi maalum?
2. Nini hukmu ya mtu aliyejimwagia maji kichwani kwa chombo?
3. Je, inajuzu mtu aliye na janaba akajitwahaarisha baada ya kuchomoza jua na akafunga swaumu ya qadhaa au swaumu ya mustahab?
4. Mtu akitokwa na manii na akawa hakuoga kwa lengo la kuoga kabla ya kuchomoza jua nini hukmu yake ikiwa atapitiwa na usingizi hadi

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

kuchomoza jua?

5. Nini hukmu ya kutapika katika mwezi wa Ramadhani?

6. Imala ni nini?

Changamoto

Nini hukmu ya mtu aliyesahau kuwa amefunga na akafanya ghusli ya irti-mas?

Swaumu

Somo la Sitini na Mbili.

SWAUMU (5)

Kafara ya kufungua kwa makusudi katika mwezi wa Ramadhani.

a. Wajibu wa kafara na aina zake

Ikiwa ndani ya mwezi wa Ramadhani mtu atafanya jambo linalobatilisha swaumu kwa makusudi bila kuwa na udhuru wa kisheria, itamlazimu kuilipa siku hiyo na ni juu yake atoe kafara. Hali hiyo itamuwajibikia iwe alikuwa anajua wajibu wa kafara wakati akivunja swaumu au hakujua.

Ikiwa mtu alidhani kuwa swaumu si wajibu juu yake na kwa hiyo hakufunga mwezi wa Ramadhani, kisha baadaye akagundua kuwa swaumu ilikuwa ni wajibu juu yake, itamuwajibikia juu yake kulipa qadhaa na kutoa kafara pamoja (kwa kuwa dhana tu ya kutokuwa na wajibu wa kufunga mwezi wa Ramadhani si sababu ya kuacha kufunga). Na ikiwa kufungua kwake kulitokana na hofu juu ya kupatwa na madhara, ikiwa hofu yake inakubalika kiakili, hatakuwa na kafara juu yake lakini itamuwajibikia kuilipa siku hiyo.

Ikiwa mtu alifanya mambo yanayobatilisha swaumu kwa hali ya kutojua hukmu za kisheria, kwa mfano hakujua ikiwa kuzamisha kichwa ndani ya maji kunabatilisha swaumu, swaumu yake itabatilika na atawajibikiwa kulipa, lakini hakuna kafara juu yake.

Kama mtu anajua uharamu wa kitendo fulani, lakini hajui kama kukifanya kunabatilisha swaumu, na akakifanya, itamuwajibikia qadhaa na kafara kwa ihtiyat wajib.

Ikiwa mtu amewajibikiwa kufungua kwa sababu maalum, kama vile kulazimishwa kufungua au kuzama katika maji kwa ajili ya kumuokoa mtu,

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

atawajibikiwa na qadhaa pekee bila ya kafara.

Ikiwa kitarejea chakula toka tumboni hadi mdomoni mwa mtu aliyefunga, haijuzu kukimeza tena, na kama akikimeza kwa makusudi atawajibikiwa qadhaa na kafara pamoja.

Ikiwa mtu amesikia habari ya kuingia usiku (wakati wa kufuturu) kutoka kwa mtu ambaye haaminiki na kutokana na habari hiyo mtu akafungua swaumu yake kisha akagundua kuwa muda haujafika atawajibikiwa qadhaa na kafara pamoja. Kama mtu amejamiiana na mkewe katika mchana wa mwezi wa Ramadhani, na ikawa mkewe alikuwa radhi na tendo hilo inawajibika kwa kila mmoja wao qadhaa na kafara.

b. Kiasi cha kafara na jinsi ya kutoa

Kafara ya kufungua kwa makusudi katika mwezi wa Ramadhani kwa sheria ya Kiislamu ni kutekeleza moja kati ya mambo matatu:

- i. Kumuacha huru mtumwa mmoja
- ii. Kufunga miezi miwili mfululizo
- iii. Kuwalisha masikini sitini.

Kwa kuwa katika zama za sasa hakuna watumwa basi mukallaf atakuwa na wajibu wa kuchagua ima kufunga au kulisha masikini pindi atakapo wajibikiwa na kafara.

Hakuna tofauti ya kafara kama mtu alifungua kwa kitu cha halali au haramu. Kwa mfano zinaa au kujitoa manii ingawa kwa ihtiyat mustahab ikiwa alifungua kwa kitu cha haramu atawajibikiwa kuchanganya kafara zote tatu.

Ikiwa mtu hawezi kufanya kafara kwa mambo haya matatu, basi ni juu yake kutoa sadaka kwa fukara kwa kiasi kile anachoweza, na ni ihtiyaat

Swaumu

afanye istighfari vile vile. Ama kama hakuweza kabisa kutoa sadaka kwa fukara, basi inamtosha kufanya istighfari kwa kusema moyoni na ulimini:

"Astaghfirullah wa Atuubu ilayhi"

(Namwomba Mwenyeezi Mungu anisamahe)

Mwenye kutaka kufunga miezi miwili mfululizo atatakiwa kufunga mwezi mmoja kamili na siku moja katika mwezi wa pili, kisha haitakuwa na shaka ikiwa ataachanisha katika mwezi wa pili. Akitaka mwanamke kufunga miezi miwili mfululizo kama atakutwa na hedhi katikati yake haitadhuru chochote, ataendelea na kufunga pindi amalizapo ada yake na haitakuwa na lazima kwake kurejea tena.

Kuwalisha masikini kuna njia mbili

- a. Kumpa chakula akashiba.
- b. Kumpa kibaba kimoja (3/4 ya kilo moja)

Mwenye kutaka kuwalisha masikini atawalisha kulingana na tulivyoona katika mas'ala yaliyotangulia, au kama ni kibaba kimoja (3/4 ya kilo), basi haijuzu kwa fakiri mmoja kupewa zaidi ya kiasi cha kisheria au pungufu, ingawa inajuzu kwa fakiri kupewa kulingana na idadi ya wanaomtegemea. Hakuna tofauti kwa fakiri kati ya mwanaume na mwanamke, mkubwa na mdogo.

c. Hukmu za kafara

Mfungaji akifanya yanayobatilisha swaumu zaidi ya mara moja kwa siku, ni juu yake kufanya kafara moja tu. Ikiwa kitendo hicho ni jimai au istimnai (kujitoa manii), kwa ihtiyat wajib, atarudia kafara kulingana na idadi ya tendo hilo. Kama mtu amefungua kwa makusudi kisha akasafiri wajibu wake wa kafara hautaondoka, au ameamka usiku hali ya kuwa ana janaba na analijua hilo, lakini hakufanya ghusli wala kutayammam kabla ya alfa-jiri, kisha akaweka nia ya kusafiri siku hiyo, kwa lengo la kukimbia swau-

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

mu na akasafiri siku hiyo mara tu baada ya adhana, nia yake ya kusafiri wala safari yake haitamuondolea wajibu wa kafara.

Anayewajibikiwa na kafara hana wajibu wa kuitekeleza kwa haraka, na hatakiwi kuichelewesha kiasi kwamba ule wajibu ukapotea. Ikiwa mtu amechelewesha kufanya kafara yake kwa miaka kadhaa hakuna kitu kitakachozidi katika wajibu wake. Si lazima kufuata taratibu katika kutekeleza qadhaa na kafara ya swaumu.

Maswali

1. Je, ikiwa mtu amefanya jambo ambalo anajua kuwa ni haramu lakini hajui kuwa linabatilisha swaumu, Je, itatosheleza kwake kulipa qadhaa tu ya siku zile?
2. Kama mke na mume walifanya jimaa ndani ya mchana wa mwezi wa Ramadhani na mke alikuwa radhi na hilo, nini hukmu yake?
3. Bainisha kiwango cha kafara kwa mtu aliyefungua kwa makusudi katika mwezi wa Ramadhani.
4. Nini hukmu ya mtu ambaye alifungua kwa tendo la haramu au istimnaa mwezi wa Ramadhani?
5. Je, ana wajibu gani mtu ambaye katika mwezi wa Ramadhani kwa siku moja akafanya zaidi ya mara moja matendo ambayo yanavunja swaumu?
6. Je, kuna ongezeko la kiasi gani katika kafara ya wajibu ikiwa utapita muda mrefu?

Changamoto

Kama mtu amewekwa kama wakili kuwalisha baadhi ya masikini, Je, anaweza kuchukua katika chakula kile na mali aliyopewa kwa ajili ya kafara kama ujira wa upishi?

Swaumu

Somo la Sitini na Tatu

SWAUMU (6)

Kafara ya kufungua qadhaa ya Ramadhani

- a. Mtu anayefunga kwa nia ya kulipa mwezi wa Ramadhani haijuzu kwake kuibatilisha fungu hiyo baada ya kupita muda wa adhuhuri, na kama aki-fanya hivyo kwa makusudi atawajibikiwa na kafara.

Mtu huyo anaweza kufungua siku hiyo kabla ya kuingia adhuhuri kwa sharti kwamba muda wa kulipa bado upo, (mfano anadaiwa siku tano na zimebaki siku tano kuingia mwezi wa Ramadhani nyingine kwa sura hii haruhusiwi kufungua iwe kabla au baada ya adhuhuri kwa ihtiyat wajib, ingawa akifungua kabla ya adhuhuri hatakuwa na kafara.

Kama mtu ameajiriwa kulipa qadhaa ya mtu ikiwa atafunga baada ya kupinduka jua hatawajibikiwa na kafara.

b. Kiwango cha kafara

Kafara ya qadhaa ya mwezi wa Ramadhani ni kuwalisha mafakiri kumi, kama hataweza basi atafunga siku tatu.

Kafara ya kuchelewesha

- a. Wajibu wake na hukmu zake.

Ikiwa mtu hakulipa qadhaa ya mwezi wa Ramadhani hadi ukaingia mwezi wa Ramadhani nyingine bila ya udhuru atatakiwa alipe qadhaa hiyo na kisha atoe kafara kwa kila siku moja, lakini kama ana udhuru ulioendelea ambao unamfanya kutofunga, kwa sura hiyo atalipa qadhaa bila kafara, (ingawa kwa ihtiyat mustahabu atoe kafara). Kuhusu maradhi tutatoa maelezo baadaye.

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Kutokujua hukmu pia hakufuti wajibu wa kafara katika kuchelewesha kulipa qadhaa ya mwezi wa Ramadhani.

Kafara ya kuchelewesha kulipa qadhaa ya mwezi wa Ramadhani hutolewa mara moja tu hata kama imepita miaka kadhaa, wala hawajibiki kuikariri kafara hiyo kwa mujibu wa idadi ya miaka.

b. Kiwango cha kafara

Kafara ya kuchelewesha qadhaa ni kutoa kibaba kimoja kwa fakiri, na pia inawezekana kutoa zaidi ya kibaba kimoja (3/4 ya kilo) kwa fakiri mmoja kulingana na idadi ya qadhaa.

Fidia

Watu wanaostahili kutoa fidia kwa kila siku ya mwezi wa Ramadhani ni:-

- a. Wazee ambao inakuwa vigumu kwao kufunga
- b. Mtu aliye na maradhi ya kiu, ambaye kufunga kwake inakuwa ni vigumu.
- c. Mjamzito anayekaribia kujifungua ikiwa funga ina madhara kwa ujauzito wake. Baada ya kutoa fidia atalipa qadhaa ya funga zake baada ya kuondokewa na udhuru huo.
- d. Mama anayenyonyesha ambaye akifunga atapungukiwa na maziwa na mtoto atadhurika
- e. Mgonjwa ambaye ugonjwa wake umeendelea hadi mwezi wa Ramadhani mwingine, hatawajibikiwa na kulipa qadhaa ya swaumu yake lakini atatoa fidia tu kwa kila siku aliyoiacha kufunga. Ikiwa mgonjwa huyo ni mwanamke wajibu wa fidia hautakuwa juu ya mumewe bali ni juu yake mwenyewe.

Swaumu

Kiwango cha fidia

Kiwango cha fidia ni sawa na kiwango cha kafara ya kuchelewesha kulipa qadhaa ya mwezi wa Ramadhani (yaani atatoa kibaba kimoja (3/4 ya kilo) kwa masikini).

Mtu aliyeweka nadhiri ya kufunga siku maalum, ikiwa siku hiyo hakufunga kwa kukusudia au alibatilisha swaumu yake atawajibikiwa na kafara.

Kafara ya nadhiri ni sawa na kafara ya kiapo ambayo tutaizungumzia mahala pengine.

Maswali

1. Taja kiwango cha kafara ya qadhaa ya Ramadhani na wakati gani hutolewa.
2. Taja kiwango cha kafara ya kuchelewesha kulipa qadhaa na wakati gani hutolewa kafara hiyo.
3. Je, kafara ya kuchelewesha qadhaa inamuwajibikia hata yule ambaye hakuwa na elimu na mas-ala hayo?
4. Ni watu gani huwajibikiwa kutoa fidia?
5. Nani anawajibikiwa na kafara ya mwanamke ambaye kutokana na maradhi alichelewa kulipa qadhaa ya Ramadhani hadi kukutana na swaumu nyingine?
6. Mwanamke akishindwa kufunga kwa miaka miwili kutokana na ujauzito nini hukmu yake kwa sasa ambapo anao uwezo wa kufunga?

Changamoto

Je, yawezekana kutoa pesa badala ya kafara au fidia ya swaumu?

Mafunzo ya Hukmu za Ibada)

Somo la Sitini na Nne

SWAUMU (7)

Sehemu zinazowajibikiwa na qadhaa bila ya kafara

Mtu ambaye hakuweka nia ya kufunga katika mwezi wa Ramadhani au alifunga kwa riya, hata kama hakufanya jambo linalovunja swaumu, atawajibikiwa na qadhaa ya siku hiyo, lakini hatawajibikiwa na kafara.

Mtu aliyesahau kuoga janaba siku ya mwezi wa Ramadhani na akafunga katika hali hiyo kwa idadi kadhaa ya siku atawajibikiwa na qadhaa ya siku hizo.

Ikiwa mtu alifanya jambo linalovunja swaumu katika wakati ambao hakuhakikisha kuwa wakati huo ilikuwa ni alfajiri au hapana, ikiwa ilishaingia alfajiri atawajibikiwa na qadhaa. Na kama alihakikisha kuwa alfajiri haijaingia na baada ya kufanya moja katika yanayobatilisha (swaumu) akabaini kuwa ni alfajiri, basi hatawajibikiwa na qadhaa ya siku hiyo.

Ikiwa kwa sababu ya giza mtu akadhani kuwa magharibi imeingia au akapata habari za kuingia kwa magharibi kutoka kwa mtu anayeaminika kwa hali hiyo akafungua kisha akabaini kuwa magharibi ilikuwa bado haijaingia, itamlazimu kulipa qadhaa ya siku hiyo.

Ikiwa kutokana na wingu ikadhaniwa kuwa magharibi imeingia na mtu akavunja swaumu yake, kisha ikabainika kuwa haikuwa magharibi, hatawajibikiwa na qadhaa ya siku hiyo.

Kabla ya kuyakinisha kuingia kwa alfajiri mtu anaweza kufanya jambo linalobatilisha swaumu, lakini ikiwa baadaye itabainika kuwa ilishaingia alfajiri, atalipa qadhaa ya siku hiyo.

Swaumu

Kabla mtu hajayakinisha kuingia kwa magharibi hataweza kuvunja swaumu yake, na ikiwa atavunja kisha akagundua magharibi haijaingia atawajibikiwa na qadhaa, lakini kama kulikuwa na kizuizi kama wingu kwa hali hiyo hatawajibikiwa na qadhaa.

Ikiwa wakati wa kutawadha mtu aliyefunga akaingiza maji mdomoni kama sunna ya wudhu na maji hayo yakapitiliza bila kutarajia, swaumu yake itakuwa sahihi na hatawajibikiwa na qadhaa. Lakini kama alitia maji mdomoni kwa lengo la kuondoa ukavu kwa sura hiyo maji yakipitiliza atawajibikiwa na qadhaa.

Hukmu za qadhaa ya swaumu

Mtu aliyepoteza fahamu kwa siku kadhaa hawajibikiwi na qadhaa ya swaumu za siku alizokuwa hana fahamu.

Ikiwa mtu alipitwa na swaumu kutokana na ulevi, anawajibikiwa kulipa siku hizo alizoacha kufunga. Kwa mfano alikosa kuweka nia ya swaumu kwa sababu ya ulevi wake.

Ikiwa mtu aliweka nia ya kufunga kisha akalewa, kisha akabakia katika ulevi mchana kutwa au sehemu fulani ya mchana akawa katika hali ya ulevi, inakuwa ihtiyaat wajib akamilishe swaumu halafu atailipa siku hiyo.

Mwanamke akiacha kufunga katika ada yake ya kila mwezi au kwa sababu ya uzazi atawajibikiwa na qadhaa baada ya mwezi wa Ramadhani.

Kama mtu aliacha kufunga kwa siku kadhaa kutokana na udhuru lakini kwa sasa hana kumbukumbu ya idadi ya siku alizoziacha, basi atalipa kiasi kidogo cha siku anazokisia lakini ni vyema kama atalipa kwa idadi kubwa ya siku anazokisia.

Mafunzo ya Hukmu za Ibada)

Kama mtu anadaiwa zaidi ya mwezi mmoja wa Ramadhani hakuna ulazi-ma wa kutanguliza kulipa deni la mwanzo, lakini kama muda uliobaki ni mchache kuingia Ramadhani nyingine, kwa hali hiyo atatanguliza kulipa mwezi wa Ramadhani ya mwisho anayodaiwa kwa ihtiyat wajib.

Mtu ambaye kutokana na ugonjwa hakuweza kufunga mwezi wa Ramadhani na ugonjwa huo ukaendelea hadi mwezi wa Ramadhani nyingine hatawajibikiwa na qadhaa, lakini kama baada ya ugonjwa alipatwa na udhuru mwingine ambao ulibaki hadi Ramadhani nyingine atawajibikiwa na qadhaa baada ya Ramadhani. Hali ni hiyo hiyo kwa udhuru usiokuwa maradhi.

Kutokuwa na uwezo wa kufunga au kulipa qadhaa hakuvunji wajibu wa swaumu.

Hukmu ya funga ya qadhaa ya wazazi

Ikiwa baba au mama hakufunga mwezi wa Ramadhani kutokana na udhuru au bila ya udhuru, na akawa baada ya mwezi wa Ramadhani hakulipa baada ya kufariki inakuwa wajibu kwa mtoto mkubwa wa kiume kulipa qadhaa za wazazi wake au kumwajiri mtu kuweza kuzilipa qadhaa hizo.

Hukmu za funga ya msafiri.

Mtu anayesafiri katika mwezi wa Ramadhani ikiwa amefikia sheria ya kupunguza swala, basi anatakiwa kutofunga katika siku hizo, na hukmu zake zinaenda sambamba na hukmu za swala ya msafiri.

Mtu aliyefunga akisafiri baada ya adhuhuri, anawajibikiwa kukamilisha swaumu yake ya siku hiyo. Ama akisafiri kabla ya adhuhuri swaumu yake itabatilika, isipokuwa hatakuwa na ruhusa ya kula kitu hadi atakapofika katika mpaka unaoruhusu kupunguza swala. Na akifungua kabla ya kufika hapo kwa ihtiyat wajib atawajibikiwa na kafara.

Swaumu

Ikiwa msafiri ataingia katika mji wake kabla ya adhuhuri au akaingia sehemu ambayo ana nia ya kubaki hapo kwa siku kumi, na ikawa hajafanya jambo ambalo linavunja swaumu, atakamilisha swaumu yake na kama alishafanya katika yanayobatilisha swaumu atawajibikiwa na qadhaa. Inajuzu kusafiri katika mwezi wa Ramadhani hata kama ni kwa lengo la kukwepa swaumu, lakini ni bora kama mtu akajizuia na safari isipokuwa tu kama safari hiyo ni muhimu au ni ya lazima.

Msafiri mwenye nia ya kufanya itikafu katika msikiti mtukufu wa Makka ikiwa ana lengo la kukaa siku kumi katika mji wa Makka au akaweka nadhiri ya kufunga akiwa safarini, atawajibikiwa kukamilisha itikafu yake katika siku ya tatu ya swaumu yake. Ama kama hakuweka nia ya kukaa siku kumi au hakuweka nadhiri ya kufunga safarini, funga yake haitaswihi akiwa safarini, na kwa kuwa swaumu haitaswihi basi pia itikafu yake haitaswihi.

Maswali

1. Je, mtu aliyefunga akiweka maji mdomoni na yakapitiliza bila kukusudia atabatilisha swaumu yake?
2. Mtu anayedaiwa qadhaa ya Ramadhani zaidi ya moja atalipa vipi qadhaa zake?
3. Bainisha binti aliyetimiza miaka tisa na akawajibikiwa na swaumu ila kutokana na woga hakufunga swaumu hiyo, Je, atawajibikiwa na qadhaa.
4. Elezea hukmu ya qadhaa ya swaumu ya wazazi.
5. Kama mtu alikuwa na uhakika wa kuwasili safari yake kabla ya wakati wa adhuhuri isipokuwa kutokana na hatari za safari akachelewa hukmu ya swaumu yake itakuwaje?
6. Je, inajuzu kusafiri safari za kawaida katika mwezi wa Ramadhani?

Changamoto

Mtu akifa Je, inakua wajibu wa nani kulipa qadhaa zake?

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Somo la Sitini na Tano

SWAUMU (8)

Njia za kuthibiti mwezi

- a. Kuonwa na mtu mukallaf
- b. Ushahidi wa watu wawili waadilifu
- c. Kuenea kwa habari zinazothibitisha kuonekana kwa mwezi.
- d. Kukamilika kwa siku thalathini za mwezi uliotangulia.
- e. Maamuzi ya hakimu wa sheria.


Kipimo cha kuutambua mwezi mwandamo ni mwezi unaozama baada ya kuzama kwa jua, na huweza kuonekana hata kabla ya kuzama jua. Kwa hali hiyo mwezi unaozama kabla ya kuzama kwa jua au ukazama sambamba na jua hautoshelezi kuwa ni uthibitisho wa kuwa ni mwezi mwandamo.

Hakuna tofauti kati ya kuuona mwezi kwa chombo maalum au kuuona kwa kawaida.

Ukubwa au udogo wa mwezi, unene au wembamba wake kuwa chini au juu hakuthibitishi kuwa ni siku ya kwanza ya mwezi au ya pili. Maneno ya wanajimu katika kalenda hayathibitishi mwandamo wa mwezi.

Ikiwa mwandamo wa mwezi umeonekana katika mji inatosheleza pia kwa miji iliyo karibu, na hata ile miji ya mbali inayoshirikiana mawio na machweo.

Mtu atakayeona mwandamo wa mwezi na akajua kuwa hakimu wa sharia hataweza kuuona, si wajibu kumpa habari hakimu huyo ila kama kufanya hivyo kutaleta ufigadi.



Swaumu

Ikiwa hakimu atatoa hukmu ya kuwa kesho ni Idi, na hukmu hii ikawahusu watu wa nchi nzima, basi hukmu hii itahusu miji yote ya nchi hizo.

Katika kutangaza mwandamo wa mwezi kunakofanyika na moja ya nchi, si lazima kuwa nchi hiyo ni nchi ya Kiislamu, lakini muhimu katika hili ni kule kuthibitika kwa mwandamo wa mwezi katika sehemu anayoishi mukallaf.

Ikiwa katika mji hakukuonekana mwandamo wa mwezi lakini vyombo vya habari vikatangaza habari hiyo, kwa kuwa habari hiyo imethibitishwa na waliyul faqiih haitakuwa na haja ya kufanya uhakiki.


Ikiwa mwezi mwandamo haujathibiti kwa njia ya kuuona hata katika sehemu zilizo na ukanda mmoja au haukutolewa ushahidi na watu wawili waadilifu au hakim wa sheria hakutoa hukmu, italazimu kufanya ihtiyat katika kuthibitisha.

Kama haikuthibiti mwandamo wa mwezi haitakuwa wajibu kufunga kwa siku hiyo, lakini baadaye ikithibiti kuwa siku hiyo ilikuwa mwanzo wa mwezi italazimika kufunga qadhaa.

Siku ambayo inatiliwa shaka kuwa ni mwisho wa mwezi wa Ramadhani au mwanzo mwezi wa Shawwaal lazima kufunga kwa siku hiyo, lakini ikiwa katikati ya siku ikathibiti kuwa ni mwanzo wa Shawwaal italazimu kukatiza swaumu hata kama imekaribia magharibi.

17. Mas'ala mbalimbali kuhusiana na swaumu

Sehemu ambazo watu wanashughulika kwa wingi katika mwezi wa Ramadhani kusoma dua, Qur' an pamoja na munajaat mbalimbali inajuzu kwa sehemu hizo kurusha shughuli hiyo kwa sauti ya juu, isipokuwa tu kama sauti hiyo itakuwa ni adha (usumbufu) kwa walio karibu, na kwa hali hiyo haitajuzu kufanya hivyo.



Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Funga ya mustahab haina uwajibu wa kuikamilisha hadi mwisho wake, bali anaweza kuikatiza wakati wowote. Yawezekana mtu aliyefunga suna akakatiza swaumu yake kutokana na mwaliko wa chakula wa ndugu yake Mwislamu, (tendo hilo japo linabatilisha swaumu lakini halitaharibu thawabu za swaumu).

Maswali

1. Taja njia za kuthibitisha mwandamo wa mwezi.
2. Kuwa katika ukanda mmoja kuna maana gani?
3. Inatosheleza kukubali kuonekana kwa mwezi kwa kuzingatia maneno ya hakim?
4. Siku ya shaka kati ya mwisho wa Ramadhani au mwanzo wa Shawwaal ina hukmu gani?
5. Nini hukmu ya kusoma dua za kila siku za mwezi wa Ramadhani ikiwa kuna shaka katika kuswihi kwake?
6. Kama mtu alishakamilisha swaumu kisha baada ya kufuturu akasafiri katika sehemu ambayo bado magharibi haijaingia, itakuwaje hukmu ya swaumu yake ya siku hiyo?




Changamoto

Kama maulamaa wawili ambao uadilifu wao unathibiti kwa watu watakhitalafiana juu ya mwandamo wa mwezi kwa dalili ambazo zinakubalika, nini kifanyike?



Sehemu ya Tano

KHUMSI



Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Somo la Sitini na Sita

KHUMSI

1. Maana ya khumsi

Kilugha ina maana ya moja ya tano (1/5), na kwa istilaha ya sheria ni moja kati ya wajibu muhimu unaohusu mali katika Uislamu. Yaani, ni mali ambayo kila mtu aliyefikia masharti yake anatakiwa kuitoa kwa mpangilio makhsusi uliowekwa.

2. Wajibu wa khumsi

Wajibu wa khumsi ni moja katika dharura za dini na kuipinga dharura hii ikiwa itapelekea kuipinga Utume au kusababisha mapungufu katika sheria kutasababisha ukafiri na kutoka katika dini.

Kutoweza kutoa khumsi hakuondoi wajibu wa khumsi, kwa hiyo watu waliokuwa na wajib wa kutoa khumsi na hadi sasa hawajatoa khumsi hiyo na kwa sasa pia hawana uwezo wa kutoa inawalazimu kwa wakati wowote watakapopata uwezo watoe khumsi. Kadhalika wanaweza kulipa taratibu kulingana na muda na maelezo ya wakili mwenye dhima ya kukusanya khumsi. Haijuzu kuchelewesha kulipa khumsi hadi kuingia mwaka mwingine wa khumsi.

Kama mali inayomilikiwa na mtu ambaye hajafika balegh imetimia kiwango cha kuitolea khumsi, ni wajibu kwa msimamizi wa kisharia (walii) amtotee khumsi, ispokuwa faida inayopatikana kutokana na mali yake si wajibu kwa walii wake kumtolea khumsi, lakini itakuwa wajibu wa ihtiyat kwa mtoto mwenyewe kujitolea khumsi, baada ya kufikia balegh, ikiwa bado ipo.

3. Vitu vilivyo wajibu kutolewa khumsi ni

- a. Faida ya kazi au biashara.
- b. Madini.



Khums

- c. Mali halali iliyochanganyika na haram.
- d. Johari zinazopatikana kwa kuzamia ndani ya bahari.
- e. Ngawira za vita.
- f. Ardhi iliyonunuliwa na kafiri dhimmi kutoka kwa Waislamu.

4. Madhara ya kutotoa khums

Kutumia mali ambayo haikutolewa khums inakuwa na hukmu ya mali ya ghasbi (yaani ni haramu) lakini baada ya kutolewa idhini ya kutumia mali hiyo kutoka kwa kiongozi au wakala wa kukusanya khums.

Kwa hali hiyo mukallaf hawezi kutumia mali yake ikiwa hajatoa khums, na kama alitumia kiasi cha mali hiyo kwa biashara kiwango ambacho kilis-tahili khums kitakuwa haram katika biashara, na lazima kilipiwe khums yake.

Ikiwa utafanyika muamala na watu ambao hawajishughulishi na kutoa khums au kula na kutumia katika mali yao, ikiwa kuna uyakini wa kuwapo khums katika mali zao ambayo ingepatikana katika kuuza au kununua kutoka kwao, kiasi cha muamala kitakuwa batili, na kutahitaji idhini ya msimamizi wa khums na wakili wake, na haitajuzu kutumia katika mali zao.

Kama mtu aliacha wosia wa kutolewa kiasi cha mali zake kwa khums au warithi wake wana yakini kwamba anadaiwa kiasi cha khums, haitajuzu kutumia katika mali ya marehemu mpaka itolewe khums iliyokusudiwa, ikiwa itatumika itaingia hukmu ya ghasbi.

Kuswali juu ya kitu ambacho kina uhusiano na mali ambayo haikutolewa khums ni batili. Lau mtu ataswali juu ya mswala au mavazi ambayo hayakutolewa khums kwa muda fulani, basi swala atakazoziswali zitakuwa batili, isipokuwa tu kama alikuwa hajui hukmu ya utoaji wa khums au utumiaji wa mali isiyotolewa khums.

Maswali

1. Je, kulipa kodi katika dola ya Kiislamu kunaondoa wajibu wa khumsi?
2. Je, ni ipi hukmu ya mtu ambaye alikuwa anadaiwa khumsi na kwa sasa hana uwezo wa kutoa?
3. Taja vitu vilivyo wajibu kutolewa khumsi.
4. Kama mtu hakufanya mahesabu yake ya nyuma na akianza kutoa khumsi kwa mahesabu ya sasa ana hukmu gani?
5. Nini hukmu ya muamala wa ardhi au mali kwa mali ambayo haikutolewa khumsi?
6. Je, inajuzu kuchukua mali ya mtu aliyeitoa kwa ajili ya msikiti hali ya kuwa hajaitolea khumsi?

Changamoto

Kama mnunuzi anajua kuwa mali aliyonunua haikutolewa khumsi na muuzaji, Je, itajuzu kwake kutumia mali hiyo?

Khumsii inayotokana na faida

Somo la Sitini na Saba

KHUMSI INAYOTOKANA NA FAIDA

Kwa kila mtu aliyetimiza masharti (ya kutoa khumsii) ni wajibu juu yake kutoa khumsii ya faida inayozidi katika matumizi yake.

1. Maana ya Faida

Maana ya faida kwa hapa ni ile mali au chumo linalopatikana kutokana na kazi za kichumi ambalo hujulikana kama kipato kinachoingia ndani ya kazi hizo.

2. Aina za faida

- a. Faida itokanayo na kilimo.
- b. Faida itokanayo na biashara.
- c. Faida itokanayo na umiliki wa kitu kwa njia ya kukodisha vitu kama vile nyumba, gari na mfano wa vitu kama hivyo. Au faida inayopatikana kutokana na kukodisha vifaa vya kutengenezea madini, au mashine ya kutengeneza soksi nk.
- d. Faida ya mshahara anayoichukua mtu kutokana na ajira ikiwemo mshahara wa mwalimu kwa ajili ya kusomesha, au mshahara wa mhandisi kutokana na kazi zake za kitaalamu, au mshahara anaouchukua mtu kwa kazi zake za kawaida. Vile vile kila ujira anaouchukua mtu kutoka kwa wengine kutokana na juhudi za mwili wake kuzitumikisha chini ya watu hao.

3. Mfano wa vitu ambavyo havina faida ndani yake ni

Urithi

Mali ya urithi au fedha zipatikanazo kutokana na kuuzwa kwa mali ya urithi hazina khumsii, hata kama iliwekwa na (hatimaye) thamani yake kuongezeka lakini kama kuwekwa kwake ilikuwa ni kwa lengo la

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

kuongezeka thamani, kwa sura hiyo urithi huo unatolewa khumsi.

Urithi anaopata mtoto mdogo hauna khumsi, lakini faida ipatikanayo kutokana na urithi tangu muda huo hadi muda ambao mtoto huyo atafikia balegh, itatakiwa kutolewa khumsi.

Mahari

Mahari haina khumsi iwe ni fedha au mali.

Zawadi

Zawadi haina khumsi lakini kwa ihtiyat wajib ikiwa zawadi hiyo inazidi matumizi ya mwaka basi itatolewa khumsi. Kubainika kwa zawadi kunategemea lengo la mtoaji. Basi matumizi ambayo hupatikana kutoka kwa wazazi au jamaa wengine, yanakuwa na hukmu ya zawadi kulingana na lengo la mtoaji.

Vitu vitolewavyo na wazazi au jamaa havina khumsi hata kama vitu hivyo vilihitajiwa na mpewaji au havilingani na hadhi ya mpewaji. Na kama zawadi ya vitu hivyo havilingani na hadhi ya mtoaji, havitahesabika kuwa katika matumizi na vitahitaji khumsi.

Zawadi atowayo mume kumpatia mkewe hata kama ana lengo la kuitumia baadaye na ikawa ina thamani ambayo inalingana na hadhi ya mtoaji na kuwa utoaji huo haukuwa kwa kukwepa khumsi zawadi hiyo inakuwa haina khumsi. Kutoa kwa lengo la kukwepa khumsi kuna khumsi ndani yake.

Pesa ipatikanayo kwa kuuza zawadi haina khumsi, isipokuwa kama zawadi hiyo iliwekwa kwa lengo la kuongezeka thamani yake, Kwa hali hiyo thamani iliyozidi inahitajia kutolewa khumsi.

Zawadi ya wafanyakazi kutoka katika sehemu zao za kazi haina khumsi lakini kama ilikuwa nusu ya zawadi ilinunuliwa kwa pesa ya mfanyakazi

Khumsii inayotokana na faida

mwenyewe (aliuza kitu kwa nusu ya thamani ya asili na nusu nyingine kama zawadi) kwa hali hiyo ikipinduka mwaka ile nusu iliyotolewa pesa itatolewa kumsii.

Waqf

Mali ya waqfu haina khumsii hata kama itazidi thamani yake maradufu. Pesa wapatiwazo wasomi wa dini wanaosoma katika hauza za kidini hazina khumsii.

Pesa za msaada kwa wanafunzi wa vyuo vikuu hazina khumsii lakini kama mwanafunzi huyo ataidhinishwa kupata mshahara kwa hali hiyo mshahara wake utatakiwa kuutolea khumsii.

Mali ambayo tayari ilishatolewa khumsii mara moja haina tena hukmu ya khumsii hata ikipita miaka kadhaa bila kutumika.

Bima itolewayo ili kulipa khasara iliyopatikana kutokana na janga fulani haina hukmu ya khumsii.

Mkopo

Mali iliyokopwa haina khumsii.

Maswali

1. Nini lengo la mapato katika khumsii ya mapato?
2. Nini hukmu ya khumsii katika mirathi?
3. Je, zawadi ina hukmu ya khumsii?
4. Nini hukmu ya zawadi zitolewazo na mabengi kuhusiana na khumsii?
5. Nini hukmu ya bima katika khumsii?
6. Mke na mume wakipeana zawadi katika mali ambayo haikutolewa khumsii kuna hukmu gani katika hilo?

Changamoto

Kama mtu hayupo kwa muda mrefu na pesa yake inawekwa benki, na kama angekuwapo angeitumia pesa hiyo, nini hukmu yake katika khumsii?

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Somo la Sitini na Nane

KHUMSI YA FAIDA (1)

Kama tulivyokwisha tangulia kusema hapo mwanzo kuwa matumizi hayana khumsi.

4. Maana ya matumizi (ma' una)

Maana ya neno ma'una hapa ni matumizi ya mwaka mzima na siyo (mapato ya mwaka) ikiwa na maana ya kuwa yale matumizi ya kawaida yanayofanyika ili kujikimu kimaisha, kama kula, kuvaa, kusoma, sadaka na kila ambacho mtu anakihitaji ili kumuwezesha kuishi maisha yake.

5. Kiwango cha matumizi

Matumizi ya lazima ni matumizi ambayo kila mtu anayahitajia katika umuhimu wa kuishi kwake. Kwa hiyo kila ambacho kinanunuliwa si katika matumizi ya lazima hatuwezi kukiweka katika hesabu ya matumizi, mfano, vileo na kila aina ya haramu.

Matumizi ya mwaka katika khumsi matumizi hayaangaliwi kwa siku, wiki wala mwezi, bali huangaliwa mahitajio ya mtu kwa muda wa mwaka mzima katika maisha yake.

Kipimo katika matumizi: yaani matumizi ya mwaka yapatikane katika mwaka huo huo na siyo kabla yake au baada yake.

Kiwango cha matumizi: Yaani mtu anatakiwa kutumia kiasi ambacho ni cha kawaida, kwa maana ya kwamba asijinyime kiasi cha kushindwa kukamilisha yale mahitaji ya msingi na kwa wakati huo huo asifanye israfu katika manunuzi ya vitu visivyo na ulazima.

Khumsi ya faida

Mtu hatakiwi kujitaabisha katika kupunguza au kuongeza matumizi yake kinyume na hali ya kawaida. Kwa hali hiyo ikiwa atapunguza mapunguzo hayo hayatahesabiwa katika matumizi. (Yale ambayo alitakiwa kuyatayarisha kwa ajili ya matumizi ila kutokana na kujinyima hakuyahitajia.)

Mume akimnunulia mke wake dhahabu ambazo zinakubalika kijamii na zinaendana na hadhi ya mume itahesabika kuwa ni sehemu ya matumizi na hivyo kutokuwa na wajibu wa kutolewa khumsi.

Pesa anazotenga mtu kwa ajili ya kufanyia jambo la kheri au kuwasaidia waliokumbwa na majanga hazina hukmu ya khumsi.

6. Matumizi yasiyo ya lazima

Ina maana ya vitu ambavyo havina ulazima wa kutumika kwa sasa mfano mtu ambaye amenunua nyumba, lakini haitumii kwa kuwa anaishi katika nyumba ya shirika au serikali. Ikiwa aliinunua kwa mapato ya mwaka huo huo au kwa pesa iliyokwishatolewa khumsi, haitakuwa na khumsi.

Ikiwa ilipatikana kutokana na mali ambayo haikuitolea khumsi italazimu kutolewa khumsi. Ikiwa ameinunua kwa pesa ambayo haikutolewa khumsi italazimu kutolewa kwa khumsi ya matumizi au kutoa kwa thamani ya sasa iwapo thamani imeongezeka. Vitabu vilivyo maktaba binafsi kwa muda mrefu bila kutumika kama vilinunuliwa kwa lengo la kusomwa au vilitolewa zawadi kwa lengo hilo havina hukmu ya khumsi.

7. Thamani ya kuuza kitu cha matumizi au faida inayopatikana kutokana na kuongezeka kwa thamani

Tumeeleza katika matumizi ambayo hayana lazima yanasimama pia katika hukmu ya uuzaji wa mali na faida, kwa maana, kitu kilichopatikana katika pesa ya matumizi ya mwaka au pesa ambayo imeshatolewa khumsi, na kisha kwa sababu maalum kikauzwa, pesa hiyo haitakuwa na khumsi.

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Maswali

1. Nini maana ya matumizi?
2. Kiwango cha matumizi ni kipi?
3. Nini hukmu ya dhahabu anayonunua mume kwa ajili ya mkewe?
4. Nini hukmu ya matumizi ya ziada?
5. Kama mtu ameuza nyumba kisha pesa ikawekwa benki ili kupata faida nini hukmu ya khums? Na je, kama anaweka pesa benki kidogo kidogo ili anunue nyumba, nini hukmu yake?
6. Kitu cha lazima ambacho hakikutolewa khums kikiuzwa, Je, khums yake inatakiwa kutolewa mara tu baada ya kuuza?

Changamoto

Kitu kilichonunuliwa kwa lengo la kutumika kisha baada ya miaka kadhaa kwa kuwa hakihitajiki tena kikauzwa ili kununua kitu kingine, Je, pesa hizo zitakuwa na hukmu ya khums?

Khumsu ya Matumizi

Somo la Sitini na Tisa

KHUMSI YA MATUMIZI

Mambo ambayo hayahusiani na matumizi

1. Mtaji

Mtaji upatikanao kutokana na kazi au mapato fulani (hata mshahara) unatahiki kutolewa khumsu.

Kama mtu amenunua kipande cha ardhi ili akiuze na kisha kwa pesa hiyo ajenge nyumba, anawajibikiwa kutoa khumsu katika pesa hiyo. Mtu akinunua au akijenga nyumba yenye tabaka tatu kwa ajili ya kupangisha baadhi ya tabaka zake ili aweze kupata matumizi yake ya maisha, atawajibikiwa kutoa khumsu kwa kiwango ambacho kilikuwa ndio mtaji.

Ardhi isiyotumika ikiwa baada ya kuihuisha kwa ajili ya kuwa shamba ili ndani yake apande miti itakayotoa matunda, inatakiwa kutolewa khumsu baada ya kutoa mahesabu yote ya kuhuisha ardhi hiyo.

Watu wafanyao kazi kwa ushirika kila mmoja anatakiwa kutoa khumsu kulingana na sehemu aliyochangia na ikiwa kazi ile italeta faida kila mmoja atatoa khumsu katika ziada hiyo kulingana na kiwango alichochochangia.

Haijuzu kutumia mali hiyo ya shirika kabla ya washiriki wote kutoa khumsu katika hisa zao. Baada ya washiriki wote kutoa khumsu kulingana na hisa zao ushirika hautakuwa na jukumu la khumsu ya pamoja.

Sehemu ya kufanyia biashara ni katika mtaji wa mtu na anatakiwa kuitolea khumsu, na kama haikuwezekana kulipa kwa mara moja anaweza kutaka

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

idhini kwa msimamizi wa khumsi au wakili wake ili atoe taratibu. Bidhaa ambayo imeongezeka thamani na kuna watu wa kuinunua katikati ya mwaka lakini (mmiliki) akawa hakuiuza kwa makusudi ili ifikie wakati wa kuongezeka kwa thamani yake, ukiingia wakati wa kutoa khumsi atatakiwa aitolee khumsi kwa thamani iliyoongezeka.

2. Chombo cha kufanyia kazi

Chombo cha kufanyia kazi kina hukmu ya mtaji na kama kimenunuliwa kutokana na mapato yaliyopatikana kitakuwa na hukmu ya khumsi. Kwa hiyo, gari atakalolilnunua kwa ajili ya kufanyia kazi zinazofungamana na kazi yake na chumo lake ni wajibu kulitolea khumsi.

Ikiwa mtu amenunua bidhaa kutokana na pesa iliyotolewa khumsi, atakapoiuza mali hiyo kwa kiasi cha juu thamani inayozidi itakuwa ni ziada ya matumizi itakayotakiwa kutolewa khumsi.

3. Akiba

Akiba inayowekwa hata kwa ajili ya maisha ya kawaida inatakiwa kutolewa khumsi, isipokuwa kama akiba hiyo itatumika kwa kitu cha lazima kama mas'ala ya ndoa, ununuzi wa kitu ambacho ni dharura kwa matumizi katika muda mchache tu baada ya kuingia wakati wa kutolewa khumsi, basi akiba hiyo haitatolewa khumsi.

4. Malipo ya kustaafu

Pesa zilipwazo baada ya kustaafu zinatakiwa kutolewa khumsi ikiwa zitazidi katika matumizi ya mwaka, na hakuna tofauti kati ya pesa hiyo kuwa inakatwa katika mshahara au inawekwa na mwajiri.

5. Sanda

Mtu aliyenunua sanda na ikakaa kwa muda mrefu anatakiwa kuitolea khumsi isipokuwa kama aliinunua kwa pesa iliyokwisha kutolewa khumsi.

Khumsii ya Matumizi

Maswali

1. Kama mmoja kati ya washirika hajatoa khumsii, nini hukmu yake?
2. Nini hukmu ya akiba katika khumsii?
3. Ipi hukmu ya chombo cha kufanyia kazi katika khumsii?
4. Je, mtaji unaoongezeka unatakiwa kutolewa khumsii?
5. Nini hukmu ya malipo ya kustaafu katika khumsii?
6. Je, ardhi iliyohuisha ina hukmu ya khumsii?

Changamoto

Nyumba ya urithi ambayo kwa sasa imepangishwa na pesa kugawanywa kwa warithi kila baada ya muda fulani, Je, ina hukmu gani katika khumsii?

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Somo la Sabini

KHUMSI YA FAIDA (2)

Mambo yenye hukmu ya matumizi

1. Mahitaji yasiyodumu

Mahitaji yanayotumika na kisha yasibakie baada ya kutumika kama vile sukari, mchele, samli na mfano wake miongoni mwa mahitaji ya kila siku yasiyobakia katika maisha.

Ikiwa vitu hivi vinanunuliwa kwa mwaka, basi vitakavyobakia baada ya mwaka vinatakiwa kutolewa khumsi. Ama mahitaji yanayotumika na yak-abakia, ni kama vile nyumba, gari, samani za ndani, mapambo ya wanawake, na vinginevyo. Ikiwa alivinunua kutokana na faida ili avitumie na anavihitajia, mali kama hizi hazina hukmu ya khumsi.

2. Mahitaji yanayonunuliwa taratibu

Baadhi ya vitu ni dharura kwa mwanadamu lakini upatikanaji wake ni kwa kukusanya pesa kidogo kidogo mfano nyumba, gari na mfano kama huo, basi pesa hizo hazitakuwa na hukmu ya khumsi.

Mtu asiyemiliki nyumba ya kuishi kisha akanunua ardhi ili ajenge nyumba kutokana na faida ya mwaka, baada ya kuanza kujenga na kabla ya kukamilisha jengo ukapita mwaka unaostahiki kulipa khumsi na ikawa hakutoa kwa ajili ya jengo hilo, basi haitakuwa na khumsi juu yake.

Maswali

1. Kwa nini matumizi hayana khumsi?
2. Nini tofauti kati ya mahitaji ya polepole na ya haraka?
3. Nini hukmu ya kiwanja ambacho hakikujengwa kwa muda mrefu kutokana na kutokuwa na uwezo wa kifedha katika hukmu ya khumsi?
4. Nini hukmu ya kiwanja kinachouzwa ili kujenga nyumba nyingine?
5. Nini hukmu ya mali za kudumu katika khumsi?
6. Taja mambo ambayo yanahesabika kuwa ni katika matumizi.

Changamoto

Vitu ambavyo havitumiki kwa muda mrefu vitakuwa na hukmu gani katika khumsi.

Khumsu ya Mapato

Somo la Sabini na Moja

KHUMSI YA MAPATO (1)

Jinsi ya kuhesabu khumsu ya mapato na jinsi ya ulipaji wake.

a. Kuthibiti kwa khumsu katika mapato

Khumsu katika mapato husika lazima yatolewe katika mapato yenyewe, na kabla khumsu haijatolewa mmiliki haijuzu kwake bila idhini ya mmiliki wa khumsu kutumia katika mapato hayo iwe kwa kula, kunywa, au kutoa kwa njia yoyote.

b. Muda wa kutoa khumsu

Muda wa kutoa khumsu ni tangu pale mtu alipopata mapato hayo hadi muda wa mwaka mmoja. Kwa hiyo mmiliki ana ijaza (ruhusa) ya kutoa khumsu muda wowote kabla ya kumalizika mwaka.

c. Khiyari katika kulipa khumsu katika mapato au thamani yake

Mmiliki ana hiyari ya kulipa katika mapato yenyewe au katika thamani ya mapato hayo, mfano mtu anatakiwa kutoa khumsu ya nyumba au kiwanja, ikiwa atataka kutoa thamani ya kiwango chake itabidi mali hiyo aitolee khumsu ikiwa ni katika faida ya mali ile.

Kila kitumikacho ndani ya mwaka kwa ajili ya kufanikisha utendaji wa kazi na hatimaye kupata faida, hakuna wajibu wa khumsu ndani yake. Kwa mfano, usafiri, ubebaji, upakuaji, wafanyakazi, dalali na hata kodi ya mahala pa kufanyia kazi au biashara.

d. Kutokuwapo kwa khumsu ya mapato katika matumizi

Khumsu ya mapato haiingii katika matumizi yaani kila ambacho kinatumika kama dharura katika maisha hakina hukmu ya khumsu, lakini kile tu kili-

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

chozidi baada ya mwaka ndio kinawajibikiwa kutolewa khumsi. Matumizi ya mwaka hupatikana katika mapato ya mwaka huo huo.

Uhalali wa kutumia matumizi pamoja na mali nyingine

Mtu anaweza kutumia matumizi pamoja na mali nyingine kwa wakati mmoja ikiwa mali hiyo ilishatolewa khumsi. Kwa hiyo baada ya mwaka kila kitakachobakia katika matumizi kitatolewa khumsi na kile kilichotoka katika mali nyingine hakina hukmu ya kutolewa khumsi kwa kuwa kilishatolewa khumsi.

e. Kuwa na hesabu za mwaka wa khumsi

Mtu anayepata kipato hata kama ni kidogo anatakiwa kuwa na mahesabu ya kila mwaka ya mapato yake ili ajue jinsi ya kutoa khumsi.

Na hii inakuwa kwa mtu ambaye anajua kuwa ana wajibu wa kutoa khumsi lakini hajui anatakiwa kutoa kiasi gani. Kama mtu anajua kuwa hana wajibu wa kutoa khumsi, yaani mapato yake yanamtosheleza matumizi tu, hatakuwa na wajibu wa kutoa khumsi.

Mke na mume ambao kila mmoja ana kipato chake hata kama wanashirikiana katika matumizi ya nyumbani, kila mmoja atatoa khumsi kulingana na ziada ya matumizi yake.

Mtu anaweza kujihesabia mwenyewe kiwango anachotakiwa kutoa khumsi na kisha akapeleka kwa mkusanyaji wa khumsi.

Kupanga mwanzo wa kulipa khumsi

Kuanza wakati wa kulipa khumsi si jambo linalopangwa na mukallaf bali hujitokeza kutokana na mwanzo wa kukusanya mapato yapatikanayo kama ni mshahara, faida ya biashara, na hata mazao. Kutoa khumsi yawezekana kwa kutegemea mwaka wa mwezi mwandamo au mwaka wa miladiyya.

Khumsu ya Mapato

Maswali

1. Je, inajuzu kuwahisha au kuchelewesha kutolewa kwa khumsu?
2. Mtu anaruhusiwa kutoa khumsu ya nyumba au shamba katika mapato yake ya mwaka?
3. Pesa ambayo imeshatolewa khumsu kwa mwaka uliopita kisha ikaongezeka, Je, kwa mwaka ujao kiasi gani kitakachotolewa khumsu (kile kilichoongezeka pekee au na kile cha mwanzo)?
4. Kijana ambaye anamilikiwa na wazazi wake ana wajibu wa kutoa khumsu?
5. Mtu anaweza kuhesabu mwenyewe kiasi cha kutoa khumsu?
6. Vipi mtu ataanza kutoa khumsu?

Changamoto

Yawezekana kutoa khumsu ya kitu kingine kutokana na mali nyingine?

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Somo la Sabini na Mbili

KHUMSI YA MAPATO (2)

Jinsi ya kuhesabu khumsi ya mapato na ulipaji wake

1. Jinsi ya kuhesabu khumsi ya mtaji na ulipaji wake

Katika kuhesabu khumsi ya mtaji, kwanza lazima kuhesabiwe kila kili-chopo katika mali na pesa, na kutolewa khumsi yake, kisha katika mwaka ujao kitalinganishwa jumla ya mali hiyo na rasilimali asilia. Basi ikiwa kutakuwa na kilichozidi kitatakiwa kutolewa khumsi, na kama hakuna kili-cho ongezeko basi hakutakuwa na khumsi ya ziada.

2. Shaka katika kuhesabu khumsi ya mapato

Mtu akiwa na shaka juu ya hesabu ya mwaka uliopita ya khumsi anatakiwa kutoijali shaka hiyo, lakini kama ana shaka katika mapato kuwa yalichanganyika na ya mwaka uliopita ambayo yalishatolewa khumsi au ni ya mwaka ambao bado khumsi yake haijatolewa, kwa hali hiyo atatakiwa mtu huyo kwa ihtiyat atoe khumsi ya mapato aliyokuwa nayo.

3. Shaka katika kutoa khumsi

Vipi Mtu akiwa na shaka kama alitoe khumsi au hakutoa? Basi ikiwa anachokiwekea shaka ni miongoni mwa vitu ambavyo vinapaswa kutolewa khumsi, basi ni wajibu juu yake kupata yakini kwamba alitoe khumsi.

4. Maelewano

Kama mtu anajua kuwa mapato yake yanawajibikiwa na khumsi ila hajui matumizi aliyofanya yalikuwa yamefanyika wakati gani, katika hali kama hiyo, mtu huyo atatakiwa kurejea kwa mkusanyaji wa khumsi ili kupata ufumbuzi wa suala hili. (Hii ni kwa wakati tu ambao mtu ana shaka).

Khumsi ya Mapato

5. Kupata ufumbuzi

Mtu ambaye ana wajibu wa kutoa khumsi lakini kwa sasa hana uwezo wa kutoa itamlazimu kupata ufumbuzi juu ya khumsi iliyoko katika dhimma yake kwa msimamizi wa khumsi au mwakilishi wake kisha (watapanga naye) namna ya kutoa khumsi kidogo kidogo kwa mujibu wa uwezo wake na muda wa kulipa.

Maswali

1. Elezea jinsi ya kuhesabu khumsi ya mtaji
2. Nini hukmu ya kuchanganya mtaji na mali ambayo ni zawadi?
3. Nini wajibu wa mtu anayekuwa na shaka juu ya mali aliyokwishatolea khumsi?
4. Wasafiri waliokwama njiani wana wajibu gani katika khumsi?
5. Maelewano katika khumsi yanafanyika wakati gani?
6. Je, khumsi yaweza kulipwa kupitia benki?

Changamoto

Nyumba iliyonunuliwa kwa kukusanya pesa miaka kadhaa itatolewa vipi khumsi?

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Somo la Sabini na Tatu

KHUMSI YA MADINI

1. Khumsi ya madini

Madini yaliyochimbwa na mtu au kundi la watu yana hukmu ya khumsi kwa sharti kuwa kiwango chake baada ya kutoa gharama yote ya kutoa na kusafishia kibakie kiasi cha dinari ishirini za dhahabu au dirhamu mia mbili za fedha. Madini yanayochimbwa na serikali hayana hukmu ya khumsi.

2. Dafina

Hazina ipatikanayo katika sehemu ambayo inamilikiwa na watu inatakiwa kutolea khumsi ila kama jambo hili litatokea katika nchi ya Kiislamu inayofuata sheria za Kiislamu italazimu kufuata utaratibu uliopangwa kulingana na sheria za serikali ya Kiislamu.

3. Mali ya halali iliyochanganywa na haramu

Kama kuna yakini katika mali ya halali kuchanganyika na mali ya haramu ambayo haijulikani mmiliki wake wala kiasi chake italazimika kuihalalisha kwa kutolea khumsi.

4. Matumizi ya khumsi

a. Khumsi inatumika katika njia mbili

- i. Sehemu ya Imam (a.s) ambapo ni Imam yeyote anayekuwapo katika zama hizo ambapo kwa sasa katika zama hizi ni Imam Mahdi (a.t.f.s), na sehemu ya masayyid yaani masharifu. Na hawa masayyid ni wale ambao nasaba yao kwa upande wa baba inakutana na Mtume kama watoto wa Imam Ali (A.S) Aqil na Abbas.

Khumsu ya Madini

ii. Sehemu ya Imam kwa sasa ambapo yuko ghaib inasimamiwa na kiongozi mkuu wa Waislamu kwa matumizi mbali mbali ya Uislamu na jamii, kama vile kuendeshea mashule ya kidini. Na haijuzu kwa mtu asiyestahiki kutumia sehemu ya Imam wala sehemu ya Masharifu.

b. Watu wanaoruhusiwa kutumia sehemu ya Masharifu (sayyid)

Awe ni Sayyid.

Awe muumini kwa maana ya Shia Ithnaashariyya.

Awe fakiri; sayyid anayejiweza hana ijaza ya kupewa khumsu, isipokuwa kama atakuwa na haja ya lazima anaweza kupatiwa khumsu kutimiza haja zake.

Asiwe ni mtu anayemuwajibikia kumlisha.

Asiwe ni mtu atakayeitumia katika maasi.

Asiwe ni mwenye kudhihirisha maasi ya wazi wazi.

5. Mas'ala mbali mbali yanayohusu khumsu

Inajuzu kutumia mali ambayo hakuna uhakika kama ilitolewa khumsu au haikutolewa.

Maswali

1. Ni kipi kiwango cha kutoa khumsu ya madini?
2. Nini hukmu ya mtu anayeishi katika familia ya watu wasiotoa khumsu?
3. Khumsu inatumika katika njia ngapi?
4. Sayyid anayejiweza Je, anaruhusiwa kuchukua sehemu ya masayyid katika khumsu?
5. Mke ambaye ni sayyida akiwa fakiri, Je, anaruhusiwa kutumia sehemu ya Imam pamoja na mume wake ambaye ni fakiri lakini si sayyid?
6. Masayyid ni kina nani?




Changamoto

Je, inajuzu kwa mtu kutumia khumsu katika kazi ya kheri bila ruhusa ya kiongozi wa Waislamu?



Sehemu ya Sita

NGAWIRA



Ngawira

Somo la Sabini na Nne

NGAWIRA

1. Maana ya ngawira

Ni mali zinazokuwa mikononi mwa Mtume (s.a.w.w) na Maasumina (as) na katika zama za ghaiba zinakuwa katika umiliki wa kiongozi wa Waislamu, yaani chini ya mamlaka ya serikali ya Kiislamu. Ni jambo la wajibu kwa ajili ya manufaa ya jamii kwa ujumla

2. Njia za kupatikana kwa ngawira



- a. Fay'u: Nayo ni mali ipatikanayo bila vita iwe ardhi au mali nyingine
- b. Ardhi zisizotumika ambazo haziwezi kutumika mpaka zihuishwe.
- c. Miji na vijiji vilivyotelekezwa.
- d. Fukwe za bahari na mito mikubwa
- e. Mali za watu waliokufa na hawana warithi
- f. Madini.

Maswali

1. Nini maana ya ngawira?
2. Kwa njia gani hupatikana ngawira?
3. Je, inajuzu kwa mtu kumiliki fukwe za bahari?
4. Msimamizi wa ngawira ana ijaza ya kuzikodisha? na Je, pesa ipatikanayo itumike vipi?
5. Faini ni nini?
6. Nini hukmu ya mtu atakayetumia pesa ya anfal kwa matumizi binafsi?


Changamoto

Ubinafsishaji wa anfal (ngawira) unaofanywa na dola au serikali unatakiwa kupata ruhusa ya wananchi?



Sehemu ya Saba

JIHAD



Jihad

Somo la Sabini na Tano

JIHAD

1. Maana ya jihad

Maana ya jihad kwa hapa ni kupigana kwa ajili ya kuwalingania watu katika Uislamu na kupanua dola yake. Au ni kupambana dhidi ya maadui wa Uislamu.

2. Wajibu wake

Ni wajibu wa dharura katika dini kwani ni moja kati ya nguzo kuu za dini.

3. Aina zake

a. Jihad hatua za mwanzo

Jihad hufanyika kwa lengo la kuondoa vizuizi ambavyo vinafanya kurudisha nyuma utangazaji na uenezi wa Uislamu. Na jihad hii ilikuwa zama za Mtume s.a.w.w na Maimamu (as) na hata kiongozi wa Waislamu ana ijaza ya kutoa amri ya jihad.

Ahlul Kitabu wanaoishi chini ya himaya ya Uislamu ikiwa hawajafanya jambo linalovunja amani ya Uislamu wanatakiwa kulindwa mali zao pamoja na heshima yao. Washirikina wakivamia nchi ya Kiislamu na baadhi yao kuwa mateka, hukmu ya mateka hao inakuwa juu ya kiongozi wa Waislamu na hakuna Mwislamu yoyote atakayekuwa na haki ya kumiliki mateka.

b. Jihad ya kujilinda

Hii ni jihad ifanyikayo kwa lengo la kuzuia wavamizi wanaotaka kuingia katika nchi ya Kiislamu na kuwatawala kijeshi, kisiasa, ama kiuchumi.

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Maswali

1. Nini maana ya jihad?
2. Elezea aina za jihad
3. Nini lengo la jihad ya mwanzo (ibtidai)?
4. Kiongozi wa Waislamu ana ijaza (ruhusa) ya kuamrisha jihad ya mwanzo katika zama za ghaiba?
5. Mwislamu anaweza kumiliki mateka waliovamia ardhi ya Waislamu?
6. Jihad ya ulinzi ni jihad gani?

Changamoto

Ikiwa kuulinda Uislamu sahihi hakuwezekani ila kwa kumwaga damu ya mtu muhtaram nini hukmu yake?

Sehemu ya Nane

*KUAMRISHA
MEMA NA
KUKATAZA
MAOVU*

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Somo la Sabini na Sita

KUAMRISHA MEMA NA KUKATAZA MAOVU (1)

1. Maana yake

Ni kuwaamrisha watu kufanya mambo mema na kuwakataza kufanya mambo maovu.

2. Wajibu wa kuamrisha mema na kukataza maovu

Kuamrisha mema na kukataza maovu, ni moja kati ya wajibu muhimu katika dini ya Kiislamu na wale wanaoacha kutekeleza wajibu huu muhimu au hawaoni umuhimu wake huhesabika kuwa ni watenda dhambi, na watapata adhabu kali inayowangojea. Na hii siyo tu ni wajibu kwa mujibu wa maafikiano ya wanachuoni bali jambo hili ni katika dharura za dini tukufu ya Kiislamu.

Jambo hili la kuamrisha na kukataza kwa kuzingatiwa sheria zake ni jukumu la kijamii kwa lengo la kuuhifadhi na kuulinda Uislamu pamoja na kuleta amani katika jamii.

Kudhania kwamba kazi hii inaweza kuleta dhana mbaya kwa dini ya Kiislamu, ni jambo ambalo haliwajibishi kupuuza wajibu huu muhimu sana. Kwa hiyo lau mtu atauona ukiukwaji wa kanuni katika moja ya ofisi za umma ukiwemo udanganyifu, basi ni wajibu juu yake kuukataza uovu huo pamoja na kuchunga masharti ya sheria.

Na haijuzu kushikamana na njia nyingine yoyote ile, kama vile rushwa katika utekelezaji wa kazi yoyote ile hata kama ni kwa lengo la kuzuia kutokea kwa ufisadi.

Ikiwa masharti ya kukataza mema na kuamrisha maovu hayakukamilika, basi hatakuwa na ulazima wa kutenda jambo hili.

Kuamrisha mema na kukataza maovu

Kwa mfano kama mtu anahofia kuwa kutekeleza kwake amri hii kutamletea madhara itamlazimu kunyamaza, lakini haya ni katika dola ambazo si za Kiislamu. Sehemu inayotawaliwa na dola ya Kiislamu ikiwa mtu amegundua ufisadi na hawezi kuuondoa itamlazimu kutoa taarifa kwa vyombo vya dola ambavyo vitachukua hatua husika katika kuondoa ufisadi huo.

Uovu ni uovu hauna tofauti, kwa hiyo sharti la kuondoa uovu linasimama mahala popote na bila kujali tofauti ya ukubwa wa uovu mmoja na mwingine.

Kama kuna wafanyakazi wasio Waislamu wanaokuja kufanya kazi katika nchi za Kiislamu ni wajibu kwa viongozi wa nchi hiyo kuwaelimisha na kuwakataza kufanya wazi wazi baadhi ya mambo ambayo ni haramu katika Uislamu, kama ulaji na unywaji wa haramu.

Vijana wanatakiwa kuwa mstari wa mbele katika jukumu hili la kuamrisha mema na kukataza maovu hasa katika sehemu za mkusanyiko wa vijana wengi kama vyo vikiu ambapo vijana wengi hujishughulisha na ufisadi.

3. Kiwango cha kuamrisha mema na kukataza maovu

Kuamrisha mema na kukataza maovu hakukomei kwenye kundi tu la watu fulani, bali ni jukumu la kila mmoja hata wanawake na watoto ikiwa watashuhudia kuachwa kwa mema na kufanywa kwa maovu kwa baba zao, mama zao au waume zao lazima watekeleze wajibu huu kwa kuzingatia masharti yaliyopo.

4. Masharti ya kuamrisha mema na kukataza maovu

a. Kuwa na elimu ya mema na maovu

Sharti la kwanza la kuamrisha na kukataza ni kwa mtu kuwa na elimu juu ya mema na maovu. Kinyume na hayo hatakuwa na wajibu wa kuamrisha mema wala kukataza maovu. Kwani, kutokana na ujinga, mtu anaweza

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

kuamrisha maovu na kukataza mema.

b. Kuwepo na athari

Anayeamrisha mema na kukataza maovu lazima awe na matumaini ya kuwa maamrisho au makatazo yake yanaweza kuleta athari japo kwa siku za baadaye. Na ikiwa mtu amekatazwa asifanye maovu na haikuleta athari yoyote italazimu ikiwezekana kumzuia hata baadhi ya mambo hali ya kuwa anaelezwa kuwa kuzuiwa kwake jambo fulani ni kwa kutokubali kwake kuacha maovu au kutofanya mema.

c. Kuendelea katika madhambi

Mtu muovu anayekatazwa asifanye maovu lazima awe amebobea katika uovu na ikiwa itaonekana kwamba mtu huyo japo kwa kufanya dhambi anaweza kuacha maovu na kufanya mema bila ya kuamrishwa, haitakuwa wajibu kufanyiwa maamrisho au makatazo.

d. Kutotokea uharibifu

Kuamrisha au kukataza kusiwe na uharibifu ndani yake. Hii ina maana kwamba ikiwa maamrisho na makatazo yatamsababishia uharibifu muamrishaji au mkatazaji au Waislamu wengine kama kupata madhara au kupoteza heshima na mali zao, kwa hali hii haitakuwa wajibu kuamrisha wala kukataza, lakini katika hili lazima kutathminiwa kwa uovu na kuamrisha na kukataza ufiisadi utakaopatikana ikiwa hakutaamrishwa wala kukatazawa kisha itaangaliwa lile ambalo ni muhimu.

Mtu kama ana hofu ikiwa ataamrisha au kukataza kwa mtu ambaye ana nafasi katika jamii yatamkuta madhara, haitakuwa wajibu kwake kuamrisha na kukataza, kwa sharti kwamba woga wake unakubalika kiakili, lakini si vizuri kuacha kuamrisha mema au kukataza maovu kwa kudhania tu madhara yake au kwa kuogopa nafasi ya mtu katika jamii, kwa kila hali ni lazima kuzingatia umuhimu wa jambo.

Kuamrisha mema na kukataza maovu

Nukta muhimu kuhusu kuamrisha mema na kukataza maovu

- a. Kuamrisha mema na kukataza maovu kunakuwa wajibu pale masharti haya manne yanapokamilika. Kupungua kwa moja ya sharti kutapelekea wajibu wa kuamrisha mema na kukataza maovu kuondoka.
- b. Si wajibu katika kuamrisha mema na kukataza maovu kwa muamrisha-ji au mkatazaji kuwa ni mfanyaji wa jambo hilo, yaani hata mfanya madhambi ana wajibu wa kuamrisha mema, na hawezi kujivua na wajibu huu kwa kuwa anafanya madhambi.
- c. Katika kuamrisha mema na kukataza maovu si sharti kuwa kuamrisha kule au kukataza kuvunje hadhi au heshima ya aliyeacha mema au anayefanya maovu.

Maswali

1. Nini maana ya *amri bil maaruf* na *nahyi anil munkar*?
2. Nini hukmu ya mtu anayefanya maovu hali ya kuwa alishaonywa kuacha kufanya maovu.
3. Je, mujarrad (ambaye hajaoa au kuolewa) anaruhusiwa kufanya *amri bi maaruf* na *nahyi anil munkar*?
4. Taja masharti ya kuamrisha mema na kukataza maovu.
5. Kukataza maovu kwa mtu ambaye haujui kuwa anafanya haramu kuna hukmu gani?
6. Kama kuamrisha mema au kukataza maovu kotalazimu kuvunja heshima ya anayeamrisha au kukatazwa nini hukmu yake?

Changamoto

Tufanye nini kwa watu ambao mara kwa mara wanaamrisha kufanya mema na kuacha maovu lakini hawaathiriki?

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

Somo la Sabini na Saba

KUAMRISHA MEMA NA KUKATAZA MAOVU (2)

5. Hatua za kuamrisha mema na kukataza maovu.

Ni wajibu kuzingatia hatua katika kuamrisha mema na kukataza maovu . Hii ina maana kwamba haiwezekani kuanza na kiwango cha juu hali ya kuwa kiwango cha chini kingetosheleza kuleta athari.

a. Kuamrisha na kukataza kwa moyo

Hatua ya kwanza ya kuamrisha mema na kukataza maovu ni kutumia moyo. Na kutumia moyo maana yake ni kudhihirisha kwa moyo kuridhika au kuchukizwa na jambo fulani, kiasi cha hali hiyo kuweza kugunduliwa na mfanyaji maovu au mtenda mema.

Njia ya kutumia moyo ina sehemu nyingi ambazo ikiwa kwa kiasi kidogo kitaleta athari, haijuzu kwenda sehemu ya juu. Kwa mfano kutomchekea, kumkunjia uso, kuuma mdomo, kumpa mgongo, kutomtolea salamu, na kutokuwa na mahusiano naye.

b. Kuamrisha na kukataza kwa ulimi

Hatua ya pili ya kuamrisha mema na kukataza maovu ni kutumia ulimi. Na maana yake ni kutumia njia ya kuzungumza ili muhusika aweze kutambua kwa jema alilofanya au ovu alilotenda. Kuzungumza pia kunatakiwa kuanzia daraja ya chini ya upole na siyo kuanza na daraja ya juu ya ukali.

Yawezekana mtu akaambiwa kwa upole, kama kupewa nasaha kumuone-sha faida na hasara za matendo yake, kumuonya, na hatimaye hata kumueleza kwa vitisho.

Kuamrisha mema na kukataza maovu

c. Kuamrisha na kukataza kwa vitendo

Hatua ya tatu ya kuamrisha mema na kukataza maovu ni kwa njia ya vitendo, nako ni kutumia nguvu ya ziada kumuamrisha mtu kufanya mema au kumzuwia kufanya maovu. Nayo pia lazima ianzwe kwa kitendo cha chini kabisa kama hakutakuwa na ulazima wa kuchukua hatua kali zaidi.

Kwa mfano, kukamata mkono wake kwa nguvu, kumpokonya vitu anavyotumia, kumsukuma, kumuangusha, kumchapa, kumpiga, kumjeruhi, kumvunja, na hata kumuua.

Nukta muhimu juu ya tabaka za kuamrisha mema na kukataza maovu

- a. Kujibu salamu ya Mwislamu ni wajibu kisheria lakini ikiwa kutojibu salamu hiyo kutampelekea aliyefanya maovu azinduke kutokana na uovu wake itajuzu kutojibu salamu hiyo.
- b. Ikiwa mtu anasikiliza muziki ni wajibu kumkataza kwa kutumia njia yoyote itakayoleta manufaa.
- c. Haijuzu kwa mtu kuingia katika nyumba ya mwingine kinyume na sheria kwa lengo la kuamrisha mema na kukataza maovu.
- d. Kama mmoja katika jamaa anafanya maovu, itakuwa lazima kwa jamaa zake wafanye kila njia itakayowezekana ili kumfanya jamaa yao asien-delee kufanya maovu, lakini haijuzu kukata udugu naye, na kama kutengana naye kwa siku kadhaa kutamfanya aache maovu, basi italazimika kufanya hivyo.

Mas'ala mbalimbali kuhusiana na kuamrisha mema na kukataza maovu

Mtu ambaye siku za nyuma alikuwa akifanya haramu, kushirikiana naye kwa sasa kunategemea na hali atakayokuwa nayo. Ikiwa ametubu,

Mafunzo ya Hukmu za Ibada

ushirikiano na watu hawa ni sawa na ushirikiano na waumini wengine. Ama mtu anayefanya maovu na kukataza hakusaidii kitu isipokuwa kwa kumtenga au kukata uhusiano naye, basi itakuwa ni wajibu kufanya hivyo.

Kuvaa mapambo ya dhahabu na vidani kwa wanaume ni haramu, na pia kuvaa mavazi ambayo yanadhihirisha uigaji wa mila za kigeni haijuzu na lazima yakatazwe.

Kama mtu amelazimika kuishi na mtu asiyetaka kufanya mema kama swala, na mtu huyo anamsaidia katika baadhi ya kazi zake, itamlazimu daima kumlingania kufanya mema na hatakuwa na wajibu zaidi ya huo.

Ikiwa itathibitika kuwa mahusiano kati ya maulamaa na viongozi madhalimu yatasaidia kuondoa dhulma basi mahusiano hayo yanaruhusiwa.

Maswali

1. Taja tabaka za kuamrisha mema na kukataza maovu.
2. Je, inajuzu kutoitikia salamu ya mtu anayefanya haramu?
3. Je, watu wanaweza kufanya kazi ya kukataza maovu ikiwa kundi la watu walioteuliwa kwa kazi hiyo wameshindwa?
4. Nini wajibu wa jamaa ikiwa mmoja wao anafanya maovu na hana dalili ya kuongoka?
5. Ni upi uhusiano na watu ambao zamani walifanya maovu kama ulevi?
6. Nini wajibu wa mke kuhusiana na mumewe ambaye hajinasibishi na mas'ala ya dini ikiwemo swala?

Changamoto

Ni ipi njia sahihi na ya wajibu kwa mtoto ambaye wazazi wake hawampi umuhimu kutokana na itikadi potofu aliyonayo?

ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka Thalathini
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia

-
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu
 27. Al-Wahda
 28. Ponyo kutoka katika Qur'an.
 29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
 30. Mashukio ya Akhera
 31. Al Amali
 32. Dua Indal Ahlul Bayt
 33. Udhuu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna.
 34. Haki za wanawake katika Uislamu
 35. Mwenyeezi Mungu na sifa zake
 36. Amateka Na Aba'Khalifa
 37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
 38. Adhana.
 39. Upendo katika Ukristo na Uislamu
 40. Nyuma yaho naje kuyoboka
 41. Amavu n'amavuko by'ubushiya
 42. Kupaka juu ya khofu
 43. Kukusanya swala mbili
 44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara
 45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipya
 46. Kusujudu juu ya udongo
 47. Kusheherekea Maulidi Ya Mtume (s)
 48. Tarawehe
 49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
 50. Kupunguza Swala safarini
 51. Kufungua safarini
 52. Umaasumu wa Manabii
 53. Qur'an inatoa changamoto
 54. as-Salaatu Khayrun Mina -'n Nawm
 55. Uadilifu wa Masahaba
 56. Dua e Kumayl

-
57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu
 58. Umaasumu wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake
 59. Umaasumu wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata
 60. Umaasumu wa Mitume - Umaasumu wa Mitume
Muhammad (s)
 61. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Kwanza
 62. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Pili
 63. Kuzuru Makaburi
 64. Maswali Na Mishkili Eلفu - Sehemu ya Kwanza
 65. Maswali Na Mishkili Eلفu - Sehemu ya Pili
 66. Maswali Na Mishkili Eلفu - Sehemu ya Tatu
 67. Maswali Na Mishkili Eلفu - Sehemu ya Nne
 68. Maswali Na Mishkili Eلفu - Sehemu ya Tano
 69. Maswali Na Mishkili Eلفu - Sehemu ya Sita
 70. Tujifunze Misingi Ya Dini
 71. Sala ni Nguzo ya Dini
 72. Mikesha Ya Peshawar
 73. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
 74. Ubora wa Imam 'Ali Juu ya Maswahaba Na Ushia ndio njia
iliyonyooka
 75. Hukumu za Kifikihi zinazowahusu Wanawake
 76. Liqaa-u-llaah
 77. Muhammad (s) Mtume wa Allah
 78. Amani na Jihadi Katika Uislamu
 79. Uislamu Ulienea Vipi?
 80. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)
 81. Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)
 82. Urejeo (al-Raja'a)
 83. Mazingira
 84. Utokezo (al - Badau)
 85. Sadaka yenye kuendelea

-
86. Msahafu wa Imam Ali
 87. Uislamu na dhana
 88. Mtoto mwema
 89. Adabu za Sokoni
 90. Johari za hekima kwa vijana
 91. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Kwanza
 92. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Pili
 93. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Tatu
 94. Tawasali
 95. Imam Mahdi katika Usunni na Ushia
 96. Maana ya laana na kutukana katika Qur'ani Tukufu
 97. Hukumu ya kujenga juu ya makaburi
 98. Swala ya maiti na kumlilia maiti
 99. Shiya na Hadithi (kinyarwanda)
 100. Mariamu, Yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
 101. Hadithi ya ThaqaLain
 102. Fatima al-Zahra
 103. Tabaruku
 104. Sunan an-Nabii
 105. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)
 106. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Pili)
 107. Mahdi katika sunna
 108. Kusalia Nabii (s.a.w)
 109. Ujumbe -Sehemu ya Kwanza
 110. Ujumbe - Sehemu ya Pili
 111. Ujumbe - Sehemu ya Tatu
 112. Ujumbe - Sehemu ya Nne

-
113. Ngano ya kwamba Qur'ani imebadilishwa
 114. Iduwa ya Kumayili
 115. Maarifa ya Kiislamu.
 116. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza
 117. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
 118. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatu
 119. Ukweli uliopotea sehemu ya Nne
 120. Ukweli uliopotea sehemu ya Tano
 121. Johari zenye hekima kwa vijana
 122. Safari ya kuifuata Nuru
 123. Idil Ghadiri
 124. Myahudi wa Kimataifa
 125. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi
 126. Visa vya kweli sehemu ya Kwanza
 127. Visa vya kweli sehemu ya Pili
 128. Muhadhara wa Maulamaa
 129. Mwanadamu na Mustakabali wake
 130. Imam Ali binamu ya Mtume Sehemu ya Kwanza
 131. Imam Ali binamu ya Mtume Sehemu ya Pili
 132. Khairul Bariyyah
 133. Uislamu na mafunzo ya kimalezi
 134. Vijana ni Hazina ya Uislamu.
 135. Yafaayo kijamii
 136. Kusoma sura zenye Sijda ya wajibu
 137. Taqiyya
 138. Vikao vya furaha

-
139. Shia asema haya Sunni asema haya Wewe wasemaje?
 140. Uislamu na Mazingatio Sehemu ya Kwanza
 141. Uislamu na Mazingatio Sehemu ya Pili
 142. Azadari-Kuhuzunika na Kuomboleza
 143. Sunna katika Kitabu *Fiqhi al-Sunnah*
 144. Mtazamo Mpya - Wanawake katika Uislamu
 145. Kuonekana kwa Allah
 146. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt
(Sehemu ya Kwanza)
 147. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Pili)
 148. Ndugu na Jirani
 149. Ushia ndani ya Usunni
 150. Maswali na Majibu
 151. Elimu ya Ghaibu
 152. Ahlul Bayt ndani ya Tafsir za Kisunni No.1
 153. Ahlul Bayt ndani ya Tafsir za Kisunni No.2
 154. Ahlul Bayt ndani ya Tafsir za Kisunni No.3

Back Cover

Kitabu kilicho mkononi mwako kimekusanya maelezo yanayohitajika kiibada kulingana na fatwa za Ayatullah Sayyid Ali Khamenei. Japokuwa mas'ala yanayohusu ibada ni mengi, lakini hapa tumetaja yale tu yanayotumika mara kwa mara katika maisha ya kila siku. Kwa mapenzi ya Allah, tuna imani kuwa siku za usoni tutayaongeza ili tuyakamilishe kwa ajili ya wale wanaohitaji elimu ya juu katika hukmu za dini.

Kitabu hiki kimepangwa na kuandaliwa kwa ajili ya kufundishia ambapo kina sehemu 8 zenye jumla ya masomo 72. Katika kila somo kuna zoezi la maswali 6, ambapo jumla ya maswali ni 462 pamoja na utafiti 72. Majibu mengi ya utafiti yanaweza kupatikana katika kitabu kiitwacho *Risalatu Ajwibatu 'l-Istifta'aat* cha Ayatullah Sayyid Ali Khamenei kilichochapishwa na al-hudaa chapa ya kwanza, na kinapatikana katika ofisi za Ayatullah Khamenei.

Kimetolewa na kuchapishwa na:

Al-Itrah Foundation

S.L.P 19701 Dar es Salaam -Tanzania

Simu: +255 22 2110640

Simu / Nukushi: +255 22 2127555

Barua Pepe: alitrah@raha.com

Tovuti: www.alitrah.org

katika mtandao: www.alitrah.info

